ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR
MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Rashid Seif Suleiman	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ziwani.
9.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa

11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa
12.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Gando
13.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Kuteuliwa.
14.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Jang'ombe
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la Makunduchi
18. Mhe. Shawana Bukheti Hassan	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/ Jimbo la Dole
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu

22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka
23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake
29. Mhe. Mohammed Said Mohammed	Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/ Jimbo la Mpendae
30.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
31.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
32. Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa
33.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
34.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
35. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
36.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake

37. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
38.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
42.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
43.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
44.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
45.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
46.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
47.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
48.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu
49.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
50.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
51.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
52.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
53.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
54.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	Jimbo la Kiembesamaki
55.Mhe. Marina Joel Thomas	Kateuliwa na Rais
56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Jimbo la Mkwajuni
57.Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake
58.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma	Jimbo la Bumbwini

59.Mhe. Mohammed Haji Khalid Jimbo la Mtambile

60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad Jimbo la Chambani

61.Mhe. Mussa Ali Hassan Jimbo la Koani

62.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali Jimbo la Uzini

63.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa Nafasi za Wanawake

64.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi Nafasi za Wanawake

65.Mhe. Nassor Salim Ali Jimbo la Rahaleo

66.Mhe. Omar Ali Shehe Jimbo la Chake-Chake

67.Mhe. Panya Ali Abdalla Nafasi za Wanawake

68.Mhe. Raya Suleiman Hamad Nafasi za Wanawake

69.Mhe. Rufai Said Rufai Jimbo la Tumbe

70.Mhe. Saleh Nassor Juma Jimbo la Wawi

71.Mhe. Salim Abdalla Hamad Jimbo la Mtambwe

72.Mhe. Salma Mohammed Ali Nafasi za Wanawake

73.Mhe. Salma Mussa Bilali Nafasi za Wanawake

74.Mhe. Salmin Awadh Salmin Jimbo la Magomeni

75.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman Nafasi za Wanawake

76.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha Jimbo la Mwanakwerekwe
77.Mhe. Subeit Khamis Faki Jimbo la Micheweni
78.Mhe. Suleiman Hemed Khamis Jimbo la Konde
79.Mhe. Ussi Jecha Simai Jimbo la Chaani
80.Mhe. Viwe Khamis Abdalla Nafasi za Wanawake
81.Mhe. Wanu Hafidh Ameir Nafasi za Wanawake

Ndugu Yahya Khamis Hamad Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Thalathini na Nne – Tarehe 31 Julai, 2013

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma dua

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 – Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, kwanza namshukuru Allah kwa kutupa uhai, uzima na taufiki ya kufika hapa. Pili nikushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii. Makofi uliyoyasikia Mhe. Spika, ni dalili ya kukaribishwa *ex-back bencher* na mimi nayapokea Mheshimiwa. *(Makofi).*

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ili liweze kupokea, kuzingatia, kujadili na hatimae kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya fedha kwa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kwa kazi za kawaida na kazi za maendeleo kwa mwaka wa fedha 2013/2014. Aidha, naomba nimshukuru Muumba Wetu kwa kutujaalia uhai na afya njema ambayo imetuwezesha kushiriki katika kikao hichi.

Mhe. Spika, kabla ya kutoa maelezo ya hoja ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza na kumshukuru Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein kwa ushauri na miongozo anayoitoa kwa Wizara hii katika utekelezaji wa majukumu yake ya kila siku. Ushauri na miongozo hiyo inaendelea kusaidia katika kuongeza ufanisi wa kazi na kasi ya maendeleo ya sekta zinazosimamiwa na wizara yetu.

Mhe. Spika, napenda kuwapongeza Makamu wa Kwanza wa Rais Mhe. Maalim Seif Sharif Hamad na Makamu wa Pili wa Rais Mhe. Balozi Seif Ali Iddi kwa kumsaidia na kumshauri Mheshimiwa Rais kwa hekma katika utekelezaji wa majukumu mazito aliyonayo. Aidha, naomba kumpongeza na kumshukuru kwa dhati Makamu wa Pili wa Rais Mhe. Balozi Seif Ali Iddi, kwa kuendelea kuongoza vyema shughuli za serikali katika Baraza lako Tukufu na kusimamia utekelezaji wa shughuli za Serikali.

Mhe. Spika, napenda pia nikupongeze wewe binafsi kwa hekma, umahiri na busara zako unazozitumia katika kuliongoza Baraza hili Tukufu ambalo limekuwa likifanya maamuzi muhimu na magumu kwa manufaa ya nchi yetu. Maamuzi hayo yamethibitisha uwezo wa Baraza hili katika kusimamia demokrasia na utawala bora nchini.

Mhe. Spika, naishukuru pia Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ya Baraza la Wawakilishi chini ya uongozi wa Mwenyekiti wake Mhe. Mahamoud Muhamed Mussa, Mwakilishi wa Jimbo la Kikwajuni kwa maelekezo na ushauri ambao umeiwezesha Wizara yangu kusahihisha baadhi ya kasoro katika uwasilishaji wa hotuba hii. Kamati hiyo ilipata nafasi ya kutembelea taasisi mbali mbali ziliomo ndani ya Wizara ya Mindombinu na Mawasiliano na kutoa ushauri na maelekezo yenye lengo la kuimarisha utekelezaji wa majukumu yetu. Ushauri na maelekezo yao yataendelea kuzingatiwa kivitendo wakati wa utekelezaji wa bajeti hii.

Mhe. Spika, nitakuwa mpungufu wa shukrani kwa kutotambua uzito wa hoja zilizomo ndani ya hotuba za Waheshimiwa Mawaziri wenzangu walionitangulia ambazo zimetoa ufafanuzi wa kina kuhusu maendeleo ya utekelezaji wa sera, ukuaji wa uchumi, maendeleo ya jamii na matarajio yetu kwa kipindi kijacho cha 2013/2014. Vile vile, napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wawakilishi wenzangu waliochangia hoja hizo na kusaidia sana katika kukamilisha hotuba ya wizara yangu.

Mhe. Spika, hotuba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo Mheshimiwa Omar Yussuf Mzee wakati akiwasilisha bajeti ya Serikali, imefafanua kwa kina hali ya uchumi na fedha nchini na mwelekeo kwa kipindi kijacho cha mwaka 2013/2014. Hata hivyo, pamoja na mafanikio yalioelezwa bado tunatakiwa kuimarisha mikakati yetu ya utekelezaji wa Sera na Programu zilizopangwa ili kuongeza ubora wa maisha ya jamii ya Wazanzibari.

Mhe. Spika, hotuba ya Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais Mhe. Mohamed Aboud Mohamed pia ilifafanua hatua za utekelezaji wa *program* mbali mbali za serikali zenye lengo la kukuza na kuimarisha hali za wananchi hususan kuwaondolea; umaskini, elimu duni, maradhi na mazingira yasioridhisha. Niwaombe Waheshimiwa Wawakilishi waendelee kuishauri serikali pamoja na wizara yangu juu ya mbinu bora zitakazotufikisha kule tunakotarajia.

Mhe. Spika, Sekta ya Usafiri na Mawasiliano itaendelea kutoa mchango wake wa kuimarisha miundombinu ya kiuchumi zikiwemo; barabara, bandari na viwanja vya ndege sambamba na kuimarisha mifumo ya uendeshaji kwa

kushirikiana na sekta binafsi na wananchi katika kupanga, kuendeleza na kutoa huduma za usafiri na teknolojia ya habari na mawasiliano. Wizara itaendelea kutumia taratibu na miongozo mbali mbali ili kuhakikisha kwamba huduma za usafiri na mawasiliano zinazotolewa zinakua bora, zenye kuzingatia viwango vinavyokubalika na zenye gharama nafuu kwa wananchi.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013 Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano ilikadiriwa kutumia jumla shilingi 5,111,000,000/- kwa kazi za kawaida na shilingi 9,950,000,000/- kwa kazi za maendeleo. Aidha, Wizara ilipangiwa kukusanya jumla ya shilingi 394,500,000/-.

Hadi kufikia mwezi Juni 2013, jumla ya shilingi 4,140,534,030/- zilipatikana kwa matumizi ya kazi za kawaida sawa na asilimia 81 na shilingi 5,018,644,000/- kwa kazi za maendeleo sawa na asilimia 50. Aidha, wizara ilikusanya shilingi 394,336,150/- sawa na asilimia 99 *(Kiambatanisho Namba 1).*

UTEKELEZAJI WA BAJETI 2012/2013 NA MALENGO YA MWAKA 2013/2014

Mhe. Spika, katika mwaka 2012/2013, wizara yetu imeendelea kusimamia utekelezaji wa kazi zake za kawaida na za maendeleo kwa kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo (*Vision 2020*), Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUZA II), Sera ya Usafiri Zanzibar (2008), Mpango Mkuu wa Usafiri (*Zanzibar Transport Masterplan, 2009*) pamoja na Sera za sekta nyenginezo zinahusiana.

Katika kutekeleza Sera hizo, wizara imeendelea kushirikiana na wadau mbali mbali katika kuhakikisha upatikanaji wa uhakika wa usafiri wa baharini, nchi kavu na anga ambao ni salama, nafuu na wenye kukidhi matakwa ya watumiaji. Wizara pia imesimamia ukuaji wa huduma ya mawasiliano kwa mashirikiano na Sekta binafsi na taasisi nyenginezo.

Kwa ujumla wizara katika kipindi cha mwaka uliopita imesimamia kazi za ujenzi wa jumla ya barabara 10 zenye urefu wa kilometa 94.9 na madaraja 15, pamoja na kufanya matengenezo ya barabara 32 zenye urefu wa kilometa 61.5. Aidha, wizara kupitia mashirika na taasisi inazozisimamia imeendelea kusimamia uimarishaji wa hatua za kiusalama kwa upande wa usafiri wa nchi kavu, angani na baharini kwa kadri uwezo wa kifedha ulivyoruhusu.

Mhe. Spika, Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano inatekeleza majukumu yake moja kwa moja kupitia Idara zake za ndani, mamlaka ama mashirika yanayojitegemea, taasisi binafsi pamoja na baadhi ya taasisi za muungano.

Wizara imeendelea kutekeleza majukumu yake kupitia sekta kuu au taasisi zifuatazo:

i) Ofisi Kuu Pemba
ii) Utawala na Sera
    - Idara ya Mipango, Sera, na Utafiti,
    - Idara ya Uendeshaji na Utumishi.
iii) Sekta ya Usafiri wa Barabara
    - Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara,
    - Idara ya Usafiri na Leseni.
iv) Sekta ya Mawasiliano
    - Idara ya Mawasiliano,
    - Kampuni ya *ZANTEL*
    - Mashirika yalio chini ya Muungano.
v) Sekta ya Usafiri wa Anga:
    a. Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (*ZAA*),
    b. Mamlaka zilizo chini ya Muungano,
    c. Sekta Binafsi
vi) Sekta ya Usafiri wa Baharini
    a. Mamlaka ya Usafiri Baharini (*ZMA*).
    b. Shirika la Meli na Uwakala (*SHIPCO*).
    c. Shirika la Bandari (*ZPC*).

IIa) OFISI KUU PEMBA

Mhe. Spika, Ofisi Kuu Pemba inaratibu na kusimamia shughuli za Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kwa upande wa Pemba.

Katika kipindi cha 2012/2013 Ofisi kuu Pemba iliweza kutekeleza kazi zake za uratibu wa shughuli za Wizara kwa upande wa Pemba ikihusisha matengenezo ya barabara, utoaji wa leseni na ukaguzi wa magari, uimarishaji wa huduma katika kiwanja cha ndege, pamoja na kusimamia masuala ya utumishi na uendeshaji wa Ofisi Kuu. Utekelezaji wa miradi ya maendeleo utaelezwa kwa ufasaha zaidi katika maelezo ya Idara ya Mipango, Sera na Utafiti.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013 Ofisi Kuu Pemba ilikadiriwa kutumia jumla ya Tsh 1,356,800,000/- kwa kazi za kawaida na kukusanya jumla ya Shilingi 42,500,000/- kutoka kwenye vyanzo vyake vya mapato.

Hadi kufikia mwezi Juni 2013 fedha zilizopatikana zilikua ni Shilingi 1,074,213,688/- sawa na asilimia 79 na fedha zilizokusanywa zilikua shilingi 47,882,500/- sawa na asilimia 112 ya malengo.

Malengo ya Mwaka 2013/2014

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2013/2014, Ofisi Kuu Pemba inatarajia kutekeleza majukumu yake ya kazi za kawaida na kuratibu kazi za maendeleo kwa upande wa Pemba. Katika mwaka 2013/2014 Ofisi Kuu Pemba inakadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 50,200,000 na inaombewa jumla ya shilingi 1,277,000,000 kwa matumizi ya kazi za kawaida.

IIb) UTAWALA NA SERA

Mhe. Spika, kama ilivyo miundo ya wizara nyengine za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kazi ya uratibu wa kisekta ikiwemo sera, mipango na miradi ya maendeleo kwa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano husimamiwa chini ya Idara ya Mipango, Sera na Utafiti. Aidha, masuala ya uendeshaji, utumishi na utawala hutekelezwa kupitia Idara ya Uendeshaji na Utumishi.

(i) IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI

Mhe. Spika, **i**dara hii ina jukumu la kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Sera na Mipango ya Sekta za Usafiri na Mawasiliano. Idara pia inaratibu kazi zote za maendeleo za wizara zikiwemo kubuni, kutayarisha na kufuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Aidha, idara ina jukumu la kubuni na kufanya tafiti za kisekta ikiwemo ukusanyaji na uchambuzi wa takwimu.

HATUA ZA UTEKELEZAJI (2012/2013)

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka 2012/2013, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti iliratibu mchakato wa maandalizi ya Sera ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) ikishirikiana na wadau mbali mbali hadi kukamilika kwake na kuidhinishwa na serikali mwezi Mei 2013. Kukamilika kwa Sera ya TEHAMA ni hatua muhimu katika kuipatia Sekta ya Mawasiliano mwongozo wa usimamizi wa teknologia hiyo ambayo inakabiliwa na changamoto nyingi zinazoenda sambamba na kasi ya mabadiliko ya kiuchumi na kijamii duniani na hapa nchini.

Mhe. Spika, **w**izara kupitia programu ya mageuzi ya mfumo wa taasisi za wizara (*Institutional Reform)* inaendelea kufanya mapitio ya muundo wake na majukumu ya kila taasisi zilizomo ndani yake. Lengo kuu la programu hii ni kufanya mapitio na kuishauri serikali juu ya mfumo wa kiutawala na muundo bora wa wizara utakaoiwezesha Sekta ya Usafiri na Mawasiliano kufanyakazi kwa ufanisi zaidi. Programu hii inasimamiwa na timu ya wataalamu wa wizara pamoja na Kampuni ya *Intercontinental Technocrats* (*ICT*) ya India

ambayo hadi sasa imeshakusanya maoni ya wadau katika ngazi mbali mbali za Serikali na tayari imekwishatoa rasimu ya tatu ya ripoti yake ya kazi.

Mhe. Spika, wizara imeratibu mapitio ya Sheria mbali mbali za sekta ya usafiri na mawasiliano. Itakumbukwa kwamba kufuatia mapitio hayo, hivi karibuni Baraza lako tukufu liliweza kupitisha Sheria ya uanzishwaji Shirika la Meli na Uwakala 2013, marekebisho ya Sheria ya Usafiri Baharini (2006) na marekebisho ya Sheria ya Shirika la Bandari ya mwaka 1997.

Mhe. Spika, katika kipindi cha 2012/2013 Idara ya Mipango, Sera na Utafiti iliendelea kufuatilia taratibu za uanzishwaji wa vyuo maalum vya kufundisha wataalamu wa fani ya Urubani na Ubaharia hapa Zanzibar (*Establishment of Zanzibar Civil Aviation Academy and Zanzibar Maritime Training Institute).* Miongoni mwa hatua zilizochukuliwa ilikuwemo kutoa muongozo kwa Kampuni ya Danaos yenye Makao yake Makuu nchini Ugiriki katika mchakato wa kuanzisha Chuo cha Ubaharia kwa kufuata taratibu za uwekezaji kupitia Mamlaka na Taasisi husika.

(i-1) MIRADI YA MAENDELEO

Mhe. Spika, Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kupitia Idara ya Mipango Sera na Utafiti imetekeleza ama kufuatilia vyanzo vya fedha kwa jumla ya Miradi ya Maendeleo 14 katika Sekta za Barabara, anga na baharini (**Kiambatanisho Namba 2**) kama ifuatavyo:-

(i-1.1) MIRADI YA UJENZI WA BARABARA

Mhe. Spika, katika kipindi cha 2012/2013, wizara kupitia programu ya ujenzi wa barabara, iliendelea kutekeleza jumla ya miradi saba (7) ya ujenzi wa barabara. Kwa mwaka 2013/2014-inakusudia kuendelea na utekelezaji wa miradi hiyo na kuanza mradi 1 mpya. Taarifa za utekelezaji wa miradi hiyo na fedha inazoombewa kwa 2013/14 ni kama ifuatavyo:

(i-1.1.1) Mradi wa Barabara Tatu za Kaskazini Pemba

Mhe. Spika, mradi huu unaogharamiwa kwa pamoja baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Afrika (*BADEA*) na Mfuko wa Maendeleo wa Saudi Arabia (*Saudi Fund*) unazihusisha barabara za Wete – Konde (kilomita 15) na Wete – Gando (kilomita 15) kwa awamu ya kwanza. Awamu ya pili itahusisha ujenzi wa barabara ya Wete-Chake Chake kilomita 22.
Mhe. Spika, hatua za utekelezaji ni kuwa ujenzi wa barabara hizi umefikia hatua mbali mbali za kifusi. Hata hivyo, utekelezaji wa mradi huu umesita

kwa muda kutokana na kuchelewa kumlipa mkandarasi madai yake kwa wakati. Hadi kufikia mwezi Juni 2013, fedha zilizopatikana ni shilingi 2,310,829,904 sawa na asilimia 66 ya makadirio.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014 wizara inakusudia kuendelea na kazi za ujenzi wa barabara hizo kwa kulipatia ufumbuzi wa kudumu tatizo la malipo ya mkandarasi na jumla ya shilingi 3.073 Bilioni zinaombwa kutoka serikalini kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu.

(i-1.1.2) Mradi wa Barabara ya Wete-Chake-Chake

Mhe. Spika, kama nilivyokwisha eleza hapo awali, utekelezaji wa mradi huu utafanyika ikiwa ni awamu ya pili ya Mradi wa Barabara Tatu za Kaskazini Pemba na utakua na urefu wa kilometa 22. Jumla ya USD 23 milioni zinatarajiwa kutumika kwa kazi za ujenzi; kati ya hizo USD 10 milioni zitatolewa na benki ya *BADEA*, USD 10 milioni zitatolewa na *Saudi Fund* na USD 3 milioni ni mchango wa Serikali. Tayari Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeshatiliana saini ya mkopo wa USD 10 milioni na benki ya *BADEA* kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii ambapo juhudi za kukamilisha taratibu za kusaini mkopo na Mfadhili wa pili (*SAUDI Fund*) zinaendelea.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014 wizara inakusudia kuanza taratibu za kumpata Mshauri wa kufanya mapitio ya usanifu wa barabara na usimamizi wa ujenzi na hakuna fedha zinazoombwa kutoka serikalini kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu kutokana na kuwa utekelezaji wa hatua hii utagharamiwa kwa kutumia fedha za Mfadhili.

(i-1.1.3) Mradi wa Barabara ya Ole-Kengeja

Mhe. Spika, Mradi wa Barabara ya Ole-Kengeja unagharamiwa na Jumuiya ya Nchi zinazosafirisha Mafuta kwa wingi Duniani (*OPEC*) na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambao una lengo la kuijenga kwa kiwango cha lami barabara inayoanzia Ole hadi Kengeja yenye urefu wa kilomita 35. Kutokana na gharama za ujenzi kuwa kubwa kulingana na fedha zilizotengwa, wizara tayari imekubaliana na mfadhili wa mradi kuwa ujenzi wa barabara hizi ufanyike kwa kutumia nguvu kazi (*labour-base*) ambao utawezesha kujenga barabara yote kwa fedha zilizopo. Aidha, Serikali tayari imeshasaini mkataba na Mfuko wa Kimataifa wa Maendeleo (*OPEC Fund for International Development - OFID)*, kuandaa mpango kazi pamoja na kupitisha bajeti. Taratibu za kumpata Mshauri wa kusimamia mradi huo zinatarajiwa kukamilika katika siku chache zijazo.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014 serikali inakusudia kutekeleza Mradi huu kwa kufanya mapitio ya usanifu na kuanza ujenzi wa barabara hii na jumla ya shilingi 300 milioni zinaombwa kutoka serikalini kwa ajili ya malipo ya fidia.

(i-1.1.4) Mradi wa Barabara za Vijijini Kaskazini Pemba:

Mhe. Spika, mradi wa Barabara za Vijijini Kaskazini Pemba unagharamiwa kwa pamoja baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Marekani kwa kupitia Mfuko wa Changamoto ya Millenia (*MCC*). Mradi huu una lengo la kujenga kwa kiwango cha lami barabara 5 za Kaskazini Pemba zenye jumla ya kilometa 35. Barabara zinazohusika na Mradi huo ni:-

- Mzambarauni-Pandani-Finya (kilometa 7.9);
- Bahanasa-Daya-Mtambwe (kilometa 13.6);
- Chwale-Kojani (kilometa 1.9);
- Kipangani-Kangagani (kilometa 2.7); na
- Mzambarauni – Mapofu (kilometa 8.9).

Utekelezaji wa barabara hizi uko katika hatua mbali mbali za kifusi na lami na hadi sasa kazi za ujenzi zimefikia asilimia 61 na unatarajiwa kukamilika kabla ya mwisho wa mwaka huu (2013).

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014 jumla ya shilingi 150 milioni zinaombwa kutoka serikalini.

(i-1.1.5) Mradi wa Barabara Zinazoingia Mjini Unguja

Mhe. Spika, huu ni mradi wenye lengo la kujenga barabara 7 zenye urefu wa kilometa 78.5 zinazoingia katika mji wa Zanzibar. Mradi huu unaojumuisha ujenzi wa barabara za Bububu-Mtoni-Kinazini-*Malindi Port* (kilometa 19), *Creek road*-Mkunazini-Mnazi Mmoja (kilometa 1.2), Tunguu-Fuoni-Magomeni-Kariakoo - Mkunazini (kilometa 13.3), Welezo – Amani-Ng'ambo-Kariakoo (kilometa 3.5), Mtoni-Amani-Kiembe Samaki (kilometa 8.5), Uwanja wa Ndege-Kiembe Samaki – Kilimani-Mnazi Mmoja (kilometa 7) na Bububu-Mahonda-Mkokotoni (kilometa 31) bado haujapata mfadhili wa kugharamia ujenzi wake. Juhudi za kutafuta fedha za ujenzi wa barabara hizi kwa kiwango cha lami zinaendelea.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Mendeleo itaendelea na juhudi za kutafuta fedha kwa ajili ya msaada au mkopo kutoka kwa Washirika wa

Maendeleo kwa ajili ya utekelezaji wa mradi na unaombewa jumla ya shilingi 50 milioni kutoka serikalini.

(i-1.1.6) Mradi wa Barabara 3 za Vijijini Unguja

Mhe. Spika, huu ni mradi unaoendelea na unagharamiwa kwa pamoja baina ya Benki ya Kiarabu ya Maendeleo ya Afrika (*BADEA*) na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Mradi huu unazijumuisha barabara za Kizimbani-Kiboje (kilometa 7.2); Koani-Jumbi (kilometa 6.3); na Jendele-Cheju-Kaebona (kilometa 11.7). Hadi kufikia mwezi Juni 2013, jumla ya kilometa 7.5 za eneo la barabara zimesafishwa na ujenzi wa kifusi kwa tabaka la awali kilometa 2.5.

Kwa mwaka wa fedha 2013/2014, wizara inakusudia kuendelea na utekelezaji wa mradi huu na unaombewa jumla ya shilingi bilioni 2 kutoka serikalini.

(i-1.1.7) Mradi wa Barabara 6 za Vijijini Unguja

Mhe. Spika, mradi huu ni mpya na una lengo la kufanya upembuzi yakinifu, usanifu na utayarishaji wa zabuni wa barabara 6 za vijijini Unguja zenye jumla ya kilometa 62.6 na unagharimiwa kwa pamoja na Benki ya Maendeleo ya Afrika (*AFDB*) na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Mradi huu unazijumuisha barabara za Matemwe-Muyuni (kilometa 7), Kichwele-Pangeni (kilometa 4.8), Njianne-Umbuji-Uroa (kilometa 11), Jozani-Charawe-Ukongoroni-Bwejuu (kilometa 22.2), Fuoni-Kombeni (kilometa m 8.5) na Mkwajuni-Kijini (kilometa 9.1).

Kwa mwaka wa fedha 2013/2014, hakuna fedha zinazoombwa serikalini kwa vile utekelezaji wake kwa hatua hii ya awali utagharamiwa na mfadhili.

(i-1.2) MIRADI YA SEKTA YA USAFIRI WA ANGA

Mhe. Spika, kwa upande wa kazi za maendeleo wizara ilipanga kutekeleza miradi 4 katika viwanja vya ndege vya Unguja na Pemba kwa mwaka wa fedha 2012/2013. Utekelezaji wa miradi hiyo kwa kipindi kilichopita na fedha inazoombewa kwa mwaka ujao wa fedha uko kama ifuatavyo:-

(i-1.2.1) Uendelezaji Ujenzi wa Uzio.

Mhe. Spika, Mradi huu unalengo la kujenga uzio wenye urefu wa kilometa 11.9. Hadi kufikia mwezi Juni, 2013 jumla ya kilometa 7.6 za uzio zimeshajengwa sawa na asilimia 64 ya lengo.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014 wizara inakusudia kuendeleza mradi huu kupitia mradi wa ujenzi wa maegesho na utanuzi wa njia ya kupitia ndege.

(i-1.2.2) Ujenzi wa Jengo Jipya la Abiria Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume

Mhe. Spika, hili ndio *common* linalojulikana kwamba ni *Terminal II*. Mhe. Spika, Mradi huu unaoendelea una lengo la kujenga jengo jipya la abiria, maegesho ya ndege, maegesho ya magari pamoja na jengo la mitambo (*machine room*) na uwekaji wa vifaa mbali mbali katika kiwanja hicho. Mradi huu unagharamiwa kwa pamoja kati ya Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China kupitia Benki ya Exim ya China na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Spika, hatua za utekelezaji ni kwamba mkandarasi amekamilisha kazi za ujenzi wa "*steel structure*" ya jengo hilo na ujenzi wa "*structure*" ya jengo la vifaa na zana (*machine room)*. Hata hivyo, shughuli za mradi huu zililazimika kusitishwa kwa muda kuanzia tarehe 10 Januari 2013 kufuatia kubainika kwa kasoro kadhaa za kiufundi ambazo serikali iliona ni vyema kuchukua hatua ya kuzitafutia ufumbuzi zaidi wa kitaalamu ili kiwanja hicho kuweze kufikia hadhi ya kimataifa na ya kiushindani kwa viwanja vyengine vilivyo jirani.

Mhe. Spika, mnamo mwezi Machi 2013 wizara ilikamilisha taratibu za kumpata Mshauri Elekezi ambaye alianza kazi mwezi Aprili na kutoa ripoti yake ya mwisho mwezi Juni 2013. Baada ya kupokea ripoti hiyo ambayo ilionyesha namna ambavyo kasoro zilizojitokeza zingeweza kutatuliwa, wizara kupitia Kamati Maalum iliyoundwa na serikali kufuatilia suala hilo ilifanya juhudi za haraka kuwasiliana na Benki ya *Exim* ya China na kuwasilisha ombi la kuongeza muda wa mkopo ambao ungefikia ukingoni tarehe 31 Julai 2013. Aidha, serikali pia iliwasilisha ombi la fedha za ziada ya mkopo ili kugharimia ongezeko linalotokana na kubadilika kwa baadhi ya michoro ya jengo hilo na mazingira yanayolizunguka.

Mhe. Spika, kufuatia juhudi hizo na kwa niaba ya serikali napenda kutamka rasmi kwamba serikali imetoa rasmi ruhusa ya kuendelea na kazi za ujenzi chini ya Mkandarasi yuleyule ambae ni Kampuni ya *Beijing Construction Engineering Group (BCEG)* chini ya usimamizi wa Serikali kupitia Mshauri Muelekezi ambae ni Kampuni ya *ADPi* ya Ufaransa. Kazi ya ujenzi imeanza katikati ya mwezi huu (Julai 2013) wakati taratibu zote tulizokubaliana zikiendelea kukamilishwa.

Mhe. Spika, serikali inatarajia kupata mkopo wa ziada wa jumla ya Dola za Kimarekani 47,000 katika kukamilisha Mradi huo. Mchango wa Serikali kwa mradi huu hadi kufikia mwezi Juni 2013 ulifikia jumla ya Tsh 397,270,096 sawa na asilimia 79 ya makadirio zilipatikana.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014 wizara inakusudia kuendeleza mradi huu na jumla ya Tsh bilioni 1.360 zinaombwa kutoka Serikalini kwa ajili ya huduma ya ushauri na usimamizi wa mradi.

Ujenzi wa Maegesho na Njia ya Kupitia Ndege uwanja wa ndege wa Kimataifa.

Mhe. Spika, mradi huu unaendelea na una lengo la ujenzi wa sehemu ya maegesho *apron* na kuimarisha njia za kupitia ndege *taxiways* katika Kiwanja cha Ndege cha kimataifa cha Abeid Amani Karume. Mradi huu unagharamiwa na Benki ya Dunia na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Hadi kufikia mwezi Juni 2013, maendeleo ya mradi huu yalifikia asilimia 52 ambapo kazi za ujenzi wa njia na eneo la kupitia ndege zimeendelea kwa hatua mbali mbali. Jumla ya Tsh. milioni 500 zilipatikana kutoka Serikalini.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Wizara inakusudia kuendeleza mradi huu na jumla ya Tsh. bilioni 2.716 zinaombwa kutoka Serikalini.

Uimarishaji wa huduma za Uwanja wa Ndege Pemba.

Mhe. Spika, mradi huu unagharamiwa na Serikali ya Mapinduzi pekee na unalengo la kuweka taa katika barabara ya kurukia na kutulia ndege na kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa huduma mbali mbali katika kiwanja hicho. Hadi kufikia mwezi Juni 2013, taratibu za kumpata Mshauri zimeendelea kwa kutoa matangazo ya kuyaalika makampuni mbali mbali kuleta maombi ya awali ya kuonesha nia na uwezo wa kufanya kazi hiyo. Kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Wizara inaomba jumla ya Tsh 2.7 bilioni kugharamia mradi huu.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Wizara inakusudia kuendelea na utekelezaji wa miradi hiyo niliyokwisha kuieleza kwenye sekta ya usafiri wa Anga ambapo jumla ya Tsh 6.7 bilioni zinaombwa kutoka Serikalini.

Mhe. Spika, kwa upande wa kazi za maendeleo, Idara imeendelea kuratibu, kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa miradi 13 ya maendeleo inayohusisha Sekta za usafiri wa nchi kavu na anga. Aidha, Idara inaendelea na juhudi za kuwasiliana na Washirika wa Maendeleo kwa lengo la kutafuta fedha za kutekeleza miradi ifuatayo:-

- Mradi wa Barabara Kuu zinazoingia mjini (Zanzibar Town Entry Roads Project);
- Mradi wa Ujenzi wa Bandari ya Mpigaduri;
- Mradi wa Uimarishaji Uwanja wa Ndege wa Pemba.

Kufuatia juhudi hizo, Serikali tayari imetiliana saini Hati ya Makubaliano *Memorandum of Understanding* kati yake na Kampuni ya *China Harbour Engineering Company (CHEC)* ambayo itashirikiana na Serikali katika kufanya Upembuzi yakinifu na Usanifu wa Ujenzi wa Bandari hiyo sambamba na jitihada za kutafuta mkopo kwa ajili ya kazi za ujenzi. Jumla ya Tsh. bilioni 1.2 zinaombwa kutoka Serikalini katika mwaka ujao wa fedha (2013/2014) kwa ajili mradi huo.

Mhe. Spika, katika mwaka 2012/2013 Idara ya Mipango, Sera na Utafiti ilipangiwa kutumia jumla ya Tsh 250,000,000 kwa matumizi ya kazi za kawaida. Hadi Juni 2013, fedha zilizopatikana kwa kazi za kawaida zilikua ni Tsh 108,007,210 sawa na asilimia 43.

MALENGO YA IDARA (2013/2014)

Mhe. Spika, kwa upande wa kazi za kawaida kwa mwaka 2013/2014, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti kwa mashirikiano na Idara na Taasisi husika zilizo ndani na nje ya Wizara itaratibu mambo makubwa yafuatayo:-

- Ukamilishaji wa marekebisho ya Sheria ya Barabara – *Road Act (Cap 134* ya mwaka 1927);
- Kuandaa Sheria, Kanuni na Mpango Mkakati wa utekelezaji wa Sera ya TEHAMA;
- Kuibua maeneo ya utafiti katika sekta ya usafiri na mawasiliano kwa lengo la kuongeza ufanisi na tija katika kazi za ujenzi wa miundombinu;
- Kuanzisha mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini ya utekelezaji miradi ya maendeleo;
- Kusimamia mpango wa Serikali wa kuanzisha Chuo cha Ubaharia na Urubani;
- Kukusanya na kuchambua takwimu za maendeleo ya Sekta na kuweka mpango bora wa utunzaji wa kumbukumbu;
- Kuimarisha utoaji wa taarifa muhimu juu ya kazi za Wizara sambamba na kuanzisha utoaji wa vijarida na matoleo ya robo mwaka; na
- Kuratibu mashirikiano ya kisekta baina ya taasisi za ndani, kikanda na nje ya nchi.

Mhe. Spika, **k**wa mwaka 2013/2014 Idara ya Mipango, Sera na Utafiti inaombewa jumla ya Tsh 288,000,000 kwa matumizi ya kazi za kawaida.

Mhe. Spika, kwa upande wa kazi za maendeleo katika mwaka wa fedha wa 2013/2014 Idara itaendelea kuratibu na kufuatilia utekelezaji miradi ya maendeleo kwa kushirikiana na wataalamu wa Sekta husika.

IDARA YA UTUMISHI NA UENDESHAJI

Mhe. Spika, Idara ya Uendeshaji na Utumishi inaendelea na kusimamia majukumu yake ikiwemo kusimamia masuala kiutumishi shughuli zote za uendeshaji wa ofisi, uwekaji kumbukumbu za wafanyakazi na mali za Wizara, uimarishaji wa mazingira mazuri ya utendaji wa kazi kwa kuhakikisha vitendea kazi vinapatikana kwa wakati, kukuza na kuimarisha mawasiliano ya habari na ofisi nyingine. Aidha, Idara inajukumu la kuhakikisha Sheria ya Utumishi wa Umma inasimamiwa vizuri pamoja na Sheria ya Manunuzi na Uondoshaji wa mali chakavu za Serikali zinafuatwa. Idara pia inajukumu la kuwaendeleza wafanyakazi wa Wizara kwa kuwajengea uwezo kielimu na kusimamia maslahi yao.

HATUA ZA UTEKELEZAJI (2012/2013)

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013 Idara imetekeleza na kusimamia masuala ya kiutumishi na uendeshaji ya wizara kwa kuimarisha mazingira mazuri ya kazi kwa kuhakikisha upatikanaji wa vifaa vyote muhimu vya kutendea kazi vimepatikana. Aidha, vespa mbili zimenunuliwa ili kurahisisha usafiri kwa watumishi katika utekelezaji wao wa majukumu ya kazi.

Mhe. Spika, Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kwa kushirikiana na Wizara ya Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora imekamilisha kazi ya kutayarisha muundo wa utumishi wa Wizara na hivi sasa Wizara inakamilisha zoezi la kuwapangia wafanyakazi majukumu yao ya kazi kwa mujibu wa elimu zao na kupatiwa nyongeza zao za kila mwaka kwa wale wanaostahiki kupitia Wizara ya Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha unaomalizika jumla ya wafanyakazi 52 (38 Unguja na 14 Pemba) wamestaafu kwa mujibu wa Sheria za utumishi Serikalini, na kupatiwa mafao yao kwa mujibu wa sheria. Aidha, wafanyakazi 5 walifariki dunia (Mwenyezi mungu azilaze roho zao mahali pema peponi Amin). Vile vile, katika kipindi cha 2012/2013 Wizara imeajiri wafanyakazi wapya 20 wenye taaluma mbali mbali Unguja na Pemba kwa lengo la kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa kazi.

Mhe. Spika**,** katika lengo la kuwasaidia wafanyakazi wake kujikwamua kimaisha, Wizara imeendelea kuwadhamini wafanyakazi wake kupata mikopo kupitia mabenki mbali mbali yaliyopo hapa nchini hususan Benki ya Watu wa Zanzibar. Jumla ya wafanyakazi 175 walinufaika na mikopo hiyo kwa kipindi

cha mwaka uliopita. Kwa niaba ya Serikali Wizara inatoa shukurani za dhati kwa Benki ya *PBZ*, Benki ya Posta na Benki ya *FBME* kwa kuendelea kuwakopesha wafanyakazi wetu bila masharti magumu pale wanapohitaji huduma hiyo.

Mhe. Spika, katika kuwajengea uwezo wa kitaaluma watendaji wake Wizara imeendelea kutoa fursa za masomo kwa mujibu wa uwezo wake. Hadi sasa jumla ya wafanyakazi 89 wanaendelea kupatiwa mafunzo ndani na nje ya nchi katika viwango tofauti. Aidha, jumla ya wafanyakazi 15 waliokuwa masomoni mwaka jana wamerudi baada kuhitimu mafunzo yao. Kwa mwaka ujao wa fedha Wizara imepanga kuwapeleka wafanyakazi 15 kwa Unguja na wafanyakazi 9 kwa Pemba katika vyuo vya ndani na nje ya Nchi kupata mafunzo mbali mbali yatakayoongeza uelewa katika utendaji wao wa kazi kwa lengo la kuongeza ujuzi na ufanisi wa kazi zao.

Mhe. Spika, kwa upande wa elimu ya kijamii Wizara kupitia Idara ya Uendeshaji na Utumishi imeendelea na jitihada za kuwaelimisha wafanyakazi wake na wadau wa sekta yetu umuhimu wa kujikinga na maambukizi mapya ya virusi vya UKIMWI. Katika mwaka uliopita "*TAC member*" ya Wizara imeundwa upya na waliochaguliwa wamepatiwa mafunzo ili waweze kutekeleza vyema majukumu yao. Aidha, mikutano ya kawaida ya utekelezaji wa kazi na semina mbali mbali kwa watendaji wa wizara imefanyika kama ilivyopangwa.

Mhe. Spika, kwa upande wa vikao vya mashirikiano na Wizara na Taasisi za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, jumla vikao 4 vimefanyika katika ngazi ya Wizara na taasisi zinazofanyakazi na Wizara yetu huko Tanzania Bara ikiwemo ziara ya wajumbe wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ya Baraza la Wawakilishi kwenye taasisi hizo.

Mhe. Spika, Idara ya Utumishi na Uendeshaji imeendelea kuratibu huduma ya manunuzi kupitia kitengo chake cha manunuzi na uhifadhi wa vifaa ambapo jumla ya zabuni 11 zilitangazwa kitaifa na kimataifa kwa ajili ya kuwapata wakandarasi na watoa huduma kwa lengo la kufanikisha miradi ya ujenzi na utekelezaji wa kazi za Wizara. Kwa mwaka ujao wa fedha kitengo hicho kimejidhatiti kutekeleza kazi zake kwa ufanisi zaidi ili kuongeza tija. Aidha, kazi za utunzaji wa kumbukumbu za manunuzi, mali na matumizi ya fedha zitaendelea kuimarishwa.

Mhe. Spika, Wizara kupitia kitengo cha uhasibu imekamilisha taarifa ya mahesabu ya mwaka 2012/2013 pamoja na kuandaa makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara kwa mwaka 2013/2014. Aidha, kitengo cha ukaguzi wa ndani kimekamilisha ukaguzi wa taasisi zote zilizo chini ya Wizara. Taarifa

ya ukaguzi huo tayari imewasilishwa kwa uongozi wa Wizara kwa mazingatio na hatua za kufaa.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2012/2013 Idara ya Uendeshaji na Utumishi ilipangiwa kutumia jumla ya Tsh 475,000,000 kwa matumizi ya kazi za kawaida na Tsh 2,178,000,000 kwa mishahara ya watumishi wote wa Wizara. Fedha halisi zilizotolewa katika kipindi cha Julai 2012 hadi Juni 2013 ni Tsh. 331,104,280 sawa na asilimia 70 ya bajeti kwa matumizi ya kawaida na Tsh 2,178,126,012 sawa na asilimia 93 kwa matumizi ya mishahara.

MALENGO YA IDARA (2013/2014)

Mhe. Spika, Idara itaendelea kutekeleza masuala ya kiutumishi na Uendeshaji ya Wizara. Idara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora itakamilisha muundo wa utumishi wa wizara ambapo wafanyakazi watapandishwa madaraja hatua kwa hatua na kupangiwa kazi kwa mujibu wa taaluma walizonazo. Aidha, Idara itasomesha wafanyakazi kozi mbali mbali kwa mujibu wa mahitaji ya Wizara.

Katika mwaka 2013/2014, Idara ya Uendeshaji na Utumishi inaombewa jumla ya Tsh 475,000,000 kwa matumizi ya kazi za kawaida na Tsh 2,082,000,000 kwa mishahara.

SEKTA YA USAFIRI WA NCHI KAVU

Mhe. Spika, Sekta ya Usafiri wa Nchi kavu imeendelea kuimarika katika kufanikisha shughuli za kiuchumi na kimaendeleo ya jamii katika nchi yetu. Ukweli ni kwamba sekta hii inatumiwa na wananchi wengi zaidi katika usafirishaji wa abiria na mizigo baina ya mijini na vijijini.

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka 2012/2013, Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano imeendelea na jukumu lake la kusimamia huduma za usafiri wa barabara kwa kuendeleza ujenzi na utunzaji wa barabara, madaraja na pia kusimamia vizuri zaidi masuala ya usalama barabarani. Majukumu hayo yanatekelezwa na Idara ya Ujenzi na Utunzaji Barabara pamoja na Idara ya Usafiri na Leseni.

IDARA YA UJENZI NA UTUNZAJI WA BARABARA

Mhe. Spika, Idara ya Ujenzi na Utunzaji Barabara ina jukumu la kuzijenga na kuzitunza barabara za hapa nchini kupitia Wakandarasi wa ndani na nje ya nchi. Kazi za matengenezo ya barabara hufanywa na Idara yenyewe kwa kutumia Wakandarasi wetu wazalendo. Idara pia inasimamia uendeshaji na matengenezo ya zana nzito na mitambo ya ujenzi wa barabara zilizopo katika Karakana ya Matengenezo ya Mitambo na zana Saateni.

Aidha, Idara inamiliki kware mbili zilizopo Kengeja na Vitongoji kwa upande wa Pemba na Kibele kwa Unguja. Kware za Vitongoji na Kibele zina mitambo ya kutolea kokoto na kupika lami.

HATUA ZA UTEKELEZAJI (2012/2013)

Mhe. Spika, hadi kufikia mwezi Juni 2013, Idara hii iliweza kuzifanyia matengenezo jumla ya barabara 32 zenye urefu wa kilometa 61.5, mijini na vijijini (Unguja na Pemba) na kufanya usafi wa barabara za lami kilometa 610 kwa kutumia fedha zinazotolewa na Mfuko wa Barabara chini ya Makubaliano Maalum ya Utekelezaji *Performance Agreement* kati ya wizara na Mfuko huo.

Mhe. Spika**,** kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara ilipangiwa kukusanya jumla ya Tsh 6,000,000 kutokana na mapato mengineyo na ilitengewa jumla ya Tsh 300,000,000 kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida. Hadi Juni 2013 jumla ya Tsh 6,650,000 zimekusanywa ambazo ni sawa na asilimia 118 na fedha zilizotolewa kwa kazi za kawaida ni Tsh 177,705,560 sawa na asilimia 59 ya makadirio.

MATENGENEZO YA BARABARA

Mhe. Spika, katika kipindi cha 2012/2013, Wizara kupitia programu ya matengenezo ya barabara, iliendelea kutekeleza jumla ya miradi 3 ya ujenzi wa barabara. Kwa mwaka 2013/2014 Wizara inakusudia kuendeleza miradi hiyo na kuanza 2 mipya kama ifuatavyo:

Barabara ya Mgagadu-Kiwani

Mhe. Spika**,** mradi huu unagharamiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na una lengo la kuijenga barabara ya Mgagadu-Kiwani yenye jumla ya kilometa 7.6. Hadi kufikia mwezi Juni 2013 jumla ya kilometa 7.6 zimekamilika kwa hatua ya kifusi tabaka mbali mbali. Fedha zilizopatikana ni Tsh187,000,000 sawa na asilimia 47 ya makadirio.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Wizara inakusudia kuendelea na kazi za ujenzi wa barabara hii na jumla ya Tsh 1.3 bilioni zinaombwa kutoka Serikalini.

Barabara ya Mkanyageni-Kangani

Mhe. Spika, mradi huu una lengo la kuijenga barabara inayoanzia Mkanyageni hadi Kangani yenye urefu wa kilomita 6.5 kwa kiwango cha lami. Mradi huu umepangwa kutekelezwa baada ya kukamilika kwa barabara ya Mgagadu-Kiwani na unagharamiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014 jumla ya Tsh milioni 50 zinaombwa kutoka Serikalini kwa ajili ya kuifanyia marekebisho madogo madogo barabara hii ili iweze kupitika kabla ya ujenzi kuanza.

Barabara ya Amani-Mtoni (Benjamin Mkapa)
Mhe. Spika, huu ni mradi unaoendelea na Wizara inalenga kukamilisha ujenzi wa sehemu ya pili ya barabara hiyo yenye jumla ya urefu wa kilometa 4. Hadi sasa jumla ya kilometa 2.2 zimekamilika kwa kiwango cha lami pamoja na ujenzi wa kalvati, mitaro ya maji ya mvua na uwekaji kifusi urefu wa 0.8 km.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Wizara inakusudia kukamilisha ujenzi wa sehemu iliyobaki. Hakuna fedha zinazoombwa kutoka mfuko wa Serikali kupitia Wizara kwa vile ujenzi wake utaendelea kugharamiwa kupitia Mfuko wa Barabara.

Barabara ya Ole-Konde.
Mhe. Spika, mradi huu unagharamiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni mpya na una lengo la kuifanyia matengenezo ya muda maalum *Periodic maintenance* barabara inayoanzia Melitano Mchangamdogo hadi Madenjani kwa urefu wa kilometa 10.
Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Wizara inakusudia kutekeleza mradi huu na hakuna fedha zinazoombwa kutoka mfuko mkuu wa Serikali kwa vile ujenzi wake utagharamiwa kupitia Mfuko wa Barabara.

Barabara ya Njianne-Umbuji
Mhe. Spika, mradi huu unagharamiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na una lengo la kuifanyia matengenezo ya muda maalum *Periodic maintenance* kwa kiwango cha lami barabara inayoanzia Njianne hadi Umbuji yenye urefu wa kilometa 5.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Wizara inakusudia kutekeleza mradi huu na hakuna fedha zinazoombwa kutoka mfuko mkuu wa Serikali kwa vile ujenzi wake utagharamiwa kupitia Mfuko wa Barabara.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014 wizara inakusudia kukamilisha ujenzi wa barabara zilizosalia kupitia miradi mbali mbali inayofadhiliwa na Serikali kupitia Mfuko wa Barabara. Jumla ya Tsh 6.923 bilioni zinaombwa kwa ajili ya utekelezaji wa mpango wa maendeleo katika sekta ya barabara.

Aidha, Idara kupitia Mfuko wa Barabara itaendelea kuzitunza na kuzifanyia matengenezo barabara mbali mbali za mijini na vijijini Unguja na Pemba ili ziendelee kupitika kwa wakati wote na kuwarahisishia wananchi usafiri.

Mhe. Spika, kwa mwaka 2013/2014 Idara ya Ujenzi na Utunzaji Barabara inatarajia kukusanya jumla ya Tsh 10,000,000 na inaombewa jumla ya Tsh 1.304 bilioni kwa matumizi ya kazi za kawaida.

Mhe. Spika, katika kutekeleza mpango wa Serikali wa kupambana na umasikini na kuishirikisha sekta binafsi Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kupitia Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara imeendelea na utaratibu wa kutoa baadhi ya kazi kwa kampuni binafsi, vikundi vya jamii na jumuiya zisizo za Serikali.

Mhe. Spika**,** kwa hivi sasa kazi zinazotolewa ni za ujenzi wa madaraja madogo madogo, ukataji majani, usafishaji wa misingi ya maji na usafishaji wa kalvati, matengenezo madogo madogo na kazi nyenginezo. Ni matumaini yetu kwamba utaratibu huu utajenga msingi mzuri wa utekelezaji wa sera ya ushirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi. Aidha, Wizara kupitia Mpango wa Mageuzi ya Mfumo wa Kitaasisi inakusudia kuweka mikakati ya kujenga uwezo wa kampuni hizo ili hapo baadae ziweze kushiriki kikamilifu katika ujenzi wa barabara zinazotekelezwa kupitia miradi mikubwa.

MALENGO YA IDARA (2013/2014)

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Idara itaendelea kuzifanyia matengenezo barabara ili ziendelee kutumika kwa wakati wote.

IDARA YA USAFIRI NA LESENI

Mhe. Spika, Idara hii ina majukumu ya kusimamia usalama wa watumiaji wote wa barabara, kuendesha shughuli za ukaguzi wa vyombo vya moto, usimamizi wa mafunzo ya udereva, upasishaji madereva na walimu wa skuli za udereva, kusimamia utoaji huduma za usafirishaji abiria na mizigo kwa njia ya barabara. Majukumu haya ya Idara yanatekelezwa kwa mujibu wa Sheria ya Usafiri wa Barabarani nambari 7 ya mwaka 2003.

Aidha, Idara inasimamia na kuendesha Karakana Kuu ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iliyoko Chumbuni na sehemu ya mitambo iliyoko Pemba.

HATUA ZA UTEKELEZAJI (2012/2013)

Mhe. Spika, hadi kufikia mwezi Juni 2013 jumla ya vyombo 35,756 vimekaguliwa ukilinganisha na vyombo 32,700 vilivyokaguliwa katika kipindi cha mwaka 2011/2012.

Aidha, katika kipindi hicho Idara ilitoa ruhusa za njia 2,421 kwa magari ya biashara mbali mbali Unguja na Pemba, ikiwemo magari ya shamba, daladala,

private hire, taxi, magari ya wanafunzi, magari ya wafanyakazi na magari ya mizigo.

Mhe. Spika**,** Idara iliwafanyia mitihani ya nadharia na vitendo jumla ya madereva wanafunzi wa magari na vyombo vya moto wapatao 7,143 waliohitimu katika skuli mbali mbali za udereva. Aidha, katika kipindi hicho jumla ya leseni 8,766 zimetolewa kwa madereva wanafunzi wa madaraja mbalimbali ukilinganisha na leseni za madereva wanafunzi 6,980 zilizotolewa katika kipindi kama hicho cha 2011/2012.

Idara pia imeendesha vipindi mbali mbali kuhusiana na usalama barabarani elimu kwa umma kwa kutumia vyombo vya habari.

Mhe. Spika, Karakana Kuu na Sehemu ya Mitambo Pemba iliyafanyia matengenezo jumla ya magari 769 katika kipindi cha Julai 2012 hadi Juni 2013 ukilinganisha na gari 548 zilizotengenezwa katika kipindi kama hicho mwaka 2011/2012. Hata hivyo, kwa kutambua nafasi ya Karakana Kuu katika kuchangia mapato ya Serikali, Wizara imeandaa waraka maalum na kuuwasilisha Serikalini ili kupata ridhaa ya kuendelea na mpango wa kuibinafsisha ama kuweka ubia na wawekezaji kutoka Sekta Binafsi.

Mhe. Spika**,** katika mwaka wa fedha 2012/13 Idara ilipangiwa kukusanya jumla ya Tsh. 346,000,000 na kutumia jumla ya Tsh. 300,000,000 kwa kazi za kawaida. Hadi kufikia Juni 2013, Idara ilikusanya jumla ya Tsh. 339,833,650 sawa na asilimia 98 na iliingiziwa jumla ya Tsh. 166,017,800 kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 55 ya makadirio.

Katika kutekeleza majukumu yake Idara inaendelea kukabiliwa na changamoto kadhaa ikiwemo uchakavu wa jengo la Idara, ukosefu wa mtambo wa kisasa wa kutolea nyaraka za huduma ya usafiri na kukosekana kwa jengo lenye vifaa vya upasishaji magari.

MALENGO YA IDARA (2013/2014)

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2013/2014, Idara itaendelea kushajiisha na kusimamia matumizi bora ya barabara yenye kuongeza usalama wa watumiaji wa barabara kwa kuendelea kutoa elimu na kuimarisha ukaguzi wa vyombo vya moto. Idara pia itazingatia na kutekeleza maagizo ya Bodi ya Usafiri Barabarani na Kamati ya Kitaifa ya Wiki ya Usalama Barabarani katika kuimarisha usalama barabarani ili kupunguza majeruhi na vifo vinavyotokana na ajali za barabarani.

Mhe. Spika**,** juhudi zitachukuliwa za kuhakikisha Karakana Kuu ya Unguja na Sehemu ya Mitambo Pemba zinaimarishwa kwa kupatiwa vifaa vya kisasa na wafanyakazi wenye ujuzi kwa kushirikiana na Sekta Binafsi mara tu itakapopatikana ridhaa kutoka Serikalini kwa mujibu wa utaratibu uliowekwa. Idara pia, imepanga kuyafanyia matengenezo magari ya kisasa na vyombo vya moto kwa kutumia teknolojia ya kisasa.

Mhe. Spika, kwa mwaka 2013/2014 Idara ya Usafiri na Leseni inatarajia kukusanya jumla ya Tsh. 346,000,000 na inaombewa jumla ya Tsh. 300,000,000 kwa matumizi ya kazi za kawaida.

SEKTA YA MAWASILIANO

Mhe. Spika**,** Sekta ya Mawasiliano inatoa mchango mkubwa katika kuimarisha huduma za kiuchumi na kijamii na inajumuisha utoaji wa huduma za mawasiliano kwa njia za posta, simu na huduma za teknolojia ya habari na mawasiliano.

IDARA YA MAWASILIANO

Mhe. Spika, Idara hii ina jukumu la kusimamia huduma za mawasiliano na masuala ya taasisi za mawasiliano za Serikali ya Muungano ziliopo Zanzibar. Idara pia, ina jukumu la kuratibu na kusimamia uwekaji wa miundombinu ya mawasiliano.

HATUA ZA UTEKELEZAJI (2012/2013)

Mhe. Spika, kwa mwaka 2012/2013 Idara iliendelea kutekeleza majukumu yake kama kawaida ikiwemo kutoa mchango wa kiufundi katika maandalizi ya Sera ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, kutoa ushauri na muongozo katika uwekaji wa miundombinu ya mawasiliano kama vile mkonga wa taifa, ujenzi wa minara ya simu, mabadiliko ya teknolojia na uwekaji wa anuani za makaazi na simbo za Posta.

Aidha, Idara ilifanya ukaguzi na usimamizi wa utumiaji wa minara ikiwemo ya simu na internet. Jumla ya minara 229 kutoka makampuni mbali mbali yakiwemo *Zantel*, *Airtel*, Tigo, *Vodacom*, *TTCL*, *Excelent com*, *Zanlink*, *Zanzibar Connection*, *Zanzinet*, *ZBC*, *HTT*, *Agape*, *Chuchu FM*, Shirika la Bandari na SMZ.

MALENGO YA IDARA (2013/2014)

Mhe. Spika, Kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Idara itaendelea kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa Sekta ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano hapa Zanzibar, kuandaa Sheria na kanuni za *TEHAMA* na Mpango Mkakati wa *TEHAMA* kwa mashirikiano na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti. Vile vile, Idara itaandaa Kanuni za Miundombinu ya Mawasiliano ili tuweze

kusimamia, kudhibiti na kukusanya mapato kupitia minara na mikonga ya mawasiliano kwa wanaomiliki.

Mhe. Spika, Idara pia itakuwa na jukumu la kusimamia mkonga wa mawasiliano kwa kushirikiana na Kampuni ya Zantel kwa upande wa matumizi ya Serikali na taasisi binafsi. Ni matarajio yetu kwamba baada ya kukamilika kwa hatua zote muhimu na mkonga kuanza kufanyakazi, Zanzibar itaondokana na usumbufu wa matumizi yote ya *TEHAMA*.

Mhe. Spika, napenda kuchukua fursa hii kuwathibitishia wananchi na wadau wote watakaotumia huduma za mkonga huo kwamba usimamizi, udhibiti na matumizi ya mkonga huo utafanywa kwa umakini mkubwa kwa ushirikiano wa kitaalamu kati ya Serikali na Kampuni ya Zantel.

Mhe. Spika, kwa mwaka 2012/2013, Idara ya Mawasiliano ilipangiwa kutumia jumla ya Tsh 175,000,000 na hadi Juni 2013 fedha iliyopatikana ilikua ni Tsh. 104,294,460 sawa na asilimia 60 ya makadirio.

Mhe. Spika**,** katika kipindi cha mwaka 2013/2014 Idara inaombewa jumla ya Tsh. 255,600,000 kwa ajili ya kazi za kawaida.

KAMPUNI YA *ZANTEL*

Mhe. Spika, Kampuni ya Zantel imeanzishwa hapa Zanzibar na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ina hisa ya asilimia 18. Kampuni hiyo inatoa huduma za simu za mkononi Tanzania na inaendelea kuimarisha huduma zake kwa wateja kwa kuongeza vituo vya huduma Zanzibar.

Mhe. Spika**,** mnamo mwaka 2012/2013 Kampuni hii imeendelea kutoa huduma za simu za mkononi hapa nchini ambapo katika kipindi cha miaka 13 iliyopita *Zantel* imefanikiwa kujenga vituo vya minara ya mawasiliano itumiayo teknolojia ya *GSM/GPRS/EDGE* na minara 80 itumiayo teknolojia ya kisasa ya 3G pamoja na minara 13 ya *CDMA* kwa thamani ya Dola za Kimarekani milioni 32. Kampuni ya Zantel ina mpango wa kupanua mtandao wake kwa kuwekeza Dola za Kimarekani milioni 30.

Mipango na Mafanikio ya Kiufundi

Mhe. Spika, Kampuni ya Zantel imeshajenga minara 720 Tanzania hivi sasa; kati ya hiyo 141 ipo hapa Zanzibar na idadi iliyobakia ipo Tanzania Bara. Aidha, juhudi za kuongeza idadi ya minara zinaendelea kutokana na mahitaji makubwa ya minara hapa nchini. Kwa lengo la kutimiza mahitaji ya wateja, Zantel inatoa huduma za Data kwa kutumia mtandao kutoka mkonga wa mawasiliano wa *EASSY* na *EIG*.

Mhe. Spika, Kampuni ya Zantel pia imetanua wigo wake wa kibiashara katika nchi za jirani za Rwanda, Burundi, *DRC* na Zambia. Kwa kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Kampuni ya Zantel itatandaza Mkonga wa Taifa wa Mawasiliano katika Ofisi za Serikali zaidi ya 70 pamoja na Ofisi nyenginezo. Hivi sasa kampuni hiyo inaendelea na utandazaji wa Mkonga huu katika baadhi ya Mikoa ya Tanzania Bara baada ya kuruhusiwa kufanya hivyo. Aidha, Zantel imefanikiwa kuongeza vituo vya *CDMA* kutoka 79 hadi kufikia 116 na ina mpango wa kupeleka mtandao katika majengo ambayo mawimbi (*signal*) hayapenyi.

Mhe. Spika, katika mwaka 2012/2013 kampuni ya Zantel imeendelea kuchangia katika shughuli mbali mbali za kijamii pamoja na kutoa ajira kwa wananchi wa Zanzibar.

(iii) TAASISI ZA MUUNGANO SEKTA YA MAWASILIANO

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2012/2013 Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano imeendelea kuratibu masuala ya mawasiliano kwa kushirikiana na taasisi za Muungano zilizopo Zanzibar ambazo hutoa huduma za mawasiliano kwa njia za simu na posta. Taasisi hizo ni Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (*TCRA*), Shirika la simu Tanzania (*TTCL*) na Shirika la Posta Tanzania (*TPC*).

Mhe. Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuzipongeza taasisi zinazoshirikiana kwa karibu na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano. Nachukua fursa hii kuziomba ziendeleze ushirikiano huo.

IIe) SEKTA YA USAFIRI WA ANGA

Mhe. Spika, Sekta ya Usafiri wa Anga ina majukumu ya kusimamia huduma za Usafiri wa Anga, kuimarisha usalama wa ndege, abiria na mizigo. Majukumu haya yanatekelezwa na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar kwa mashirikiano ya pamoja na taasisi mbali mbali za Serikali ya Jamhuri ya Muungano Tanzania na sekta binafsi.

(i) MAMLAKA YA VIWANJA VYA NDEGE ZANZIBAR

Mhe. Spika, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege inaratibu na kusimamia maendeleo ya usafiri wa Anga Zanzibar pamoja na uendeshaji wa viwanja vya ndege vya Unguja na Pemba.

HATUA ZA UTEKELEZAJI (2012/2013)

Mhe. Spika, katika kipindi cha kilichoanzia Julai hadi Juni 2012/13 Mamlaka ya Viwanja vya Ndege imetekeleza kazi mbali mbali za kawaida za kuhudumia ndege, abiria na mizigo. Viwanja vya Unguja na Pemba vimehudumia jumla ya ndege 55,499 ikilinganishwa na ndege 51,391 zilizohudumiwa katika kipindi kama hicho cha 2011/2012 ikiwa ni ongezeko la asilimia 7.9.

Kati ya ndege hizo, ndege 46,871 zilihudumiwa katika kiwanja cha Kimataifa cha Abeid Amani Karume na ndege 8,628 zilihudumiwa katika kiwanja cha Pemba **(**Kiambatanisho Namba 6)**.**

Mhe. Spika, idadi ya abiria waliohudumiwa katika viwanja vya ndege vya Zanzibar ilikuwa ni 774,669 kuanzia mwezi Julai 2012 hadi Juni 2013 ikilinganishwa na abiria 745,308 waliohudumiwa katika kipindi kilichopita ikiwa ni ongezeko la asilimia 3.9 (Kiambatisho Namba 6). Kati ya abiria hao, abiria 708,683 walihudumiwa katika kiwanja cha Kimataifa cha Abeid Amani Karume na abiria 65,986 walihudumiwa katika kiwanja cha Pemba. Abiria waliopita (*Transit*) wamefikia 94,616.

Mhe. Spika, kwa upande wa mizigo (*freight*) jumla ya tani 1,159 zilihudumiwa katika viwanja vyetu vya Unguja na Pemba ikilinganishwa na tani 900 zilizohudumiwa katika kipindi kilichopita ikiwa ni ongezeko la asilimia 34 kutokana na kuongezeka kwa ndege za mizigo.

Mhe. Spika, katika mwaka 2012/2013 Mamlaka ilipanga kukusanya jumla ya Tsh. 3,060,372,000 na kutumia jumla ya Tsh. 3,060,372,000 kwa kazi za kawaida. Hadi kufikia mwezi wa Juni 2013, Mamlaka imeweza kukusanya mapato halisi ya Tsh 3,543,651,969 kutokana na vianzio vyake vya mapato ya ada ya utuaji wa ndege viwanjani (*landing fees*), kodi ya majengo, faida ya biashara (*concession fees*), huduma za kumbi za watu mashuhuri, ada za kuegesha magari na mapato mengineyo, sawa na asilimia 115.79 ya makadirio (Kiambatanisho Namba 6). Aidha, jumla ya Tsh. 3,319,083,066 zilitumika kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 108 ya makadirio ya kipindi hicho.

MALENGO YA MAMLAKA (2013/2014)

Mhe. Spika, kwa mwaka 2013/14 Mamlaka ya Viwanja vya Ndege itaendelea kuimarisha huduma mbali mbali katika viwanja vya ndege vya Unguja na Pemba ili kukidhi mahitaji ya watumiaji kwa mujibu wa matakwa ya kitaifa na kimataifa ya Usafiri wa Anga kupitia miradi ifuatayo ya Mamlaka:-

Ujenzi wa Ukumbi *(Business Arrivals Lounge*)

Mhe. Spika, Mradi huu una lengo la kuongeza huduma za abiria katika ukumbi wa kuondokea abiria wa daraja la kwanza (*business lounge*) na kuanzisha ukumbi mpya kwa abiria wanaowasili (*business arrival lounge*) ili kujenga mazingira mazuri kwa abiria wanaotumia uwanja wetu.

Ujenzi wa Kituo cha Biashara (*Business Centre*)

Mhe. Spika, Mradi huu unaoendelea una lengo la kukamilisha ujenzi wa kituo cha biashara (*business centre*) ambacho kitaongeza idadi ya ofisi za wadau wa Mamlaka na kutoa fursa zaidi kwa wafanyabiashara kufanya biashara mbali mbali zitakazosaidia kuongeza ajira kwa vijana wetu sambamba na kuongeza mapato ya Mamlaka.

Ununuzi wa Mashine za Ukaguzi (*X-rays Machine*)

Mhe. Spika, ili kuhakikisha hali ya usalama wa abiria na mizigo inaimarika katika viwanja vyetu, Mamlaka ina lengo la kununua mashine za ukaguzi wa mizigo (*x-rays machine*) na kuzifunga katika maeneo husika. Uwekaji wa mashine hizo utaweza kupandisha hadhi ya viwanja vyetu ambavyo vinahudumia abiria wa ndani na wa kimataifa.

Ufungaji wa Mkanda wa Mizigo (*Conveyor Belt*)

Mhe. Spika, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege inakusudia kufunga mkanda wa kusukumia mizigo katika eneo la kuwasili abiria. Mkanda huu utasaidia kurahisisha uchukuaji wa mizigo kwa abiria mara tu baada ya kuwasili na kuondosha msongamano wa abiria wakati wa kusubiri mizigo yao.

Ujenzi wa Kipaa (*Canopy*) eneo la kuwasili abiria

Mhe. Spika, katika kuimarisha huduma za abiria na wadau wengine, Mamlaka inakusudia kujenga kipaa kutoka eneo la kuwasili abiria hadi eneo la maegesho ya magari ili kuwaondoshea usumbufu abiria na wapokeaji wageni wa kupigwa na jua na mvua pamoja na kuwajengea mazingira mazuri wananchi wanaosubiri wageni wao katika eneo la maegesho.

Uwekaji Kipaza Sauti (*Passenger Address Equipment*)

Mhe. Spika, Katika kutekeleza Mradi huu Mamlaka inakusudia kufunga kipaza sauti katika sehemu za kuhudumia abiria ili kurahisisha mawasiliano ndani ya jengo la abiria kwa kutoa matangazo ya safari za ndege na taarifa

nyengine muhimu kwa abiria na kuwaondolea usumbufu abiria wakati wa kusafiri.

Mhe. Spika, kwa mwaka 2013/2014 Mamlaka imekadiria kukusanya jumla ya Tsh 7,735,022,400 na kuzitumia kwa matumizi ya kazi za kawaida.

(ii) MASHIRIKA YA MUUNGANO - SEKTA YA ANGA

Mhe. Spika, katika kipindi cha 2013/2014 Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano iliendelea kutekeleza majukumu yake ya kuratibu shughuli za usafiri na Mawasiliano kwa kushirikiana na mashirika yaliyo chini ya Jamhuri ya Muungano yaliyopo Zanzibar. Miongoni mwa mashirika hayo ni Mamlaka ya Usafiri wa Anga (*TCAA*) na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (*TMA*). Mashirikiano na taasisi hizi yamechangia kwa kiasi kikubwa katika upatikanaji wa huduma na usimamizi wa Sekta ya Usafiri wa Anga hapa Zanzibar.

(iii) SEKTA BINAFSI – USAFIRI WA ANGA

Mhe. Spika, Sekta binafsi imeendelea kutoa mchango mkubwa katika kusaidia juhudi za Serikali za kuendeleza na kuimarisha usafiri wa anga hapa Zanzibar. Mchango huu unaisaidia nchi yetu kwa kuingiza mapato yatokanayo na kodi mbali mbali na kutoa ajira kwa wananchi.

Mhe. Spika**,** kwa mwaka wa fedha 2012/2013 Kampuni mbali mbali za ndege za ndani na nje ya nchi ziliendelea kutoa huduma katika viwanja vyetu vya ndege (Kiambatisho Namba 6).

IIf) SEKTA YA USAFIRI WA BAHARINI

Mhe. Spika, Zanzibar kama nchi ya visiwa inategemea sana Sekta ya usafiri wa baharini kwa usafirishaji wa abiria na bidhaa baina ya visiwa vya Unguja na Pemba, mwambao wa Afrika ya Mashariki na duniani kwa jumla. Kwa kutambua umuhimu wa sekta hii kwa maendeleo ya uchumi na kijamii, Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kupitia Mamlaka husika imeendelea kusimamia maendeleo ya usafiri wa baharini Zanzibar kwa kuimarisha miundombinu ya bandari, kusimamia utoaji wa huduma za usafiri na kulinda usalama wa watu na mali zao pamoja na mazingira ya baharini yasichafuliwe.

Utekelezaji majukumu ya usafiri wa baharini hufanywa moja kwa moja kupitia Mamlaka ya Usafiri Baharini (*ZMA*), Shirika la Bandari Zanzibar (ZPC), Shirika la Meli na Uwakala (*SHIPCO*) pamoja na kampuni za watu binafsi ambazo zimewekeza katika sekta hii.

(i) MAMLAKA YA USAFIRI BAHARINI

Mhe. Spika, Mamlaka ya Usafiri Baharini imeanzishwa chini ya Sheria namba 3 ya mwaka 2009 (*Zanzibar Maritime Authority, Act No. 3 of 2009*). Mamlaka hii ina jukumu la kusimamia usalama na ulinzi wa vyombo vya baharini. Majukumu mengine ya Mamlaka hii ni pamoja na kusimamia shughuli za ukaguzi na usajili wa meli, utoaji wa leseni kwa vyombo vidogo vidogo, udhibiti wa uchafuzi wa mazingira ya baharini, utoaji wa hati na vitambulisho vya mabaharia.

Vile vile, Mamlaka hudhibiti safari za baharini, uchunguzi wa ajali baharini, usimamizi wa maslahi ya mabaharia, pamoja na utoaji wa leseni za manahodha na wahandisi wa vyombo vidogo vidogo.

Aidha, Mamlaka inasimamia utekelezaji wa kanuni ya kimataifa ya ulinzi wa meli na bandari (*ISPS Code*) na uratibu wa shughuli za utafutaji na uokozi kwa maeneo ya Zanzibar.

HATUA ZA UTEKELEZAJI (2012/2013)

Kusimamia Usalama wa Vyombo vya Usafiri Baharini:

Mhe. Spika, katika mwaka 2012/2013 Wizara kupitia Mamlaka ya Usafiri wa Baharini iliendelea kusimamia usalama wa vyombo vya baharini vya abiria na mizigo. Napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru wale wote wenye vyombo vya abiria na mizigo wanaozingatia maelekezo ya serikali kuhusu usalama wa safari za vyombo baharini.

Mhe. Spika, napenda pia kuchukua fursa hii kuwakumbusha wenye vyombo wote kufuata sheria na taratibu zote za usalama wa vyombo vyao. Aidha, ni muhimu kuhakikisha kuwa vyombo hivyo vinakaguliwa katika muda unaotakiwa na wana vifaa vya kutosha vya usalama na kuzingatia umuhimu wa kutoa mafunzo kwa abiria jinsi ya kutumia vifaa hivyo kila wanapochukua abiria katika vyombo vyao. Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano itaendelea kuipa hadhi Mamlaka ya Usafiri Baharini ili iweze kusimamia vyema usalama wa usafiri wa baharini.

Mhe. Spika, katika kipindi cha Julai 2012 hadi Juni 2013 Mamlaka ilisajili meli 18 zenye uzito wa jumla GRT 15,342.10 kwa usajili wa ndani (*Tanzania Zanzibar Registry*) na meli 38 zenye uzito wa jumla GRT 361,440.79 kwa usajili wa nje (*Tanzania Zanzibar International Registry*) (Kiambatanisho Namba 7). Aidha, vyombo vidogo vidogo 81 ambavyo vilisajiliwa pamoja na

kutolewa vitabu vya mabaharia (*Discharge Book*) 660 na vitambulisho vya kimataifa vya mabaharia 21. Mamlaka pia imetowa hati za wahandisi wa Meli (*Boat Master*) 76.

Mhe. Spika, hadi kufikia mwezi Juni 2013 Mamlaka ilikusanya jumla ya Tsh. 1,114,743,825.60 sawa na asilimia 60 ya makadirio na imetumia jumla ya Tsh. 848,245,392 sawa na asilimia 50 ya makadirio iliyopangiwa.

MALENGO YA MAMLAKA (2012/2013)

Mhe. Spika, kwa mwaka 2013/14 Mamlaka itaendelea kujiimarisha katika utendaji wake wa kazi na kukuza vyanzo vyake vya mapato, kuendelea kukamilisha kanuni za Sheria ya Usafiri Baharini na kuongeza matawi mengine ya usajili wa kimataifa.

Aidha, Mamlaka kwa kutumia kanuni za kusimamia makampuni na taasisi zinazotoa huduma katika bandari na meli zilizotayarishwa, itaendelea na hatua za kuwapatia leseni waendeshaji wa huduma hizo na kudhibiti shughuli zao.

Vile vile, ushirikiano mzuri na imara uliopo baina ya Mamlaka na wamiliki wa vyombo vya usafiri baharini pamoja na washirika wengine wa masuala ya usafiri baharini utaendelea kuimarishwa.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Mamlaka imepanga kukusanya jumla ya Tsh. 1,738,088,225 na kutumia Tsh. 1,625,569,760 kwa matumizi ya kazi za kawaida.

(ii) SHIRIKA LA BANDARI

Mhe. Spika, Shirika la Bandari lina jukumu la kutoa huduma za uingizaji na utoaji meli katika bandari za Unguja na Pemba, ufungaji na ufunguaji wa meli kwenye gati, uangalizi wa alama za kuongozea usafiri wa meli (minara na maboya), uteremshaji na upakiaji wa bidhaa kwenye meli pamoja na vyombo vyengine vya usafiri wa baharini na usimamizi wa usalama ndani ya maeneo ya bandari hizo.

Vile vile, shirika linawajibu wa kuhifadhi mizigo na utunzaji wake katika Bandari pamoja na kuvifanyia matengenezo madogo madogo vyombo mbali mbali vya usafiri wa Baharini kwa kutumia Karakana yake kuu ya Malindi.

HATUA ZA UTEKELEZAJI (2012/2013)

Mhe. Spika, Katika kipindi cha Julai, 2012 hadi Juni, 2013 Shirika limehudumia vyombo mbali mbali vya abiria na mizigo katika bandari za Unguja na Pemba. Jumla ya meli za kigeni 174 zimehudumiwa zenye uzito wa GRT 2,596,897 meli za ndani 5,0484 na vyombo vya kienyeji 6,480. Aidha, Shirika limehudumia jumla ya tani 267,442 za mizigo mchanganyiko na makontena 50,271. Kwa upande wa abiria jumla ya abiria 2,146,898 wa ndani na abiria wa nje 2,053 wamehudumiwa (Kiambatisho Namba 8).

Kazi za kiufundi:

Mhe. Spika, katika kipindi hicho Shirika limefanya kazi mbali mbali za kiufundi zikiwemo matengenezo ya vyombo vya baharini vinavyomilikiwa na Shirika lenyewe, pamoja na vyombo vya Kampuni binafsi vilivyohitaji huduma za Chelezo.

Aidha, Karakana Kuu ya Shirika ilifanya kazi za utengezaji wa maboya bubu manne (4) uchongaji wa vipuri kwa ajili ya vitendea kazi vya Bandarini na Baharini pamoja na kuyafanyia matengenezo maboya manane (8) kwa kuyaekea taa mpya za nguvu za jua na kufunga taa mpya za *solar* katika minara mikubwa sita (6) ya Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, katika kipindi cha Julai 2012 hadi Machi 2013, Shirika limetekeleza miradi ifuatayo:-

Ujenzi wa Jengo la Abiria Katika Bandari ya Malindi

Mhe. Spika, lengo la mradi huu ni kujenga jengo la abiria ikiwa ni hatua za uimarishaji wa huduma za Abiria katika Bandari ya Malindi. Mradi huu umetekelezwa kwa kushirikiana na Muekezaji wa ndani kwa kuyafanyia matengenezo makubwa majengo yaliopo katika gati ya abiria. Mradi huu umekamilika na kuzinduliwa rasmi tarehe 8 Julai 2013.

Uimarishaji wa Bandari ya Mkoani

Mhe. Spika, Mradi huu una lengo la kuimarisha Bandari ya Mkoani kwa kurekebisha sehemu ya kiungo cha Gati ya Bandari hiyo iliyoathirika kutokana na mawimbi na kugongwa na vyombo wakati wa kufunga gati. Mradi huu tayari umekamilika.

Ununuzi wa Taa za Solar

Mhe. Spika, Mradi huu una lengo la kununua taa zinazotumia nishati ya nguvu za jua (*solar*) kwa ajili ya minara yote mikubwa ya kuongozea Meli iliopo Unguja na Pemba. Mradi huu umeendelea kutekelezwa ambapo taa zimeshafika na zimeanza kufungwa kwa awamu ya kwanza katika minara 6 mikubwa ya Unguja.

Ununuzi wa vifaa vya kufanyia kazi Bandarini

Mhe. Spika, lengo la mradi huu ni kuimarisha utendaji bandarini kwa kununua zana mpya za kufanyia kazi bandarini kwa awamu. Shirika limefanikiwa kununua "*Reach Stacker*" moja ya tani 45, "*Fork Lift*" moja ya tani 16 na "*Fork Lift Empty Handler*" moja tani 7. Vifaa hivyo tayari vimeshawasili hapa nchini tokea tarehe 27 Februari 2013 na tarehe 27 Mei 2013 na kuanza kutumika.

Uchunguzi wa Kina cha Maji Gati ya Malindi

Mhe. Spika, lengo la mradi huu ni kufanya uchunguzi wa kina cha maji (*Hydrographic Survey*) katika bandari ya Malindi gati ya Magharibi na Kaskazini katika maeneo ambayo yamejifukia. Mradi huu umekamilika ambapo matokeo yanaonesha kupungua kwa kina cha maji kwa wastani wa mita 1.5.

MAPATO NA MATUMIZI YA SHIRIKA

Mhe. Spika, katika kipindi cha 2012/2013 Shirika lilikadiria kukusanya jumla ya Tsh 16.7 bilioni kutokana na mauzo ya huduma zake mbali mbali. Hadi kufikia mwezi Juni, 2013 jumla ya Tsh 15.24 bilioni zilikusanywa ikiwa ni sawa na asilimia 91.1 ya makadirio. Aidha, jumla ya Tsh 11.04 bilioni zilitumika kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 102.03 ya makadirio ya matumizi Tsh bilioni 11.18 kwa kipindi hicho.

MALENGO YA SHIRIKA (2013/2014)

Mhe. Spika, Shirika la Bandari litaendelea kutekeleza majukumu yake kama kawaida. Aidha, katika kipindi hicho Shirika linakadiria kuhudumia jumla ya meli 180 za kigeni zenye uzito (*GRT*) wa tani 2.6 milioni, Meli za ndani zipatazo 3,900 na majahazi 4,100 pamoja na kuhudumia tani 156,500 za mzigo mchanganyiko na makontena 54,146.

Mhe. Spika, kwa upande wa miradi ya maendeleo, katika kipindi cha 2013/2014, Shirika linakusudia kukamilisha miradi iliyoanzishwa mwaka wa fedha unaomalizika niliyokwishakuieleza pamoja na ununuzi wa tagi mpya kubwa na uchimbaji wa mchanga katika Gati ya Malindi sehemu iliyojifukia baada ya kukamilika kazi ya uchunguzi wa kina cha maji.

Mhe. Spika, katika kipindi cha 2013/2014 Shirika limekadiria kukusanya jumla ya Tsh. 17.03 bilioni katika kutekeleza malengo hayo na limepanga kutumia jumla ya Tsh. 14.1 bilioni kwa kazi za kawaida.

(iii) SHIRIKA LA MELI

Mhe. Spika, Shirika la Meli lina jukumu la kuendesha meli zote za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na kutoa huduma za uwakala wa meli za kigeni zinazoingia katika bandari za Zanzibar. Kwa sasa Shirika linaendesha meli mbili za MT Ukombozi na MV Maendeleo na lina matawi mawili katika bandari za Dar es salaam na Pemba.

Mhe. Spika, katika mwezi wa Januari 2013, Baraza lako tukufu lilipitisha Mswada wa Sheria ya uanzishwaji Shirika la Meli na Uwakala Zanzibar kwa madhumuni ya kuimarisha shirika hilo ili liendelee kutoa huduma ya usafiri wa baharini hususan baina ya visiwa vya Unguja na Pemba.

HATUA ZA UTEKELEZAJI (2012/2013)

Mhe. Spika, Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano imeendelea na hatua za kuliimarisha Shirika la Meli ili liweze kuhudumia usafiri wa baharini hususan baina ya visiwa vya Unguja na Pemba na kumudu ushindani wa kibiashara uliopo hivi sasa. Katika hatua hizo, Shirika limeandaa rasimu ya Mpango wa Biashara (*Business Plan*) unaotoa dira, dhamira na mikakati ya kuliendesha Shirika hilo.

Aidha, kwa madhumuni ya kuongeza biashara katika tawi la Dar es Salaam, Shirika limeandaa Mpango wa Biashara ya uwakala wa meli za kigeni utakaowezesha Shirika kufanya shughuli za uwakala katika eneo hilo.

Mhe. Spika, sambamba na jitihada zote hizo, Serikali imeshatoa maamuzi ya kulifanyia mageuzi makubwa ya kimfumo na kiuendeshaji wa Shirika hilo, ili liweze kujiendesha kibiashara na kutoa mchango wake kwa Serikali. Mageuzi hayo yanatarajiwa kufanyika mapema kabla ya kupatikana kwa meli mpya za abiria, mizigo na mafuta.

Mhe. Spika, katika kipindi cha Julai 2012 hadi Juni 2013 Shirika kwa kutumia meli yake ya MV. Maendeleo imeweza kutoa huduma za usafiri wa baharini baina ya visiwa vya Unguja na Pemba. Katika kipindi hiki meli ya MV Maendeleo imefanya safari 137 kwa kusafirisha abiria na mizigo katika visiwa vyetu. Jumla ya abiria 83,764 walisafirishwa kwa kutumia meli hiyo na shehena ya mizigo tani 9,217. Aidha, Shirika limehudumia meli za kigeni zipatazo 103 zilizoingia nchini kwa kutumia bandari zetu.

MAPATO NA MATUMIZI YA SHIRIKA

Mhe. Spika, katika kipindi cha Julai 2012 hadi Juni 2013 Shirika lilikusanya jumla ya Tsh. 4.301 bilioni sawa na asilimia 81 ya makisio ya mwaka 2012/2013 na kufanya matumizi ya jumla ya Tsh. 3.99 bilioni sawa na asilimia 85 ya makisio ya mwaka 2012/2013.

Mhe. Spika, Shirika bado linakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo ushindani wa kibiashara katika sekta ya usafiri baharini, uchakavu wa meli zake, kuongezeka gharama za matengenezo na uagiziaji vipuri pamoja na upandaji wa bei za mafuta. Changamoto nyengine ni uhaba wa wataalamu wa uendeshaji wa meli katika fani ya uhandisi wa meli, wataalamu wenye ujuzi katika fani ya IT na masoko na idadi kubwa ya wafanyakazi wa ofisini wa Shirika.

MALENGO YA SHIRIKA (2013/2014)

Mhe. Spika, kwa mwaka 2013/2014 Shirika litaendelea kutekeleza majukumu yake ya uendeshaji wa meli za Serikali kwa kusafirisha abiria na mizigo kwa kutumia meli ya MV Maendeleo. Shirika litachukua hatua makhsusi ya kupunguza matumizi makubwa yatokanayo na matengenezo ya meli kwa kutumia utaratibu maalum wa "*preventive maintenance*".

Katika utaratibu huu Shirika tayari limeajiri kwa mkataba Wahandisi bingwa wa matengenezo ya meli kutoka Kenya watakaokuwa na uwezo wa kuzikagua mashine za meli zetu kwa lengo la kuzikinga na maharibiko ya mara kwa mara. Pia, Shirika litaendelea na taratibu za kuajiri kwa mkataba wahandisi kwa kazi za melini (*Sign-on/Sign- Off).*

Mhe. Spika, Shirika pia litaendelea kutoa huduma za uwakala wa meli za kigeni zinazoingia nchini kwa kutumia bandari zetu pamoja na kukamilisha taratibu za shughuli za uwakala katika tawi la Dar es salaam. Vile vile, Shirika litaendelea kutoa mchango wa kitaalamu katika zoezi la ujenzi wa meli mpya ya abiria na mizigo ya serikali ambayo inatarajiwa kutoa huduma

za usafiri baina ya visiwa vyetu na sehemu nyengine za mwambao wa Afrika Mashariki.

Mhe. Spika, kwa taarifa yako *sign* imeshatiwa ya kununua meli hii ambayo itajengwa Korea ya Kusini na Kampuni ya *Daewoo International* kwa gharama ya dola za Kimarekani milioni 30.5. Meli hii inatarajiwa kufika Zanzibar katika mwezi wa Juni 2014 na kuanza shughuli zake.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2013/2014 Shirika linategemea kukusanya jumla ya Tsh. 5.4 bilioni kutokana na vianzio vyake vya mapato na kutumia jumla ya 4.8 bilioni.

UJENZI WA MELI MPYA YA ABIRIA NA MIZIGO

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013 Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia bajeti yake yenyewe imefanya maamuzi ya kununua meli kubwa ya abiria na mizigo itakayokua na uwezo wa kutoa huduma nafuu na salama za usafiri katika bandari zetu kubwa za hapa Zanzibar pamoja na bandari nyengine zilizo katika mwambao wa Afrika Mashariki bila ya matatizo.

Mhe. Spika, napenda kuchukua fursa hii kuliarifu Baraza lako tukufu kwamba mchakato wa ujenzi wa meli hiyo sasa umekamilika na Serikali tayari imetia saini mkataba na kufanya malipo ya awali (*down payment*) ya asilimia 35 kwa Kampuni ya *Daewoo International* ya Korea Kusini. Hatua ya utiaji huo wa saini na malipo ya awali umefanywa baada ya Serikali kujiridhisha juu ya uwezo wa *Kampuni* ya *Daewoo* kuifanya kazi hiyo na kukubaliana kwake na masharti ya kiufundi, kisheria na mpango wa malipo ya kazi hiyo.

Mhe. Spika, meli tuliyoamua kuijenga itakuwa na uzito wa *GRT* 5,000 urefu wa mita 90 na upana wa mita 17 na itakua na uwezo wa kuchukua abiria 1,200 katika daraja tatu tofauti kama ifuatavyo:-

- Abiria wa *VIP* 50;
- Abiria wa Daraja la Kwanza 316; na
- Abiria wa Daraja la tatu 834.

Mhe. Spika, wote watakuwa wamekaa kwenye viti na wala hakuna ambaye atakuwa amekaa juu ya nondo. *(Makofi)*

Aidha, meli hiyo itakua na uwezo wa kupakia na mizigo mchanganyiko (ikiwemo magari) tani 200. Kazi hii ya uundaji wa meli inatarajiwa

kuchukua muda wa miezi 23 kuanzia tarehe 10 Julai 2013, siku ambayo utiaji saini wa mkataba huo ulifanyika huko mjini Seoul – Korea ya Kusini.

MCHANGO WA SEKTA BINAFSI KWA USAFIRI WA BAHARINI

Mhe. Spika, Sekta Binafsi imeendelea kuchangia maendeleo ya sekta ya usafiri wa baharini hapa nchini. Hivi sasa kuna zaidi ya makampuni binafsi 24 ambayo yamewekeza katika usafirishaji wa abiria na mizigo kati ya Unguja na Pemba na baina ya bandari za visiwa hivi na bandari nyengine katika mwambao wa Afrika Mashariki (Kiambatanisho Namba 9)

Mhe. Spika, serikali inatambua na kuthamini mchango wa Sekta Binafsi katika kujenga uchumi wa nchi yetu kupiti kutoa huduma mbali mbali inazotoa ambazo hutoa fursa ya kuzijengea uwezo Sekta nyengine kiuchumi na kijamii, kuchangia pato la taifa na kutoa ajira kwa wananchi. Wizara itaendelea kuhamasisha na kuweka mazingira mazuri ya kisera kwa Sekta hiyo ili iendelee kuimarisha huduma hii ya usafiri baharini.

HITIMISHO

Mhe. Spika, kabla sijamaliza hotuba yangu hii, sina budi kutoa shukrani zangu za dhati kwa wale wote walioshirikiana nasi katika kufanikisha malengo tuliyojiwekea ikiwemo Washirika wa Maendeleo mbali mbali waliotusaidia katika kukamilisha programu na mipango ya sekta ya usafiri na mawasiliano katika kipindi kilichopita. Napenda kuchukuwa fursa hii kuzitambua, kuzishukuru na kuzipongeza nchi, jumuiya na taasisi zifuatazo kwa misaada yao muhimu katika kuendeleza sekta mbali mbali za wizara hii.

Mhe. Spika, miongoni mwa nchi ama mashirika yaliyochangia katika maendeleo ya Sekta yetu ni: Jamhuri ya Watu wa China, Norway, Libya, Japan, Saudi Arabia, India, Misri, Marekani, Ujerumani, Oman na UAE. Mashirika ya Kimataifa ni pamoja na Benki ya Dunia (*World Bank*), China *Exim Bank*, Jumuiya ya Nchi za Ulaya (*EU*), Benki ya Maendeleo ya Afrika (*ADB*), Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Afrika (*BADEA*), Mfuko wa Umoja wa Maendeleo ya Kimataifa wa Nchi Zinazosafirisha Mafuta kwa Wingi ulimwenguni (*OPEC Fund*), *SAUDI Fund*, *NORAD*, Mashirika ya Umoja wa Mataifa ya *UNDP*, *IMO* na *ICAO*. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kadhalika, nachukuwa fursa hii kuyashukuru makampuni ya kibiashara ya kitaifa na kimataifa ambayo yamechangia katika Sekta ya usafirishaji wa anga ikiwemo *Precision Air, ZANAIR, Coastal Aviation, Tropical Aviation, Alsalaam Air, Oman Air, Kenya Airways na Ethiopian Airline.* Kwa upande wa usafiri baharini napenda kuyashukuru mashirika ya

Azam Marine, Afican Shipping Cooperation, Maersk, MSC, UAFL, Emirates Shipping na CMA CGM pamoja na Kampuni ya *Danaos* inayotoa ajira ya Ubaharia kwa wananchi wa Zanzibar. *(Makofi)*

Aidha, shukrani za pekee ningependa ziwaendee wamiliki na watendaji wa vyombo vya usafiri baharini, usafiri wa nchi kavu (daladala na magari ya shamba).

Mhe. Spika, kwa niaba ya serikali na kwa kupitia Baraza lako Tukufu naomba kutoa wito kuwaomba wadau tuliowataja hapo juu na wengineo kuendelea kushirikiana na serikali katika kutoa huduma za usafirishaji.

Mhe. Spika, namalizia kwa kuwapongeza na kuwashukuru viongozi wenzangu katika Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano nikianza na Naibu Waziri, Mheshimiwa Issa Haji Ussi Gavu, Mwakilishi wa Jimbo la Chwaka, Katibu Mkuu Dkt. Juma Malik Akil, Naibu Katibu Mkuu Nd. Tahir M. K. Abdullah, Wakuu wa Idara, Mashirika na Mamlaka tunazozisimamia, pamoja na wafanyakazi wote wa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano. *(Makofi)*

Ushirikiano wao mkubwa walionipa umenisaidia sana katika kutekeleza majukumu ya serikali na hasa jukumu la kuendeleza sekta hii. Kwa hivyo, ni wazi kwamba, bila ya mchango wao isingekuwa rahisi kutekeleza majukumu ya wizara kwa mafanikio na ufanisi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, shukrani za pekee zimwendee Mpiga Chapa wa kitabu hiki na wafanyakazi wake wote kwa kufanikisha uchapaji wa hotuba hii. Naomba kuwashukuru wafanyakazi wote wa Taasisi za Serikali na Watu Binafsi pamoja na wananchi kwa jumla kwa kufanikisha kazi za maendeleo ya nchi yetu. Aidha, napenda kuwashukuru wafanyakazi wote wa Baraza la Wawakilishi kwa kufanya kazi kwa uaminifu, nidhamu na moyo wa kuipenda nchi yao. *(Makofi)*

Mhe. Spika, hotuba yangu hii haitokamilika kama sijatoa shukurani zangu za dhati kwa wananchi wa Jimbo langu la Ziwani kwa ushirikiano wao mkubwa wanaonipa na kunivumilia pale ninapokuwa mbali nao kutokana na majukumu mengine ya kitaifa yanayonikabili. Nakiri kwamba imani na heshima yao kwangu ni kubwa na ya kipekee. *(Makofi)*

Mhe. Spika, ni matumaini yangu maelezo niliyatoa yanatosha katika kuliarifu Baraza lako Tukufu pamoja na wananchi kwa jumla kuhusu utekelezaji wa majukumu ya sekta ya usafiri na mawasiliano katika kipindi kilichopita na mpango wa utekelezaji majukumu kwa kipindi kijacho cha 2013/2014. *(Makofi)*

apenda kuchukua fursa hii kueleza kwamba juhudi kubwa zinaendelea kuchukuliwa katika kukabiliana na matatizo mbali mbali yanayoikabili sekta hii. Tutaendelea na jitihada za kuimarisha miundombinu ya usafiri na mawasiliano na huduma zetu zote kama inavyoelekezwa na mwelekeo wa shughuli za sekta. Lengo la serikali ni kuona kwamba sekta hii inaimarika na kuendelea kuchangia maendeleo ya uchumi na ustawi wa jamii wa nchi yetu.

Mhe. Spika, ni matumaini yangu kwamba Waheshimiwa Wawakilishi watachangia hotuba hii kwa kutukosoa pale tulipokosea, kutuweka sawa pale tulipoteleza na bila shaka kuwapongeza wafanyakazi wa sekta hii pale walipofanya vizuri. *(Makofi)*

MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2013/2014

Mhe. Spika, kwa madhumuni ya kuiwezesha Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kutekeleza majukumu yake na malengo yaliyoelezwa katika hotuba hii, naomba kutoa hoja kwamba, Baraza lako Tukufu liidhinishe matumizi ya jumla ya shilingi 20.092/= bilioni kwa mwaka wa fedha 2013/2014. Kati ya fedha hizo, shilingi 5.192/= bilioni zinaombwa kwa ajili ya kazi za kawaida na shilingi 14.90/= billioni zinaombwa kwa ajili ya kazi za maendeleo.

Aidha, naliomba Baraza lako Tukufu kuruhusu Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kukusanya mapato ya jumla ya shilingi 406,200,000/= kutokana na vianzio mbali mbali vilivyomo ndani ya wizara hii.

KIAMBATANISHO NAMBA 1

SEHEMU A: MUHTASARI WA MAKADIRIO YA FEDHA KWA KAZI ZA KAWAIDA, MAENDELEO NA MAPATO KWA KIPINDI CHA JULAI 2012 HADI MACHI 2013 NA MAKISIO YA MWAKA 2013/2014

KASMA	MATUMIZI HALISI 2011/2012	MAKADIRIO 2012/2013	FEDHA HALISI Julai 2012-Juni 201		
			Mishahara/ Maposho	Matumizi Mengineyo	Jum
030 1PEMBA	879,966,277	1,356,800,000	863,966,810	211,312,088	1,075,
0401 MIPANGO	91,000,000	250,000,000	-	108,007,210	108,
0501 MERITIME	104,000,000	-	-	-	
0601 ANGA	1,514,053,329	-	-	-	
0701 UUB	866,095,055	300,000,000	-	177,705,560	177,
0801 LESENI	320,307,550	300,000,000	-	166,017,800	166,
0901 UENDESHAJI	680,606,500	2,653,000,000	2,178,126,012	331,104,090	2,509,
0100MAWASILIANO	67,000,000	175,000,000	-	104,294,460	104,
JUMLA	**4,523,028,711**	**5,111,000,000**	**3,042,092,822**	**1,098,441,208**	**4,140,**

Kiambatanisho 1: Inaendelea…….

SEHEMU B: MAPATO

KASMA	MAPATO HALISI 2011/2012	MAKADIRIO 2012/2013	FEDHA ZILIKUSANYWA JULY-JUNI 2012/2013	ASILIM
0301 PEMBA	87,628,623	42,500,000	47,882,500	
0401 MIPANGO	-	-		
0501 MARITIME	375,813,914	-		
0601 ANGA	1,694,444,561	-		
0701 UUB	3,200,000	6,000,000	6,650,000	
0801 LESENI	224,299,500	346,000,000	339,833,650	
JUMLA	**2,385,386,648**	**394,500,000**	**394,336,150**	

Kiambatisho 1: Inaendelea…….

SEHEMU C: KAZI ZA MAENDELEO

KASMA	MATUMIZI HALISI 2011/2012	MAKADIRIO 2012/2013	FEDHA ZILIZOINGIZWA JULY-JUNI 2012/2013	ASILIM
0301 PEMBA	2,947,116,918	4,950,000,000	2,497,829,904	
0401 MIPANGO	1,785,875,902	1,900,000,000	897,270,096	
0601 ANGA	-	-	-	
0701 UUB	1,602,999,263	3,100,000,000	1,623,644,000	

JUMLA	**6,335,992,083**	**9,950,000,000**	**5,018,644,000**	

KIAMBATANISHO NAMBA 2:

MIRADI YA MAENDELEO ILIYOPANGWA/KUTEKELEZWA 2012/2013

NA.	UJENZI	UREFU (km)	MFADHILI	BA SM
1.	**Ujenzi wa barabara 3 za Pemba** Wete – Gando (13.6) Wete – Konde (15.1) Wete – Chake (24)	52.7	SMZ/BADEA /SAUD FUND	
2	**Ujenzi wa barabara 3 za Pemba** Wete – Chake *(mradi mpya)*	24	SMZ/BADEA /SAUD FUND	
3.	Ujenzi wa barabara ya Mgagadu- Kiwani	7.6	SMZ	
4.	Ujenzi wa barabara ya Mkanyageni - Kangani	6.5	SMZ	
5.	Ujenzi wa barabara ya Ole – Kengeja	3.5	SMZ /OPEC	
6	Upembuzi yakinifu wa barabara za vijijini-Unguja (Matemwe –Muyuni, Kichwele-Pangeni, Njia nne-Umbuji-Uroa, Jozani-Charawe-Ukongoroni-Bwejuu naMkwajuni-Kijini) *(mradi mpya)*	48	AfDB	
7.	Ujenzi wa Barabara ya Amani – Mtoni (Benjamin Mkapa)	4	ROAD FUND	
8	Barabara zinazoingia mjini	83.5		
9	Ujenzi wa barabara 3 Vijijini -Unguja Barabara ya Koani – Jumbi (6.3) Barabara ya Kizimbani – Kiboje (7.2) Barabara ya Jendele – Cheju – Kaebona (11.7)	25.2	SMZ/BADEA	
NA.	**UJENZI**	**UREFU (km)**	**MFADHILI**	
10	Ujenzi wa barabara za vijijini Kaskazini Pemba (Mzambarauni-Pandani –Finya, Bahanasa-Daya-Mtambwe,Chwale-Kojani na Kipangani-Kangagani)	35	SMZ/MCC	
	JUMLA NDOGO			
11	Ujenzi na utanuzi wa maegesho na njia za kupitia ndege.		SMZ/WB	

12	Ujenzi wa jengo jipya la abiria A.AKIA		SMZ /EXIM CHINA	
13	Uimarishaji huduma uwanja wa Pemba		SMZ	
14.	Ujenzi wa bandari mpya Hubport - Maruhubi		SMZ	
	JUMLA NDOGO			
JUMLA KUU				**1**

KIAMBATANISHO NAMBA 3:

WAFANYAKAZI WALIOPATA MAFUNZO KWA KIPINDI CHA MWAKA 2012/2013.

IDARA	SHAHADA YA UZAMILI		STASHAHADA YA UZAMILI		SHAHADA YA KWANZA		STASHAHADA YA JUU	
	MKE	MME	MKE	MME	MKE	MME	MKE	MME
Utumishi na Uendeshaji		1			1		1	
Mipango, Sera na Utafiti	1							
Mawasiliano					1			
Usafiri na Leseni						1		
Ujenzi na Utunzaji Barabara					1	2		
Ofisi Kuu					1	1		1
Jumla	1	1			4	4	1	1

MASOMO YA MUDA MFUPI

IDARA	W/WAKE
Utumishi na Uendeshaji	6
Mipango, Sera na Utafiti	2
Mawasiliano	3
Usafiri na Leseni	2
Ujenzi na Utunzaji Barabara	1
Ofisi Kuu	5
Jumla	19

KIAMBATANISHO NAMBA 4:

BARABARA ZILIZOFANYIWA MATENGENEZO KUPITIA MFUKO WA BARABARA 2012/13

A: UNGUJA: Matengenezo ya kawaida (routine maintenance)

Matengenezo haya yanajumuisha kazi za udhibiti wa majani, usafi wa mitaro, usafi wa culvert na barabara, utunzaji wa alama na michoro, uzibaji wa mashimo kwa barabara za lami na kifusi. Barabara zilizofanyyiwa matengenezo ni:-

KAZI ZA USAFI WA BARABARA ZILIZOFANYWA NA WAKANDARASI/VIKUNDI VYA JAMII

BARABARA ZILIZOFANYIWA MATENGENEZO KUPITIA MFUKO WA BARAB		
S/N	**JINA LA BARABARA**	**LENG**
1	Bububu - Mndo	
2	Kwanyanya-Mkanyageni	
3	Regezamwendo-Mfenesini	
4	Kitundu-Ndagaa	
5	Amani -Dunga	
6	Koani - Machui - Kitumba	
7	Kidimni- Kitope	
8	Pongwe - Matemwe	
9	Kinyasini - Tunguu	
10	Mkwajuni - Nungwi	
11	Upenja - Kiwengwa	
12	Kipilipilini - Pongwe	
13	Mahonda - D/Mkokotoni	
14	Njianne - Bambi	
15	Mfenesini-Bumbwini	
16	Kinazini - Bububu	
17	Bububu - Mahonda	
18	Mahonda-K/Mkokotoni	
19	Mazizini - Fumba	
20	Kitogani - Paje	
21	Paje - Michamvi	
22	Mnazimmoja - U/ndege	

23	Mazizini-Chukwani/U/ndege	
JUMLA		

Kiambatanisho 4: Inaendelea…..
KAZI ZA USAFI WA BARABARA ZILIZOFANYWA NA IDARA 2012/2013

S/No	BARABARA	KAZI ILI
1.	Tunguu – Makunduchi	Matengenezo ya kawaid
2.	Paje – Makunduchi	Matengenezo ya kawaid
3.	Dunga – Chwaka	Matengenezo ya kawaid
4.	Mshelishelini – Pwani - Mchangani	Matengenezo ya kawaid
5	Chukwani – Buyu	Matengenezo ya kawaid
6	Tunguu – Nyambiza	Matengenezo ya kawaid

Kiambatanisho 4: Inaendelea…..
B: PEMBA - ***KAZI ZA USAFI WA BARABARA ZILIZOFANYWA NA WAKANDARASI /VIKUNDI VYA JAMII***

	MATENGENEZO YA KAWAIDA (BARABARA ZA LAMI)	
S/No	**BARABARA**	**LENG**
1	Ole – Konde	
2	Madenjani - M/Takao	
3	Chajaani - Mbuguani(Mkoani)	
4	Mtuhaliwa - Chokocho	
5	Machomane - Vitongoji	
6	Chanjaani - U/Ndege	
7	Chake Chake - Wesha	
8	Mtambile - Kangani	
9	Chanjamjawiri - Tundauwa	
10	Chanjaani - Pujini	

Kiambatanisho 4: Inaendelea…..

	MATENGENEZO YA KAWAIDA (BARABARA ZA LAMI)	

S/No	BARABARA	LE
11	Kenya – Chambani	
12	Mtambile - Mwambe	
13	Mizingani - Wambaa	
14	Chake Chake - Wete	
15	Konde - Kiuyu cha Manda	
16	Chanjaani - M/Manne	
17	Mbuguani - Mkoani Port	
18	Kilindini - Micheweni	
14	Mkoani - Ngo'mbeni school	
15	Mkoani - Makombeni	
16	Bogoa - Michenzani	
17	Mkanyageni - Shidi	
	JUMLA	

Kiambatanisho 4: Inaendelea….. KAZI ZA KAWAIDA ZA USAFI WA BARABARA ZILIZOFANYWA NA WAFANYAKAZI WA IDARA 2012/2013

S/No	LOT NA JINA LA BARABARA	LE M
1.	Chake Chake - Wete	
2.	Konde - Kiuyu cha Manda	
3.	Chanjaani - M/Manne	
4.	Mbuguani - Mkoani Port	
5.	Kilindini - Micheweni	
6.	Mkoani - Ngo'mbeni school	
7.	Mkoani - Makombeni	

8.	Bogoa - Michenzani	
9.	Mkanyageni - Shidi	
Jumla		

Kiambatanisho 4: Inaendelea….. KAZI ZA KAWAIDA ZA KIFUSI ZILIZOFANYWA NA IDARA 2012/2013

S/No.	BARABARA	K
1.	Shidi – Mwambani	Matengenez maintenance
2.	Pweni – Kiuyu	Matengenez maintenance
3.	Mchanga wa kwale - Pembeni	Matengenez maintenance
4.	Wawi – Vikunguni	Matengenez maintenance
5.	Ole – Vitongoji	Matengenez maintenance
6.	Kijangwani - Birikau	Matengenez maintenance

Kiambatanisho 4: Inaendelea….. MATENGENEZO YA MUDA MAALUM (PERIODIC MAINTENANCE) ZILIZOFANYWA NA IDARA/MKANDARASI 2012/2013

S/No	BARABARA	K
1.	Kivunge-Mkokotoni (3.5km)	Imejengwa
2.	Machomanne-Meli Tano (Pemba)(2.7km)	Kiwango ch
3.	Wesha-Mkumbuu (Pemba) (4km)	Imejengwa
4.	Kiuyu kwamanda – Makangale (Pemba)	Imejengwa
5.	Msitu wa Ngezi (Pemba)	Imejengwa
6.	Mtaa wa chakechake (1km)	Imejengwa
7.	Sharifumsa-Mwanyanya-Bububu Skuli (2.6km)	Imejengwa
8.	Kama – KMKM (1.3 km)	Imejengwa
9.	Mkwajuni – Gamba (2 km)	Imejengwa
10.	Hanyengwa – Cheju (5.3 km)	Inaendelea
11.	Kiuyu kwa Manda (2 km)	Imekamilika
12.	Finya – Kicha (3.5 km)	Imekamilika
13.	Mtaa wa Chake (1.5 km)	Imekamilika
14.	Ikulu – Chake (1km)	Matengenez
15.	Amani - Mtoni	Ujenzi

Kiambatanisho 4: Inaendelea….. MATENGENEZO YA SEHEMU KOROFI (SPOT IMPROVEMENTS) YALIYOFANYWA NA WAKANDARASI/IDARA 2012/2013

S/No	BARABARA	K
1.	Bububu-Mahonda (sehemu ya kihinani na Polisi Mfenesini) (Unguja)	Imejengwa
2.	Upenja – Kiwengwa (Unguja)-1.3km	Imejengwa
3.	Chake – Wesha (Pemba)	Imejengwa
4.	Kianga – Ngambwa – Mkoroshoni (Pemba)	
5.	Kwamchina mwanzo	Matengene yanayofany
6.	M/Kwerekwe – Tunguu Mwisho (0.6km)	Imejengwa
7.	Ndagaa – Kitope Sehemu ya Gana (0.5km)	Imejengwa

Kiambatanisho 4: Inaendelea….. MATENGENEZO YA MADARAJA/KALVATI NA MITARO YA MAJI YALIYOJENGWA NA WAKANDARASI 2012/2013

S/No	BARABARA	
1.	Chanjaani – Pujini (Pemba) – ujenzi wa daraja Pujini	I
2.	Finya – Kicha (Pemba) – ujenzi wa daraja Kicha	I
3.	Bububu – Mndo (2 km)	K
4.	Ujenzi wa daraja la Zingwezingwe	U
5.	Ujenzi wa daraja la Shangafu	I
6.	Ujenzi wa daraja la Mkia wa Ng’ombe	U
7.	Ujenzi wa Kalvati ndogo ndogo – Kijitoupele 2No	U
8.	Ujenzi wa Kalvati ndogo ndogo - Amani – Mtoni 2No	U
9.	Ujenzi wa Kalvati ndogo ndogo - Matangini – Kilindi 2No	U
10.	Ujenzi wa Kalvati ndogo ndogo - Finya – Kicha 5No	U
11.	Ujenzi wa Kalvati ndogo ndogo - Weni – Wete mtaa wa Selem 2No	U
12.	Ujenzi wa mitaro Kilimani na Migombani (0.5km)	I
13.	Ufunguzi wa mitaro barabara ya Regezamwendo – Mndo (3km)	U
14.	Ujenzi wa mtaro barabara ya Ole – Konde (0.4km)	U
15.	Ujenzi wa mtaro barabara ya Chake – Mkoani (0.4km)	U
16.	Ujenzi wa mtaro barabara ya Chake – Kibirinzi (0.35km)	U

Kiambatanisho 4: Inaendelea….. MATENGENEZO YA DHARURA (EMERGENCY) ZILIZOFANYWA NA IDARA 2012/2013

S/No	BARABARA	K
1	Ujenzi wa barabara ya Kituo cha umeme Fumba (0.3km)	Uwekaji l
2	Ujenzi wa barabara ya Mazizini - Vitambulisho (0.3km)	Uwekaji l
3.	Ujenzi wa barabara ya Kipitacho – Makombeni (1km)	

Kiambatanisho 4: Inaendelea….. MATENGENEZO YA KAWAIDA BARABARA ZA KIFUSI ZILIZOFANYWA NA IDARA 2012/2013

S/No	BARABARA	K
1	Kangani – Kuukuu (1km)	Imekamil
2	Shindi – Mwambani (1km)	Imekamil
3.	Wawi – Vikunguni M/mboko (2km)	Imekamil
4.	Ole – Vitongoji (1km)	Imekamil
5.	Kijangwani – Birikau (2km)	Imekamil
6.	Penjeni – M/Kiuyu (2.3km)	Imekamil
7.	M/Kwale – Penjeni (2.3km)	Imekamil
8.	Kipitacho – Makombeni (1km)	Imekamil
9.	Barabara ya ndani – Mbweni (0.4km)	Imekamil
10.	Tunguu – Nyamazi – Tunguu (7km)	Imekamil
11.	Chukwani - Buyu (3.5km)	Imekamil
12.	Ndijani skuli – Mkwajungoma (2km)	Imekamil

Kiambatanisho 4: Inaendelea…..KWA KUTUMIA WAKANDARASI/VIKUNDI VYA JAMII

BARABARA ZITAKAZOFANYIWA MATENGENEZO KUPITIA FEDHA ZA MFU 2013/2014		
S/No	**JINA LA BARABARA**	**LENG**
1	Bububu – Mndo	
2	Kwanyanya-Mkanyageni	
3	Regezamwendo-Mfenesini	
4	Kitundu-Ndagaa	
5	Amani –Dunga	
6	Koani – Machui – Kitumba	
7	Kidimni- Kitope	
8	Pongwe – Matemwe	
9	Kinyasini – Tunguu	
10	Mkwajuni – Nungwi	
11	Upenja – Kiwengwa	
12	Kipilipilini – Pongwe	
13	Mahonda – D/Mkokotoni	
14	Njianne – Bambi	
15	Mfenesini-Bumbwini	
16	Kinazini – Bububu	
17	Bububu – Mahonda	
18	Mahonda-K/Mkokotoni	
19	Mazizini – Fumba	
20	Kitogani – Paje	
21	Paje – Michamvi	
22	Mnazimmoja – U/ndege	
23	Mazizini-Chukwani/U/ndege	
JUMLA		
C. MATENGENEZO YA SEHEMU KOROFI (Kwenye makutano ya barabara)		**L**
	MAKUTANO YA BARABARA	
1	Mkunazini	
2	Mchina mwanzo	

3	Malindi	
JUMLA		

Kiambatanisho 4: Inaendelea…..

	MATENGENEZO YA MUDA MAALUM	**LI**
	BARABARA	
1.	Kikwajuni-Kisiwandui school (kwa kiwango cha kifusi)	
2.	Amani-Mtoni (Uwekaji wa kingo za barabara-kerbstones)	
3.	Fuoni-Kibondeni school (Kwa kiwango cha kifusi)	
4.	Njianne - Umbuji	
JUMLA		
F	**UJENZI/UFUKUAJI WA MITARO YA MAJI**	
	JINA LA BARABARA	**LI**
1	Bububu - Mfenesini (Kihinani)- stone pitching	
2	Mfenesini-Kitundu	
JUMLA		
	KAZI ZINAZOHUSIANA NA USALAMA BARABARANI	**LEN**
1	Uwekaji wa CCTV camera na taa za kuongoza magari kwenye makutano ya barabara (Malindi, Mkunazini na Kwamchina mwanzo)	
2	Road Marking in kilometers	
3	Road Sign	
4	Repair and painting of the round about (Amani)	
5	Uwekaji wa nguzo za mpaka wa barabara (Road reserve posts)	

Kiambatanisho 4: Inaendelea…..

	B PEMBA –KAZI ZITAKAZOFANYWA NA WAKANDARASI/VIKUN VYA JAMII
	MATENGENEZO YA KAWAIDA (BARABARA ZA LAMI)
S/No	**BARABARA**
1.	Ole – Konde
2.	Madenjani - M/Takao
3.	Chajaani - Mbuguani(Mkoani)
4.	Mtuhaliwa - Chokocho
5.	Machomane - Vitongoji
6.	Chanjaani - U/Ndege
7.	Chake Chake - Wesha
8.	Mtambile - Kangani
9.	Chanjamjawiri - Tundauwa
10.	Chanjaani - Pujini
11.	Kenya - Chambani
12.	Mtambile - Mwambe
13.	Mizingani - Wambaa
14.	Chake Chake - Wete
15.	Konde - Kiuyu cha Manda
16.	Chanjaani - M/Manne
17.	Mbuguani - Mkoani Port
18.	Kilindini - Micheweni
19.	Mkoani - Ngo'mbeni school

20.	Mkoani - Makombeni
21.	Bogoa - Michenzani
22.	Mkanyageni - Shidi
	JUMLA

Kiambatanisho 4: Inaendelea…..

D	**MATENGENEZO YA MADARAJA NA KALVATI**	
S/No	**JINA LA BARABARA**	
1.	Konde-Kiuyu kwa Manda	
E	**(BOX CULVERTS)**	
SN	JINA LA BARABARA	LENG
1.	Mgagadu – Kiwani	
F	**MITARO YA MAJI**	
S/No	**JINA LA BARABARA**	**LENG**
1.	Ole-Konde	
2.	Chake-Mkoani	
	JUMLA	
G	**ALAMA ZA USALAMA BARABARANI**	
S/No	AINA YA KAZI	LENG
1	Uwekaji wa mistari barabarani (Road Marking)	
	JUMLA	

Kiambatanisho 4: Inaendelea…..KAZI ZA MATENGENEZO YA BARABARA ZITAKAZOFANYWA NA IDARA 2013/2014
UNGUJA: KAZI ZA KAWAIDA 9 (Routine maintenance)

	MATENGENEZO YA KAWAIDA (BARABARA ZA LAMI)	
S/No	**JINA LA BARABARA**	**LEN**
1.	Tunguu-Makunduchi	
2.	Kaebona-Unguja Ukuu	
3.	Mtegani-Mtende	
4.	Kibuteni-Kizimkazi	
5.	M/shelini - P/Mchangani	
6.	M/kwereke - Tunguu	
7.	Kwamchina-Mbuyu mnene/ Nyumbambili	
JUMLA		

Kiambatanisho 4: Inaendelea…..

	UZIBAJI NYUFA BARABARANI-BARABARA ZA LAMI	
S/No	**JINA LA BARABARA**	**LENG**
1.	Fumba-Mazizini	
2.	Mtegani-Mtende	
3.	Kitope-Kidimni	
4.	Regezamwendo-Mndo	
JUMLA		

Kiambatanisho 4: Inaendelea…..

	UZIBAJI MASHIMO BARABARA ZA LAMI	LENG
	AINA YA BARABARA(ROAD CATEGORY)	
1.	Barabara za mjini (Urban roads)	
2.	Barabara za Kuu (Primary roads)	
3.	Barabaraza vijijini (secondary roads)	
4.	Barabara za kawaida (Basic roads)	
JUMLA		

Kiambatanisho 4: Inaendelea…..

PEMBA: KAZI ZITAKAZOFANYWA NA WAFANYAKAZI WA IDARA (Force Account)

A1: KAZI ZA KAWAIDA

S/No	LOT NA JINA LA BARABARA	
1.	Chake Chake - Wete	
2.	Konde - Kiuyu cha Manda	
3.	Chanjaani - M/Manne	
4.	Mbuguani - Mkoani Port	
5.	Kilindini – Micheweni	
6.	Mkoani - Ngo'mbeni school	
7.	Mkoani – Makombeni	
8.	Bogoa – Michenzani	
9.	Mkanyageni – Shidi	
Jumla		

Kiambatanisho 4: Inaendelea…..

A2: Kazi za kuziba mashimo barabarani (Patch works)

S/No	JINA LA BARABARA	
1.	Chake - Chake – Wete	
2.	Kilindini – Micheweni	
3.	Chake - Chake – Mkoani	
4.	Konde - Kiuyu kwa Manda	
5.	Chanjaani - M/Manne	
6.	Chanjaani - U/Ndege	
7.	M/Manne – Vitongoji	
8.	Mtuhaliwa – Chokocho	
9.	Mkoani – Makombeni	
Jumla		

A3: Matengenezo ya muda maalum (periodic maintenance) barabara za kifusi

S/N	JINA LA BARABARA	
1.	Wesha – Mkumbuu	
2.	Msitu wa ngezi	
Jumla		

B Matengenezo ya sehemu korofi (spot improvement) barabara za lami

S/No	JINA LA BARABARA	
1.	Chajaani Mbuguani	

Jumla	

C: Matengenezo ya muda maalum (periodic maintenance) barabara za lami

S/No	JINA LA BARABARA	LEN
1	Kilo road	
2	Selem Street road	
3	Ole - Konde	
Jumla		

KIAMBATANISHO NAMBA 5

UKAGUZI WA VYOMBO VYA MOTO JULAI 2012 HADI JUNI 2013:

AINA YA VYOMBO	IDADI YA VYYOMBO VYA MOTO VILIVYOKAGULIWA				
	UKAGUZI WA KAWAIDA		UKAGUZI WA SHAKA		UKAGUZ AJALI
	UNGUJA	PEMBA	UNGUJA	PEMBA	UNGUJA
GARI	17,862	1364	512	167	676
MOTORCYCLE	12,910	2342	496	13	413
JUMLA	**30,772**	**3706**	**1,008**	**180**	**1,089**

Kiambatanisho 5: inaendelea: RUHUSA ZA NJIA NA USAFIRISHAJI

MAHALI ZILIPOTOEWA	AINA YA HUDUMA ILIOTOLEWA						
	Daladala	Shamba	P/Hire	Taxi	Mizigo	School	Sta
UNGUJA	545	306	544	209	452	23	18
PEMBA	27	223	13	12	93	1	0
JUMLA	**572**	**529**	**557**	**221**	**545**	**24**	**18**

Kiambatanisho 5: Inaendelea: TAKWIMU ZA WAOMBAJI WALIOJARIBIWA KUENDESHA VYOMO VYA MOTO:

AINA YA MADEREVA	WALIOJARIBIWA KUENDESHA			WALIOFAULU KUENDESHA		
	Gari	M/c	**Jumla**	Gari	M/c	**Jumla**
UNGUJA	3,397	1,646	**5,043**	2,527	1,379	**3,906**
PEMBA	1121	1312	**2433**	758	964	**1722**
JUMLA	**4,518**	**2,958**	**7,476**	**3,285**	**2,343**	**5,628**

Kiambatanisho 5: Inaendelea: UTOAJI WA LESENI KWA MADEREVA WANAFUNZI

DARAJA	M	A	B1	B	C1	C	D1	D
UNGUJA	75	3,206	3,037	25	506	208	1,035	
PEMBA	10	394	103	116	11	21	17	
JUMLA	**64**	**2,618**	**2,154**	**93**	**346**	**182**	**811**	

Kiambatanisho 5: Inaendelea: UKUSANYAJI WA MAPATO

S/No	Aina ya mapato	Unguja	Pemba
1	Majaribio ya madereva	63,603,500	11,979,700
2	Ukaguzi wa vyombo	195,377,000	20,993,800
3	Fomu za maombi	31,910,500	8,711,000
4	Kadi za njia	13,330,000	2,750,000
5	Mapato mengineyo	35,612,650	3,438,000
	Jumla	**339,833,650**	**47,882,500**

KIAMBATANISHO NAMBA 6:

IDADI YA NDEGE ZILIZOHUDUMIWA KATIKA KIPINDI CHA JULAI 2012 HADI JUNI 2013

AINA YA NDEGE	IDADI YA NDEDGE 2011/2012		JUMLA	IDADI YA NDEGE 2012/13		JUMLA
	UNGUJA	PEMBA		UNGUJA	PEMBA	
SHEDULE	28,283	7,452	35,735	28,909	8,198	37,107
CHARTER	13,914	377	14,291	16,649	332	16,981
CARGO	2	-	2	12	-	12
PRIVATE	435	-	435	733	-	733
MILITARY	48	-	48	82	-	82
OTHERS	668	100	768	486	98	584
JUMLA	**43,462**	**7,929**	**51,391**	**46,871**	**8,628**	**55,499**

Kiambatanisho 6: Inaendelea: IDADI YA ABIRIA WALIOHUDUMIWA KATIKA KIPINDI CHA JULAI 2012 HADI JUNI 2013

KIWANJA	IDADI YA ABIRIA 2011/2012		JUMLA	IDADI YA ABIRIA 2012/13		JUMLA
	INTER	DOMESTIC		INTER	DOMESTIC	
UNGUJA	307,692	377,396	685,088	295,232	413,451	708,683
PEMBA	32	60,188	60,220	45	65,941	65,986
JUMLA	**307,724**	**437,584**	**745,308**	**295,277**	**479,392**	**774,669**

KIAMBATANISHO NAMBA 7:

ORODHA YA MELI ZILIZOSAJILIWA CHINI YA USAJILI WA NDANI (LOCAL REGISTRY) KIPINDI CHA JULAI 2012 JUNI 2013

NAM	JINA LA MELI	UZITO (GT)
1.	AZAM SEA LINK 1	1,588

2.	BATELEUR (EX PACIFIC MAPLE)	780
3.	MV WETE	199.84
4.	YASSIR	284
5.	COMARCO 232	1424
6.	COMARCO 233	1424
7.	MV. TAWAKAL	170.93
8.	ROYAL EXPRESS 1 (EX. JONEYFUL 5)	409
9.	ROYAL EXPRESS 3 (EX. JONEYFUL I)	475
10.	FALON (EX. PACIFIC DART)	863
11.	COMACO SWFT	391
12.	KILIMANJARO IV	584
13.	MV BARAKAT	399
14.	CISL LEENE (EX EMMA)	3,412
15.	JETMARK	1,219
16.	MV ALLAWI (BUMU)	1,300
17.	SVS BONNY (EX SEIKAI MARU NO.2)	131
18.	FB KHADIJA	288.33
	J U M L A	**15,342.10**

Kiambatanisho 7: Inaendelea: MELI ZILIZOSAJILIWA CHINI KUPITIA "TANZANIA ZANZIBAR INTERNATIONAL REGISTER OF SHIPPING" JULAI 2012 – JUNI 2013

NAM	**JINA LA MELI**	**UZITO (GT)**
1	MT. Grace 1	4147
2	Ali H.R.Z	3016
3	Silva	44322
4	Flora	11833
5	Spartacus	2240
6	Setia 3	254
7	Sea Breeze	5306
8	Cpt. Ahmad II	2827
9	Al Shroog	1827
10	Juliette Pride I	151
11	Juliette Pride II	151
12	Khalil II	780
13	Feiry 1	258
14	RJM	2172.79
15	Atlantis	164796
16	CARAN	13322

17	SEA ROSE	1516
18	CPT. AHMAD II	2827
19	GOZDE	3994
20	GULF LION	1707
21	JASMINE	2478
22	KEF	17066

Kiambatanisho 7: Inaendelea:

NAM	JINA LA MELI	UZITO (GT)
23	LADY MIRA	525
24	LADY SAFIA	1996
25	NAVI MOON	2749
26	ORANUS	5934
27	PHYLLIS	28
28	SADRA	258
29	SPARTACUS	2240
30	AL BARAKA - 8	1378
31	SPIRIDON (EX GOZDE)	3994
32	TOPAZ II	10230
33	ACACIAN	14321
34	CROATIA	2319
35	ITALIA	2265
36	LIMESTONE	21630
37	SPANIA	2265
38	HELVETIA	2318
	JUMLA	**361,440.79**

KIAMBATANISHO NAMBA 8

HUDUMA ZA MELI

S/N	AINA YA MELI	KIPINDI	
		JULAI, 2011 – JUNI, 2012	JULAI 2012 – JUNI, 201
1.	Meli za Nje	152	
2.	Uzito wa Meli	2,005,760	2,59

	(GRT)		
3.	Meli za Ndani	4,664	5,
4.	Majahazi	4,585	6,

HUDUMA ZA MIZIGO

S/N	AINA YA MIZIGO	KIPINDI	
		JULAI, 2011 – JUNI, 2012	JULAI, 2012 – JUNI,201
1.	Mzigo Mchanganyiko	110,586	158,
2.	Makontena	44,643	50,
3.	Mafuta	39,331	33,
4.	Mzigo wa Majahazi	92,856	108,
5.	Abiria wa Ndani	2,074,098	2,146,
6.	Abiria wa Kigeni	824	2,

KIAMBATANISHO NAMBA 9

MAKAMPUNI BINAFSI YA SEKTA YA USAFIRI WA BAHARINI

S/NO	JINA LA KAMPUNI
1	FAST FERRIES
2	AFRICA SHIPPING CORPORATION
3	AZAM MARINE
4	KILIMANJARO FAST FERRIES
5	JAK ENTERPRISES
6	OCEAN SHIPPING
7	SEA STAR SERVICES LTD
8	HAMMY DISTRIBUTORS
9	ZANZIBAR SHIPPING CORPORATION
10	HIDAYA MARINE
11	ONE STOP CENTRE
12	M.S SEPIDEH
13	SEAGULL SEA TRANSPORT

14	SAHARA LINE LTD
15	SEVEN SEAS MARINE SERVICES
16	KAMAL MARINE SERVICES LTD
17	BAOBAO BEACH CO. LTD
18	MARINE TRANSPORT CO. LTD
19	AL-FAT SHIPPING
20	ALBA PETROLEUM
21	KENYA MARINE CONTRACTORS
22	UNITED PETROLEUM
23	COASTAL INTERNATIONAL SHIPPING LINE LTD
24	OCEAN ENTERPRISES CO. LTD

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

TAARIFA

Mhe. Spika: Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano, nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kuwasilisha hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi kwa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano, umetumia karibu muda wa saa 1:35.

Waheshimiwa Wajumbe, baada ya kumshukuru Mhe. Waziri na kabla hatujaendelea nitangulize tena kuwashukuru na nyinyi kwa kutoa mashirikiano makubwa ya kuendesha shughuli zetu. Vile vile nimekumbushwa na Mhe. Ali Mzee Ali kwamba siku kama leo ndio siku ambayo tulipiga kura ili kuleta mfumo wa serikali huu tulionao hivi sasa. Mfumo ambao umetusaidia kuimarisha amani na utulivu katika nchi yetu lakini pia umetusaidia sana kujenga mashirikiano katika chombo chetu hichi cha Baraza la Wawakilishi na utekelezaji wa shughuli ambazo tuna wajibu wa kuzitekeleza kama Wawakilishi wa wananchi. *(Makofi).*

Mategemeo yangu ni kwamba mashirikiano hayo, tukikumbuka siku ya leo ambayo matokeo ya kura yalikuwa ni asilimia 67.4 ndiyo yaliyowezesha kuleta mfumo huu ambao kwa kweli ni mfumo wa aina yake na sisi ni waanzilishi duniani. Kwa hivyo, nichukue nafasi hii kuwapongeza wale

ambao tulikaa pamoja na mpaka tukafikia hapo ndani ya chombo kama hichi. Waheshimiwa Wajumbe, niwapongeze Kamati yangu ile ya Wajumbe sita ambao walifanya kazi hiyo ikiwemo pamoja na kuelimisha wananchi hadi kufikia utaratibu wa kupiga kura siku kama ya leo tarehe 31/07/2010. *(Makofi).*

Waheshimiwa Wajumbe nitoe shukurani nyengine kwamba jana pande zote mbili za *caucus* mulikaa, kwa ajili ya kuzingatia ratiba yetu ilivyo jinsi ilivyokwishatumiwa muda mrefu kidogo. Lakini kwa madhumuni yale yale ya kuleta ufanisi mkubwa katika kupitisha bajeti za wizara mbali mbali. Sasa pamoja na ufanisi huo tumepaswa kuona kwamba shughuli zetu zinamalizika kwa wakati muafaka, nafikiri punde tu tumegaiwa ratiba mpya inayoonesha shughuli zetu zimalizike tarehe 06/08/2013 unaoanzia kesho.

Kutokana na kwa mujibu wa ratiba hiyo karibu kila wizara imeekewa siku lakini tumeona hapo nyuma kina wizara zimechukua zaidi ya siku mbili jambo ambalo limetufikisha hapa tulipo. Kwa maana hiyo, kwa mujibu wa ratiba hii inaonekana shughuli zetu tuzifanye tukiingiza pia siku ya Jumamosi na kama hapana budi pia siku ya Jumapili, ili tuweze kumudu kumaliza shughuli zetu tarehe 06/08/2013 ili hatimaye kwa siku ya pili yake tuweze kuwaruhusu Waheshimiwa Wajumbe kwa maana ya tarehe 07/08/2013 warudi katika maeneo yao, kwa ajili ya kuungana na familia zao katika kusubiri kumaliza mwezi Mtukufu wa Ramadhani na hatimaye kuifaidi Idd-el-Fitri tukiwa pamoja na familia zetu.

Kwa mnasaba huo na kwa maelekezo ambayo nilijaribu kuyatoa kwenu kwa pande zote mbili za *caucus* zetu na kuleta taarifa kwamba tumekubaliana na hayo. Kwa hivyo, sasa kilichobaki ni kuweka utaratibu rasmi ambao kuna baadhi ya maeneo yatakuwa kuna haja ya kutenga Kanuni kando kwa ajili ya kuongeza muda, lakini pia kuweza kuitumia siku ya Jumamosi ambayo kwa kawaida huwa tunapumzika, lakini ikibidi pia na siku ya Jumapili ili tuhakikishe kwamba shughuli zetu tunazimaliza kwa wakati. *(Makofi).*

Waheshimiwa Wajumbe kutokana na hayo nimuombe Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Serikali aweke utaratibu kuwaomba Waheshimiwa Wajumbe, kukubaliana na huu utaratibu ili hatimae uanze mjadala tukiwa tumeshajiwekea utaratibu kama tutakavyokubaliana hapa. Kwa hivyo, nikuombe Mhe. Mwanasheria Mkuu utoe hoja hiyo ya kuweka utaratibu huo.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, nakushukuru pamoja na kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuamsha hai na uzima. Mhe. Spika, nimeona nitoe pendelezo kabla Mhe. Mwanasheria Mkuu hajanyanyuka, kwa sababu akinyanyuka itabidi utuhoji tu kwamba katika utaratibu hatujui ndani yake

kuna nini, isipokuwa tunao muongozo tuliopewa siku zile ambazo tutajadili wizara zilizobakia.

Lakini kumekuwa na utaratibu mara nyingi wa kuongeza muda wakati tunapofanya majumuisho na hasa tunapopitisha vifungu. Kwa hivyo, ninaomba na sijui huo utaratibu unaopendekezwa kama utaruhusu lakini hata muda wa kujadili wajumbe kwa siku zilizobakia na hasa kwa wizara muhimu zilizobakia, basi katika kuongezwa muda wa kuchangia pia uongezwe ili Wajumbe wengi kadri inavyowezekana wapate muda wa kutosha kujadili wizara hizi muhimu kuanzia wizara hii ambayo iko mbele yetu leo Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano, ni wizara nyeti, nzito tena ni muhimu na nadhani kwa makofi haya Waheshimiwa Wajumbe wako tayari kufika hata saa 10:00, lakini kutumikia wananchi wa Zanzibar kuja kupatikana kiwango cha juu kabisa. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nataka kutoa pendekezo hilo kwamba katika huo utaratibu unaopendekezwa baada ya majadiliano ya *caucus* mbili jana, basi zingatio hilo la kuwapatia fursa wajumbe kuna la kuweza kujadili masuala haya mazito katika wizara ambazo zimebakia. Kwa hivyo Mhe. Spika, naomba sana pendekezo lizingatiwe na kwa makofi haya nina hakika wenzangu wamenikubalia. Mhe. Spika, ahsante sana. *(Makofi).*

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Spika, nina heshima ya kuomba kutoa hoja kwamba kwa sababu muda ambao umebaki kwa shughuli zetu za mkutano huu wa bajeti na kwa sababu wizara na hoja ambazo zinahitajika kuwasilishwa bado zimebaki nyingi. Kutokana na hali hiyo, Mhe. Spika naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako hili tukufu likubali kutenga kando Kanuni ya Muda na badala yake tutumie muda kama ifuatavyo.

Kwanza katika siku za kawaida badala ya saa 8:00 Baraza likubali kwamba mikutano yetu iishie saa 9:00. *(Makofi).*

Pili siku ya Jumamosi tarehe 03/08/2013 tuitumie pia kama ni siku ya kazi na ikihitajika tarehe 04/08/2013 kwa muongozo ambao atakuwa anaongoza kiti chetu cha Uspika, basi pia tuitumie kama ni siku ya kazi kwa muda ule ule kuanzia saa 3:00 mpaka saa 9:00, ili tuweze kufanikisha kazi zetu hizi na kumaliza shughuli zetu itakapofika tarehe 06/08/2013.

Mhe. Spika, kwa heshima na naomba kutoa hoja. *(Makofi).*

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, hoja imetolewa niwahoji wale ambao wamekubaliana na hoja wanyanyue mikono, wanaokataa. Waliokubali wameshinda. *(Makofi).*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, nichukue nafasi tena kukushukuruni kukubali hoja hiyo iliyotolewa ambayo itatusaidia kufanya shughuli zetu kwa ufanisi. Kwa hivyo, hoja imeungwa mkono kwa maana hiyo sasa tuanze mjadala na tutangulie kumkaribisha Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi. *(Makofi).*

Mhe. Panya Ali Abdalla (Makamo Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi): Mhe. Spika, awali ya yote napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametuwezesha sisi kukutana hapa katika Baraza lako tukufu tukiwa katika hali ya uzima na afya njema.

Lakini pia ningependa kwa heshima na taadhima, nikushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi ya kusimama mbele ya chombo hiki muhimu cha wananchi ili kuweza kutoa maoni ya kamati juu ya makadirio ya bajeti ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kwa mwaka wa fedha 2013/2014.

Mhe. Spika, nivumilie pia nichukue nafasi hii niwashukuru kwa dhati kabisa Wajumbe wenzangu wa kamati kwa mashirikiano makubwa waliyonipa wakati wa kufanya kazi zetu hizi. Bila ya shaka, bila ya wao leo hii ingekuwa vigumu kusimama hapa na kutoa maoni haya.

Hivyo kwa heshima, naomba niwatambue kwa kuwataja kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa - Mwenyekiti
2. Mhe. Panya Ali Abdallah - Makamo Mwenyekiti
3. Mhe. Ismail Jussa Ladhu - Mjumbe
4. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu - Mjumbe
5. Mhe. Mohammed Haji Khalid - Mjumbe
6. Mhe. Salma Mohammed Ali - Mjumbe
7. Mhe. Marina Joel Thomas - Mjumbe
8. Ndg. Latifa Saleh Suleiman - Katibu
9. Ndg. Himid Haji Choko - Katibu

Mhe. Spika, Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ya Baraza la Wawakilishi ilipata fursa ya kulifikiria kwa kulifanyia uchambuzi wa kina fungu la makadirio ya bajeti ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kama ambavyo imeelezwa katika Kanuni ya 96(1) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi Toleo la 2012 ambayo inaeleza:-

96(1) "Kabla ya Kamati ya Matumizi haijashughulikia fungu lolote la makadirio ya matumizi, fungu hilo kwanza litapelekwa kwenye kamati husika likafikiriwe na halitaletwa kwenye Kamati ya Matumizi ya Baraza Zima mpaka Mwenyekiti amuarifu Spika kwamba Kamati yake imelimaliza kulifikiria fungu hilo".

Mhe Spika, kwa mantiki hiyo nachukua nafasi hii kukutaarifu kuwa kazi hiyo tuliifanya kwa umakini wa hali ya juu na leo hii tupo hapa kuwasilisha taarifa ya kazi tuliyoifanya kama ilivyoelezwa katika Kanuni ya 93 (9) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi Toleo la 2012 kwamba:-

93 (9) "Kabla ya mjadala kuhusu hotuba juu ya Makadirio ya Bajeti kuanza Mwenyekiti wa Kamati ya Wenyeviti wa Kamati atatoa taarifa kuhusu Maoni ya Kamati juu ya makadirio hayo kama atahitaji kufanya hivyo. Pia utaratibu huu utatumiwa na Mwenyekiti wa Kamati wakati wa kujadili Makadirio ya Wizara moja moja."

Mhe. Spika, Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano ni moja ya wizara muhimu katika nchi yetu kutokana na ukweli kwamba inasimamia sekta muhimu kwa maendeleo ya nchi yetu ambazo ni sekta ya usafiri wa baharini, usafiri wa anga, usafiri wa nchi kavu pamoja na mawasiliano.

Mhe. Spika, ni ukweli usiopingika kwamba kioo au uso wa nchi yoyote ni kuwa na miundombinu bora ya usafiri na mawasiliano, ikiwa na maana kuwa na huduma bora za bandari, viwanja vya ndege, miundombinu ya barabara pamoja na upatikanaji wa huduma bora na za uhakika za mawasiliano ya ndani na nje ya nchi. Kwa kulielewa na kulikubali hili, kamati yangu imejitahidi kuhakikisha kwamba tunaipatia Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano maelekezo, ushauri na maagizo ya kutosha ili kuimarisha sekta hizi muhimu.

Mhe. Spika, napenda kuliarifu Baraza lako tukufu kuwa licha ya ugeni na upya wa kamati yako katika wizara hii, lakini imejitahidi katika kuyatafutia ufafanuzi wa maswali mbali mbali ya msingi ambayo kwa namna moja au

nyengine yalikuwa yakihojiwa sana na Wajumbe wako katika Baraza lako tukufu.

Mhe. Spika, kwa kuanzia na ufafanuzi wa tathmini ya jumla iliyofanywa na kamati yangu kwa makadirio ya bajeti ya mapato na matumizi ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kwa mwaka wa fedha 2013/2014, ni kama ifuatavyo:-

HALI YA MAKADIRIO YA MAPATO

Mhe. Spika, makadirio ya mapato yamezidi ambayo ni shilingi 406,200,000/= ukilinganisha na yale ya mwaka wa fedha wa 2012/2013 ambapo yalikuwa ni shilingi 394, 500,000/=, hii ni dalili kwamba Wizara imejipanga kuiongezea zaidi mapato serikali, hatua ambayo kamati yangu inaipongeza.

HALI YA MAKADIRIO YA FEDHA ZA MATUMIZI YA KAWAIDA

Mhe. Spika, wizara pia imeonekana kuongeza makadirio ya matumizi ya kazi za kawaida, ingawa ni kwa asilimia ndogo ambapo kwa mwaka wa fedha 2012/2013 ilikuwa ni shilingi 5,111,000,000/= ambayo ni ndogo ukilinganisha na makadirio ya mwaka wa fedha 2013/2014 ambayo ni shilingi 5,192,000,000/=.

Mhe. Spika ni imani ya kamati kwamba ongezeko hili la fedha za matumizi ya kazi za kawaida limelenga kuleta ufanisi katika kazi.

HALI YA MAKADIRIO YA FEDHA ZA MAENDELEO

Mhe. Spika, katika upande wa makadirio ya fedha za maendeleo, kamati imeguswa na kima kidogo kilichopangwa kwa ajili ya Mradi wa Barabara Tatu (3) za Kaskazini Pemba, fedha hizo ni kidogo na hazitoshelezi kwa kukamilisha mradi huo.

Mhe. Spika, kamati pia imeguswa na kilio cha wizara hii cha kutopatiwa fedha zilizopangwa kwa ajili ya mradi huu kwa robo ya mwisho, fedha ambazo zingesaidia kukwamua mradi huu kwa kiasi kikubwa, hivyo basi kilio hiki tunakifikisha mbele ya Baraza lako tukufu, ili serikali wasikie na kukipatia tahfif inayofaa.

Mhe. Spika, kamati yangu inaiomba serikali kufikiria upya namna ya kuuongezea fedha mradi huu ili uweze kukamilika kwa haraka zaidi.

Mhe. Spika, hiyo ilikua ni tathmini ya jumla ya Makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano.

Sasa kwa heshima kubwa naomba kutoa maoni ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi, kuhusu uchambuzi wa makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2013/2014 kama yalivyotolewa na wajumbe wa kamati hii wakati wa kupitia makadirio hayo.

HALI YA KIUTENDAJI YA WIZARA

Mhe, Spika, kamati yangu katika kazi zake za kamati ilibahatika kuitembelea Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kwa upande wa Pemba na kubaini kwamba, hali ya utekelezaji wa kazi za kila siku umeegemezwa zaidi kwa upande wa Makao Makuu ya Wizara ambayo ipo Unguja. Kwa kweli kiasi kwamba miradi yote hata ile iliyopo Pemba inaratibiwa Makao Makuu Unguja, hali iliyosababisha kamati kukosa majibu ya maswali mengi ambayo ilitarajia kuyapata kuhusu miradi hiyo.

Mhe, Spika, kamati inaishauri wizara kukasimisha baadhi ya kazi zake kwa watendaji wa wizara waliopo Pemba, hasa kwa shughuli ambazo zinafanywa huko, hii italeta urahisi katika utekelezaji wa majukumu na pia itapunguza gharama za kuwatoa watendaji kutoka Unguja kwenda kushughulikia miradi ya Pemba. *(Makofi)*

Mafunzo kwa Watumishi

Mhe. Spika, kamati yangu imefarijika kuona kwamba, kwa mwaka huu wa fedha Wizara imekusudia kusomesha watendaji wake ili kuwaongezea ufanisi katika kazi. Hili linadhihirika katika mafungu yanayohusika na mafunzo kwamba kasma hizo zimeongezeka zaidi ukilinganisha na bajeti ya mwaka 2012/2013.

SEKTA YA USAFIRI WA NCHI KAVU

Miundombinu ya Barabara

Mhe. Spika, Kamati inaanza na pongezi kwa watendaji wa Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara, kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kuhakikisha Miundombinu ya barabara inaimarishwa kwa hali ya juu.

Hata hivyo, Mhe. Spika, Idara hii inashindwa kufanya kazi zake za kukamilisha ujenzi wa barabara mbali mbali kutokana na kuwa kasma ndogo (ukomo wa Bajeti) ya fedha wanazopangiwa na serikali kupitia Wizara ya

Fedha, hali inayopelekea ulipaji wa fidia kwa wananchi kuwa zinasuwa suwa hali hii pia inapelekea hata wakandarasi kushindwa kufanya kazi zao kwa wakati.

Hata hivyo, Mhe Spika, wakati kamati inatembelea miradi ya barabara za Pemba Kaskazini na Kusini, imeweza kujionea kwa macho hali ilivyo katika mradi wa barabara tatu (3) za Kaskazini Pemba (Wete- Gando, Wete- Konde, na Wete- Chake). Mradi mbao umesita kwa muda mrefu sasa na Mkandarasi ameamua kuondoka eneo la mradi kutokana na madai ya fedha anazodai kutokana na kazi aliyokwisha kuifanya. Hapa tunaishauri serikali kufunga mikataba na wakandarasi wenye uwezo wa kumudu kuendesha miradi ili kuepusha usumbufu unaoweza kujitokeza.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014 mradi huu umeombewa shilingi 3,073,356,000 kutoka serikalini ili uendelee ambapo kwa sasa mkandarasi anadai shilling 1.2 bilioni kwa kazi iliyofanyika. Hivyo ni dhahiri fedha zilizotengwa hazitotosha kumalizia mradi huo, pamoja na kulipia madeni ya mkandarasi.

Mhe. Spika, kamati yangu inachukua nafasi hii kuiomba Serikali itafute njia ya kuuongezea fedha mradi huu ili umalizike, kwa sababu mitaro imeanza kubomoka, kifusi kilichoachwa njiani kimeanza kuibiwa na hii yote ni hasara kubwa kwa Serikali.

Vile vile, Kamati inaishauri serikali wakati inapoomba mikopo kwa taasisi za fedha kwa ajili ya kufanyia miradi kama barabara, basi mikopo hiyo ijumuishe pia fedha za fidia kwa watakaoathirika na ujenzi huo, hii itasaidia kupunguza uchereweshaji wa kuanza miradi na kumalizika kwa wakati uliopangwa.

Mhe. Spika, kamati pia ilipata fursa ya kutembelea maeneo mbali mbali yaliyopita miradi ya Barabara kwa upande wa Pemba na kuona nyumba zilizovunjwa kwa kupisha ujenzi wa barabara.

Mhe. Spika, kamati inapenda kuitahadharisha Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano, kuwahamisha wale wote waliolipwa fidia kupisha ujenzi wa barabara ili kuepusha kuja kujenga tena katika maeneo yale yale waliyolipwa fidia.

Mhe. Spika, kamati pia inaiagiza Wizara kulipatia ufumbuzi tatizo la matuta ya Barabarani yanayowekwa na wananchi bila ya ruhusa wala kufuata utaratibu wa kisheria. Hali hii inaleta usumbufu mkubwa kwa watumiaji wa barabara na pia inaweza kusababisha ajali. Hata hivyo, kamati yangu inaamini

kwamba, kuchelewa kwa wizara katika kuweka matuta maeneo ambayo yanahitajika kutokana na kuwa na ajali nyingi, imechangiwa kwa kiasi kikubwa kwa wananchi kujichukulia sheria mikononi mwao. Hivyo basi, tunaishauri wizara ilitafutie ufumbuzi wa haraka tatizo hili la matuta yasiyokuwa na kiwango kwani yanasababisha ajali na uharibifu wa magari na vyombo vyengine vinavyotumia barabara hizo.

Mhe. Spika, kamati pia inaishauri wizara kuhakikisha kwamba wakati wa kuweka alama za Barabarani, viwango vizingatiwe ili alama hizo ziweze kudumu kwa muda mrefu, kwa sababu tunaamini kwamba alama hizo zinasaidia kupunguza ajali za barabarani.

Udhibiti wa Vyombo Vya Moto

Mhe. Spika, kamati inasikitishwa sana na hali halisi ya usafiri wa barabarani ilivyo kwa sasa, ambapo tumekuwa tukishuhudia uvunjaji wa sheria za barabarani hasa kwa madereva wa daladala. Ni kweli kwamba, usimamizi hauangukii moja kwa moja kwa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kutokana na ukweli kwamba hizi ni sheria za jinai ambapo jeshi la polisi linatakiwa kuzisimamia, lakini tunaimani kwamba kwa hiyo sehemu ndogo ambayo wizara hii inahusika basi ingejipanga vyema katika bajeti hii ili kuhakikisha matatizo hayo yanamalizika au kupungua kwa kiasi kikubwa.

Mhe. Spika, ni dhahiri kwamba kuna magari mengi yanayoingizwa Zanzibar na kutoka bila ya kulipa kodi ya usajili. Pia kuna magari mengi yanayotembea bila ya kuwa na namba, ishara ya kwamba hazijasajiliwa. Vile vile kuna mfumko mkubwa wa madereva wengi ambao hawana leseni wala hawajapitia vyuo vinavyotambulika na serikali kujifunza udereva hali inayochangia kuongozeka kwa ajali na uvunjaji wa sheria za Barabarani.

Mhe. Spika, Kamati inaipongeza serikali kwa hatua ya kufanya marekebisho ya Sheria ya Usafiri Barabarani Nam.7 ya mwaka 2003, marekebisho yenye lengo la kuvisajili vyombo vya moto vinavyoingia Zanzibar kabla ya kuanza kutumika. Hatua hii ni ya kupongezwa sana, lakini Kamati inaikumbusha serikali kwamba tatizo letu Zanzibar sio sheria, bali ni usimamizi wa Sheria hizo. Hivyo, tunaamini kila mmoja atatimiza wajibu wake kwa hili.

Mhe. Spika, Idara ya Usafiri na Leseni imeonekana kuweka kiwango kikubwa cha fedha kwa ajili ya huduma za mtandao, Kamati inaimani kwamba kasma hii ya Shilingi 22,400,000 ina lengo la kuleta ufanisi zaidi katika kazi kama ilivyoelezwa kwamba lengo ni kuweka mtandao mkubwa utakaowawezesha kuweka Data system itakayotumika katika maeneo yote yanayohusika na usajili na utoaji wa leseni.

Karakana za serikali

Mhe. Spika, kamati inaipongeza Wizara kwa kuwa na mikakati ya kuziimarisha Karakana zake ziwe katika hali nzuri. Hali hii itaziwezesha Karakana hizo kuweza kutoa huduma kwa vyombo vya serikali. Hata hivyo, Kamati inaitaka Wizara kuharakisha mpango huo ili kuipunguzia serikali mzigo wa kulipia gharama za matengenezo ya vyombo vyake katika karakana za watu binafsi.

SEKTA YA USAFIRI WA BAHARINI

Mhe. Spika, napenda nianze kwa kuishukuru na kuipongeza serikali kwa jitihada zake za kuimarisha usafiri wa baharini kwa kuwa na nia na juhudi za kutafuta usafiri wa uhakika, ili uweze kurahisisha huduma za safari kwa wananchi wa visiwa viwili vya Unguja na Pemba. Mhe. Spika, Kamati yangu inachukua nafasi hii kupongeza sana suala hili.

Vile vile, tumekuwa tukishuhudia jitihada mbali mbali za Wizara kuzifanyia marekebisho sheria zinazohusika na usafiri wa baharini, kama vile Sheria za Bandari, Shirika la Meli na Uwakala, Mamlaka ya Usafiri Baharini n.k, kwa lengo la kuweka mazingira mazuri ya kiusalama yatakayoliepusha taifa hili na majanga makubwa kama yaliyowahi kutokea huko nyuma. Hivyo basi, Kamati inapongeza hatua hiyo.

Shirika la Bandari

Mhe. Spika, kamati imefurahishwa na hatua ya Wizara kutenga shilingi bilioni 1.2 kwa lengo la kufanya utafiti yakinifu juu ya ujenzi wa bandari ya Mpiga Duri, bandari ambayo itaiwezesha Zanzibar kupata maendeleo ya haraka. Hata hivyo, tunaamini kwamba gharama za kazi hiyo ni kubwa na fedha hizo hazitatosheleza, lakini ni vyema tukaanza ili kujua wapi tutafikia. Hivyo basi, kwa niaba ya Kamati naiomba Serikali kuiingizia Wizara fedha hizo kwa wakati ili lengo hilo liweze kufikiwa.

Mhe. Spika, kamati inaiomba serikali kwa kushirikiana na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano, kutafuta utaratibu wa kuifanyia matengenezo ya kudumu gati ya Mkoani Pemba kutokana na ukweli kwamba kwa sasa imeanza kudidimia, hali inayohatarisha maisha ya watu na mali zao. Vile vile, gati hiyo inahitaji kuongezwa urefu kutokana na mahitaji ya sasa ya matumizi ya gati hiyo kuwa ni makubwa ukilinganisha na hapo kabla.

Aidha Mhe. Spika, kamati yangu inatoa pongezi za dhati kabisa kwa Kampuni ya Said Salim Bakharesa kwa kuifanyia matengenezo makubwa Bandari ya

Abiria ya Malindi ambayo imezinduliwa rasmi na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa baraza la Mapinduzi tarehe 8/7/2013.

Mhe. Spika, kwa kweli kazi iliyofanywa katika matengenezo hayo ni kubwa sana, na hivi sasa Bandari yetu inavutia sana hasa katika sehemu ya kukaa abiria pamoja na Ofisi zilizopo katika sehemu hiyo. Tunampongeza sana ndugu yetu Said Bakharesa kwa kazi aliyoifanya na tunatoa wito kwa wafanyabiashara wengine kuiga mfano kama huu wenye lengo la kuileta nchi yetu maendeleo.

Mamlaka ya Usafiri Baharini

Mhe. Spika, Kamati yangu haikufurahishwa na hali ya taasisi hii kwa namna ilivyo kwa sasa, Hata hivyo Kamati inatanabahisha kwamba Zanzibar ni visiwa ambavyo vinahitaji kwa kiasi kikubwa huduma za chombo hiki muhimu.

Mhe. Spika, ni vyema ikaeleweka kwamba juhudi za kuweka usalama wa raia na mali zao wakati wa safari, na kuwahami wakati wa dharura hazitafikiwa iwapo Mamlaka hii haitawezeshwa na kuwa katika hali nzuri. Hii ina maana kwamba, Mamlaka hii ili ifanye kazi zake vizuri, inahitaji vifaa vya kutosha, wataalamu wa mambo ya baharini wakutosha, kama mabaharia wenye elimu ya uokozi, jengo litakalotosheleza mahitaji ya watendaji wake n.k., Kutokana na ukweli kwamba kwa sasa Mamlaka hii ipo jina tu. Kamati inachukua fursa hii kuitaka Wizara kuipa uwezo Mamlaka hii ili ifanye kazi kama ilivyoelezwa katika sheria yake. Si hilo tu, lakini pia kuipa uwezo huko kuambatane na kukamilisha Kanuni za Mamlaka hii ambazo ndizo zitakazoiwezesha kufanya kazi vizuri.

SEKTA YA USAFIRI WA ANGA

Mhe. Spika, Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi inapongeza jitihada zinazooneshwa na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege, pamoja na watendaji wake kwa juhudi kubwa wanazozionesha katika kuhakikisha huduma hizi zinapatikana katika ubora wa hali ya juu, ingawaje wanakabiliana na changamoto kubwa ya kuwa na bajeti ndogo. Hali hii inapelekea kutegemea wafadhili zaidi katika shughuli zao za maendeleo, ambapo kiujumla Mamlaka inahitaji jumla ya shilingi bilioni 7.6 kwa kukamilisha miradi yote, ingawa wao kiwango chao cha makusanyo ni chini ya hapo ambapo ni shilingi bilioni 4.6 tu.

Huduma katika Viwanja vya Ndege

Mhe. Spika, viwanja vya ndege vyote duniani huwa na utamaduni wa kuwa na huduma tofauti zinazotolewa kwa wasafiri, na ndio maana katika maeneo ya viwanja vya ndege, taasisi mbali mbali huwa na ofisi zao ndogo ili kuhakikisha huduma hizo zinapatikana kwa urahisi. Huduma hizo ni kama huduma za afya, huduma za zima moto wakati wa dharura, Uhamiaji, n.k.

Mhe. Spika, kamati ina masikitiko makubwa kulieleza Baraza lako kwamba, kwa upande wa kiwanja cha ndege cha Pemba huduma sio nzuri hata kidogo, ambapo kuna baadhi ya ofisi zimefungwa kabisa. Hivyo basi, Kamati inaitaka Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka husika kulishughulikia tatizo hili mara moja, ili lengo la kuwekwa ofisi hizo liweze kufikiwa.

Mhe. Spika, napenda kuweka msisitizo kwa huduma za zimamoto, wafanyakazi wake hawana nguo maalum zinazoridhisha za kuzimia moto, sehemu wanayolala hairidhishi na wanafanya kazi vituo viwili kwa wakati mmoja, hali ambayo si nzuri kwa uwanja wa ndege ambapo dharura inaweza kutokea wakati wowote. Pia huduma za afya, ambapo kwa sasa hakuna hata panadoli ya kumpatia abiria iwapo atapata maradhi ya ghafla katika kiwanja hicho.

Mradi wa Ujenzi wa Airport Terminal.

Mhe. Spika, kamati ilitaka Maelezo kuhusiana na ujenzi wa jengo jipya la abiria katika uwanja wa ndege wa Abeid Amani Karume Unguja, na majibu ya mwisho ambayo Kamati hii iliyapata kutoka kwa Uongozi wa Wizara kabla ya kuja katika Kikao hiki ni kwamba, Mshauri Mwelekezi alitafutwa na kupatikana kutoka Ufaransa, alifanya kazi na kuwasilisha ripoti yake Wizarani ikiwa na mapendekezo ya hatua za kuchukuliwa pamoja na tathmini ya gharama kwa kila hatua itakayochukuliwa. Hivyo Wizara imepokea ripoti hiyo na inatarajia kuiepeleka Baraza la Mapinduzi kwa ajili ya kufanyiwa maamuzi.

Mhe. Spika, kamati inapenda kutoa taarifa kwako kwamba, maelezo hayo yamepokelewa lakini hayatoshi kuondoa mashaka ya Wajumbe waliyonayo juu ya jengo hilo. Hivyo basi Kamati inaiomba Serikali kuja na maamuzi yatakayopelekea kuchukuliwa kwa hatua muwafaka na za haraka juu ya jengo hilo.

Mradi wa Ujenzi wa Uzio katika Uwanja wa Ndege wa Unguja.

Mhe. Spika, kwa mujibu wa maelezo yaliyotolewa na Wizara kwa kwamba kwa sasa mradi huu umesita, kwa sababu ya kukosekana kwa fedha za kuwalipa fidia wananchi ambao wameathirika na ujenzi wa uzio. Hali hii imepelekea Wizara kushindwa kuendelea na ujenzi kwa sababu haitakuwa sahihi kuwaondosha wananchi katika makaazi yao bila ya kuwalipa.

Mhe. Spika, ni vyema ikaeleweka kwamba, Mkataba wa Mradi huu unatarajiwa kumalizika Mwezi Disemba Mwaka 2013, ambapo kazi hiyo inatakiwa iwe imemalizika lakini ni dhahiri kwamba muda huo utamalizika na kazi haijamalizika. Hivyo basi, Kamati inapenda kuiomba Serikali kuchukua hatua za haraka ili kunusuru Mkandarasi kuja kuondoka na kuiwacha kazi bila ya kumalizika, hali ambayo inaweza kuleta hasara kubwa kwa Serikali.

Mradi wa Uwekaji wa Taa katika Uwanja wa Ndege wa Pemba.

Mhe.Spika, pia Kamati yangu inapenda kutoa maoni yake juu ya Mradi wa Kuweka taa katika Uwanja wa ndege wa Pemba. Itakumbukwa kwamba ahadi hii imekuwepo kwa muda mrefu sasa lakini utekelezaji wake umekuwa mgumu.

Mhe. Spika, inaeleweka vyema kwamba ukosefu wa taa hizo katika Uwanja wa ndege wa Pemba ni hali inayoirejesha nyuma Mamlaka na kuikosesha mapato, hasa ukizingatia kwamba Uwanja umekuwa ukifanya kazi zake kwa nyakati za mchana tu. Kamati inasikitika kwamba katika mwaka wa fedha 2012/2013 mradi huu ulitengewa fedha jumla ya shilingi milioni 400, lakini kutokana na sababu zisizoeleweka Serikali haikutoa fedha hizo na badala yake Wizara iliambiwa kwamba hakutakuwa na fedha za maendeleo kwa robo ya mwisho ambapo fedha hizo zilitarajiwa kupatikana.

Kutokana na hali hiyo Kamati inaishauri Serikali kulipa kipaumbele suala hili kwa kuingiizia Wizara fedha zilizopangwa katika mwaka huu wa fedha kwa ajili ya kazi hiyo ambazo ni shilingi bilioni 1.6, ili kazi hii iweze kukamilika katika Mwaka huu wa fedha.

Mradi wa Ujenzi wa Uzio katika Uwanja wa Ndege wa Pemba

Mhe. Spika, Kamati inaiombwa Wizara kulifikiria kwa umakini suala la kujenga uzio wa uwanja wa ndege wa Pemba ambapo kwa sasa kuna uzio wa magongo ambapo wanyama wanaweza kuuangusha na kuingia uwanjani hali inayoweza kusababisha hatari wakati wa ndege zinapotua au kuruka .

Hata hivyo, Kamati imepata mashaka kutokana na ujenzi wa uzio wa kilomita moja uliojengwa katika uwanja huo, ambao umegharimu shilingi milioni 68, hivyo Kamati inaitaka Wizara kuipatia majibu juu ya kadhia hii.

SEKTA YA MAWASILIANO

Mhe. Spika, Kwa upande wa sekta ya Mawasiliano, kiujumla hali ya sekta hii nchini, inaridhisha ingawa imekuwa ikikumbwa na changamoto za hapa na pale. Hii inadhihirika pale tunapoona kwamba katika harakati za kuimarisha sekta hii kunajitokeza mambo tafauti ambayo yanaweza kuleta athari kwa jamii. Kwa mfano Kamati imelizungumzia kwa upana suala la kuongezeka kwa minara ya mitandao ya simu karibu na maeneo ya makaazi ya watu na hata karibu na viwanja vya ndege, hali ya kuwa inaaminika ya kwamba minara hiyo ina athari kubwa kwa afya za wanaadamu na pia inahatarisha usalama katika vinja nya ndege.

Mhe. Spika, Katika kuhakikisha tatizo hili linapatiwa ufumbuzi, Kamati inaishauri Wizara kuanzisha utaratibu wa kuwa na minara kidogo ambayo itatumiwa na Kampuni tafauti kwa pamoja.

Mhe. Spika, pia kumekuwa na changamoto kubwa ya kukosekana kwa *network (coverage*) katika maeneo tofauti lakini zaidi kwa upande wa maeneo mengi ya kisiwa cha Pemba. Kamati inaiomba Wizara kulitafutia ufumbuzi suala hili kwa haraka zaidi.

Huduma za Posta

Mhe. Spika, huduma za Posta zimeshuka kwa kiwango kikubwa kwa nchi yetu, kwa kuzingatia kwamba kuimarika kwa huduma za usafiri pamoja na huduma za simu kumechangia kwa kiasi kikubwa kupunguza idadi kubwa ya watumiaji wa huduma za posta, hata hivyo, kumekuwa na malalamiko hasa kutoka kwa watendaji wa posta kwamba kuibuka kwa wimbi kubwa la taasisi zisizo rasmi za kusafirishia fedha na vifurushi , kumechangia kwa kiasi kikubwa kwa huduma za posta kukosa wateja, hali ambayo inapelekea Serikali kukosa mapato.

Mhe. Spika, Kamati inashauri Wizara kwa kushirikiana na Serikali kuzitizama kwa umakini taasisi hizi zisizo rasmi na kuhakikisha zinasajiliwa rasmi ili kuongeza Mapato ya Serikali.

Mkonga wa Taifa

Mhe.Spika, kuhusu Mkonga wa Taifa, Kamati ilipata maelezo kutoka Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kwamba, shughuli za kuendesha Mkonga huo kwa sasa zimekabidhiwa rasmi kwa Wizara hiyo, ambazo zitakuwa chini ya Idara ya Mawasilino. Ni imani ya Kamati kwamba kwa bajeti ya mwaka 2013/2014 Wizara imejipanga vyema kwa ajili ya kuitekeleza kazi hiyo ipasavyo, hasa ukizingatia kwamba kazi za Idara zitaongezeka kwa kiasi kikubwa.

Kulithibitisha hili, kasma ya Idara hii katika matumizi ya kazi za kawaida hasa kwa vifaa vya kompyuta imeonekana kuongezeka kutoka shilingi 27,725,000 kwa mwaka wa fedha unaomalizika hadi kufikia shilingi 117,200,000 kwa mwaka ujao wa fedha. Kamati imeridhia kasma hii kwa kuamini kwamba fedha hizi zitatumika vyema kwa huduma za kuimarisha Mkonga wa Taifa.

Mhe. Spika, hata hivyo, Kamati ingependa kueleza masikitiko yake kutokana na kile tulichokiona Pemba wakati wa ziara ya Kamati, kwamba Miundombinu ya Mkonga wa Taifa imepitishwa karibu sana na barabara, hali inayoonyesha kwamba iwapo barabara hizo zitahitajika kuongezwa upana kwa hatua chache tu, Miundombinu hiyo ya Mkonga itaathirika. Kutokana na hali hiyo, Kamati inapenda kuishauri Serikali kufanya mashauriano kabla ya kuanza kutekeleza miradi baina ya taasisi ambazo zinahusika na miradi hiyo kwa sekta tofauti ili kuepusha mradi mmoja kuja kuathiri mradi mwengine hali inayoweza kusababisha hasara kubwa kwa Serikali.

TAASISI ZA MUUNGANO

Mhe. Spika, Kamati inapenda kulitaarifu Baraza lako tukufu kwamba imeshatoa agizo kwa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano, kuipatia Kamati taarifa sahihi, na za kutosheleza kuhusiana na mapato na Tasisi ya Uwakilishi wa Zanzibar katika vyombo vya Muungano ambavyo vinasimamiwa ama vinaratibiwa na Wizara hii kwa upande wa Zanzibar, kama vile Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (*TCRA*), Shirika la Posta Tanzania (*TPC*), Shirika la simu Tanzania (*TCCL*) nk. Hivyo Mhe. Spika, napenda niahidi kwamba hili tutalisimamia ipasavyo.

HITIMISHO

Mhe. Spika, mwisho napenda nichukuwe fursa hii, kuipongeza Wizara , akiwemo Waziri, Naibu Waziri pamoja na Watendaji wake wote wa ngazi za juu, pamoja na wale wa ngazi za chini, kwa mashirikiano yao waliyotupa

katika kipindi kifupi tulichokuwa pamoja. Ni imani yangu kwamba mashirikiano haya yataimarishwa ili kuleta ufanisi na kuweza kufikia lengo la kuleta maendeleo katika jamii na nchi ya Zanzibar kwa ujumla.

Mhe. Spika, Kamati inaunga mkono hoja ya makadirio ya matumizi ya shilingi 20.092 Bilioni ikiwa ni matumizi ya kazi za kawaida, Mishahara na kazi za Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2013/2014. Hivyo basi, nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wachangie na kuyajadili makadirio haya na hatimae kuyapitisha.

Mhe. Spika, kwa niaba ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi na kwa niaba yangu mimi binafsi naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Kabla ya hapo Mheshimiwa baada ya kuwasilisha hotuba hii nilikuwa nina maoni yangu machache, nilikuwa naomba uniruhusu ili niweze kutoa mchango wangu.

Mhe. Spika, mimi ni Mjumbe wa Kamati hii ya Mawasiliano na Ujenzi ambapo naishi katika kijiji cha Mkokotoni. Mara nyingi nimekuwa nikisema kwamba pale tupo katika Bandari ya Mkokotoni. Bandari ile inaonekana kukuwa kwa kasi kubwa kila siku, hili huwa nalieleza. Naiyomba sana serikali iiyone bandari ya Mkokotoni na kuifanyia matengenezo kwa haraka ili serikali iweze kujiongezea mapato.

Mhe. Spika, nasema hilo kutokana na tabu inayopatikana hivi sasa. Bandari ile ukuta ambao umejengwa kwa sasa wote unafunikwa na maji, hali ambayo wafanyakazi wa pale wachukuzi wanapotaka kupakia mizigo inakuwa ni usumbufu mkubwa. Saa nyengine inabidi waende maji ya kifua kwa ajili ya kushusha mizigo. Wanapata athari ya kuumia miguu yao kwa kujichoma na vile vichomi vya mle baharini. Hivyo naiyomba sana wizara ifikirie kujenga ukuta ambao utaweza kuegesha vile vyombo na hatimaye waweze kushusha mizigo hiyo katika hali ya usalama. Lakini pia ukizingatia bandari hiyo itakapokuwa katika hali nzuri serikali itaweza kujipatia mazuri.

Pia nawaomba katika ofisi ya bandari kwa hivi sasa ni chakavu na inaonekana imeanza kubomoko ukizingatia ile ofisi imejengwa kwa mbao. Hivyo naiyomba wizara kuifanyia marekebisho ofisi ile, ukizingatia inashushwa mizigo na kuhifadhiwa pale, kwa usalama wa mizigo hiyo ile ofisi ifanyiwe ukarabati ili mizigo hiyo iweze kudumu na kubaki katika hali ya usalama.

Mwisho Mhe. Spika, naiyomba tena wizara kwa kuzingatia pale inapofanya ujenzi wa hizi barabara kuzingatia sana kuweka *road reserve* kwa sababu barabara tunapotaka kuziongeza kunakuwa hakuna *road reserve* na inakuwa ni usumbufu mkubwa kwa serikali na serikali inatumia gharama kubwa sana

kwa ajili ya kulipa fidia hiyo. Barabara zile ambazo hazijajengwa nitoe ushauri huo ili serikali izingatie kulifanya hilo kwa umakini mkubwa.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo napenda pia nichukue fursa hii kumshukuru sana Waziri wa Miundombinu. Tangu tumeanza bajet sijapata kuona kitabu ambacho kina rangi nyeusi, lakini kwa bajeti hii ya mawasiliano kitabu kimekuja na rangi nyeusi. Mheshimiwa niwaombe wajumbe wenzangu waichangie bajeti hii na kuipitisha na kuikosoa lakini hatimaye waikubali na kuipitisha. Kitabu hicho cheusi ni ishara ya miundombinu ya Mhe. Waziri kwamba barabara zote ambazo anazifanyia matengenezo basi zitakuwa kwa kiwango cha lami. Hiyo inaonyesha ni ishara ya lami.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja. Ahsante (*Makofi*).

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Bi. Panya kwa maoni hayo ya Kamati na ile sehemu ya mchango wako binafsi.

Waheshimiwa Wajumbe niendelee kukuombeni kwamba tushirikiane ili tuweze kumaliza shughuli hii vizuri na kwa ufanisi mkubwa. Nina wachangiaji 31 najua wachangiaji hawa wameitikia wito wa Mhe. Waziri kwamba bajeti hii ichangiwe kwa michango mingi ikosolewe pamoja na kufikia pale ambapo shughuli zimefanyika vizuri. Tukitumia muda wa dakika 20 maana yake tutatumia muda wa saa 10 na dakika 20, maana yake uchangiaji utakwisha kesho saa 8 mchana, halafu yaanze majumuisho na kupitisha vifungu, inaweza ikatupeleka mpaka saa 2 za usiku. (*Makofi*)

Najua makofi hayo yanathibitisha ule ugumu wa shughuli hii. Kwa hivyo nikuombeni tupunguze muda lakini pamoja na kupunguza muda hapana shaka kuna wengine watakosa kuchangia. Mhe. Waziri tayari ameshaanza kupokea michango ya maandishi. Ameniomba tu niseme kwamba wale wanaopeleka kwa maandishi wasisahau kutia majina yao ili ajue na kuja kuwataja vizuri wakati wa majumuisho.

Baada ya hayo basi sasa naomba nimkaribishe Mhe. Mbarouk Wadi Mussa.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Nakushukuru Mhe. Spika, kunipa nafasi ya pili baada ya Mwakilishi wa Mwenyekiti wa Kamati na mimi niweze kutoa mchango wangu kwa wizara hii.

Mhe. Spika, kama ulivyotuelekeza tuende kwa *points* na tujali muda na mimi nataka niende huko huko kwa kuheshimu maamuzi ya kiti

Mhe. Spika, baada ya kukushukuru wewe nimshukuru Mhe. Waziri kwa uwasilishaji wa hotuba yake vile vile niwashukuru watendaji wa Wizara hii kwa kazi kubwa waliyoifanya hadi leo Mhe. Waziri akaweza kuwasilisha hotuba yake.

Mhe. Spika, mimi nitaenda kwenye maeneo matatu manne mpaka matano lakini kidogo kidogo. Nianze kwenye miradi ya ujenzi wa barabara kwenye kitabu cha Mhe. Waziri ukurasa wa 12. Mimi naangalia ule mradi wa barabara tatu Kaskazini Pemba.

Mhe. Spika, nikiangalia kitabu cha Mhe. Waziri hapa kwenye *paragraph 25* anaeleza namna ya hatua za utekelezaji ni kuwa ujenzi wa barabara hizi umefikia hatua mbali mbali za kifusi, hata hivyo utekelezaji wa mradi huu umesita kwa muda kutokana na kuchelewa kumlipa mkandarasi madai yake kwa wakati. Hadi kufikia mwezi wa Juni na hivyo na hivyo, sasa hoja yangu Mhe. Spika, hapa kidogo mimi ndio napata shaka, kama serikali inafanya makubaliano au inafunga mkataba na mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa barabara unaona hapa wanasema ujenzi huu umesita kutokana na kutokulipwa yule mkandarasi, maana yake mkandarasi ameondoka *site* na kama ameondoka kile ambacho amekifanya ameshatoa *certificate*, kwa maana kinachosalia ikiwa ameondoka kwa sababu ya kushindwa serikali kumlipa fedha, maana yake hapa tunaongeza hasara. Mkandarasi yule anapokuwa ameondoka pale huwa analipwa anadai fedha kwa serikali badala ya zile za kawaida ambazo tumetiliana mkataba, anadai na fedha nyengine za ziada kwa kule kukawilishwa kwake.

Lakini suala hili Mhe. Spika, hata ukitizama na huko mwanzo kabla ya kuanza na hizo barabara zenyewe vile vile alikuwa amekaa pasi na kazi na kukaingia hasara ya mamilioni ya shilingi. Mhe. Spika, sisi Wajumbe wako wa kamati ya *PAC* tuliwahi kukagua barabara hizi tulienda pale na tukaona ule ujenzi ulivyokuwa ukiendelea kwa kipindi kile. Lakini tulipata mshtuko baada kuona deni lilivyokuwa kubwa mkandarasi anaidai serikali, tulipouliza deni lile tukaambiwa limesababishwa na serikali kukawia kumpa *site* ya kufanyia kazi. Kuna karibu bilioni moja pale anadai. Sasa leo hapa tunaona tena hapa kwamba serikali kwa kukawia yenyewe kumlipa mkandarasi aliyeondoka kwenye *site*, maana anaendeleza deni. Sasa mimi napata shaka sana Mhe. Spika, yanakuaje mambo haya, maana yake sasa hizi badala ya kujengea barabara nyengine tutakuwa tunaendelea kulipa madeni tu kwa uzembe wetu sisi wenyewe. Maana huu ni uzembe mimi nasema ndio unaosababisha tuendelee na madeni haya.

Lakini Mhe. Spika, ukiangalia kitabu cha Mhe. Waziri cha mwaka jana na kitabu cha mwaka huu, hamna kitu yale ya mwaka jana ndio haya haya, ina

maana hapa kwa mwaka mzima hapakufanyika kazi. Mimi ninajiuliza itakuwaje tutakuwa tunaendelea kuwakamua wananchi wetu wanaolipa kodi tu kwa kazi ambazo hazifanyiki. Mimi hapa nasema tutakuwa tunamnufaisha huyu mkandarasi tu ingawa ni haki yake, maana kama mkataba mliekeana msiponipa pesa zangu mimi kazi simalizi na ni lazima akeshatoa *certificate*, maana yake apewe pesa zake. Sasa kama ana *certificate* ametoa fedha halipwi hapo inakuwaje, sasa nilikuwa nataka Mhe. Waziri atakapokuja hapa anipe maelezo ya kina hasa kwa nini yanatokea haya, sababu za msingi kabisa.

Kwa sababu Mhe. Spika, kwenye haya matumizi ya fedha hizi hapa ndio penye kishindo chote isije kuwa kuna ujanja ya kimikataba unatusababishia sisi kututia hasara na haya tumejaribu kuyazungumza mara nyingi sana kwamba wakati mwengine inawezekana kwa kutokujua au kwa makusudi tu watu wanaamua kufanya vitu vya namna hii. Lakini hasara inapokuja haiendi kwa yule ambaye alisaini tu ule mkataba, hasara hii inakuja kwa taifa kwa sababu wananchi ndio wanaotozwa hizi fedha. Sasa tutakuwa tunaendelea kuwakamua wananchi kuwatoza kodi kwa ajili ya kulipia gharama za ujenzi wa barabara tatu hizi za Pemba ambazo hazikamiliki. Kila kitabu kinachokuja au kila mwaka wa bajeti fedha hizi zinaonekana hazijalipwa na linaongezeka deni. Maana yake ule mkataba wa mwanzo ambao wa ujenzi wa ile barabara upo tayari lakini kila mwaka tunaongezewa fedha za ziada kwa ajili ya kwenda kulipia gharama ambazo tumesababishwa na mkandarasi. Mhe. Spika, mimi nilikuwa ninamuomba sana Mhe. Waziri atakapokuwa hapo aje anisaidie nini tatizo hasa linalosababisha mambo haya.

Mhe. Spika, kwa kujali muda wako ninasogea mbele haraka haraka kwenye ukurasa wa 37 katika Mamlaka ya Viwanja vya Ndege. Mhe. Spika, kwenye kitabu cha Mhe. Waziri hapa alieleza mambo ameyafanya pale katika uwanja wa ndege na anayotarajia. Lakini Mhe. Spika, mimi naona kuna baadhi ya mambo pale mimi siridhiki nayo au kama ndio sera ile imewekwa au vipi juu ya utaratibu mzima unaofanyika pale *airport*.

Nije kwenye suala lile kwanza la maegesho. Mhe. Spika, suala la maegesho mimi kulipia *parking* sio tatizo lakini ninachojiuliza yule ambaye anapeleka abiria ha-*park* anamshusha tu na kuondoka, kwa nini atozwe kodi pale, maana yake wao wanachosema wana-*charge parking* ni kuegesha gari, gari ukaliweka ukasubiri abiria wako lakini mimi nimepeleka abiria ambaye lazima nimpeleke pale hivi mimi natozwa kodi kwa sababu ipi, maana huku kwa wenzetu kote tunakokwenda tunaona *parking* ni kwamba wende uka-*park* lile gari lakini kuegesha pale kushusha abiria na kuondoka unapewa dakika tano viwanja vyote hivi karibu vingi sana unapewa dakika tano ya kumshusha abiria na kuondoka. Ukikawia zaidi ya hapo ndio unatozwa kodi lakini wenzetu hapa naona ukiingia tu unatozwa kodi.

Mimi ninaiona si haki ni lazima tutoe nafasi kwa yule abiria kupelekwa pale *airport* kwa sababu, tayari tumesham-*charge* kuna kitu kinaitwa *airport service charge* analipia abiria. Maana yake ni huduma ambazo atakuwa anapewa pale kwenye kile kiwanja miongoni mwao ni ile gari kwenda kumpelekia pale kushuka na kuondoka, lile gari kama lita-*park* ni sahihi kutozwa kodi lakini kama haliku-*park* pale ni kumshusha na kuondoka mimi ninafikiria sio sahihi.

Lakini Mhe. Spika, vile vile kuna suala zima hili la kulipia *VIP*. Mhe. Spika, mimi naona si sahihi kunambia kwamba *VIP* inalipiwa. Kama unalipia *VIP* maana yake mtu yeyote mwenye pesa yake apite pale lakini *VIP* ni mahala maalum, humu Mhe. Waziri katwambia hapa anataka kuanzisha ujenzi wa ukumbi wa *business arrival lounge* ule wa *first class*, *second class* wale watakuwa wanapitia kule, maana kule watakuwa wanalipia hii, mimi nakubaliana nayo na naunga mkono kabisa lakini hapa mtu ambaye *status* ndio imemfanya apite pale mahala maalum anapita mtu maalum. Sasa unapomlipisha inakuwaje, wakati tayari ameshalipia *airport serives charge* ambayo imejumuishwa kwenye tiketi yake. Kama yule ambaye nimemzungumza ambaye anaenda kuteremshwa na gari yake pale na huyu ni mahala maalum pametengwa kwa watu mashuhuri kupita hapa. Sasa ule umashuhuri wako inabidi uulipie hii kidogo, mimi inanishughulisha. Hebu Mhe. Waziri utakapokuja uje utueleze inakuwaje. Maana yake mimi leo hapa ni Mwakilishi ndio maana nitapita pale *VIP*. Lakini kesho mimi ninaondoka kwenye hili, nitarudi katika eneo la kawaida kule. Sasa leo unapita pale unaambiwa aah! lazima ulipoe elfu ishirini kama hutaki pita kule, kwani huku mimi nilijileta tu, ile *status* ndio iliyonileta huku.

Sasa kama ile *status* ndio iliyonileta na ndio inayonifanya nikapita pale *VIP* si kwamba mimi nakuja pale kwa sababu ya pesa zangu aah! kama kupita kwa kawaida mimi napita siku zote lakini baada ya kupata ule uheshimiwa ndio nimeanza kupita pale. Sasa kama ule uheshimiwa tunaulipia maana yake sasa tunakuwa hatuwatendei haki wale wananchi ambao wametuchagua. Sisi tumechaguliwa Mhe. Spika, na wananchi na tumepewa ile hadhi. Kwa hivyo kama tumepewa hadhi ile sasa lazima tupite pale *VIP* lakini tusilipishwe. Maana yake sasa itakuwa waheshimiwa wote utawakuta wamepanga foleni kule kwa kawaida na pale pamewekwa mahala maalum. Kwa hivyo Mhe. Spika, mimi nilikuwa namuomba sana Mhe. Waziri hili atakapokuja aje atueleze kwa kina, kwa nini anatulipisha pale.

Mhe. Spika, nikiondoka hapo mimi nisogee kwenye ukurasa wa 42 kwenye Mamlaka ya Usafiri Baharini. Mhe. Spika, kwenye Mamlaka ya Usafiri Baharini tulikwenda kufanya ukaguzi pale kwenye Wizara ya Miundombinu, kamati yako ya Baraza ya *PAC* tumefika pale kwenda kufanya ukaguzi katika

wizara ile, miongoni mwa mambo ambayo tulikuwa tunakagua tuliikagua hii Taasisi ya Mamlaka ya Usafiri Baharini. Lakini Mhe. Spika, cha kusikitisha kuna taarifa tulikuwa tunazihitaji pale katika mamlaka husika bahati mbaya sana tukaambiwa taarifa zile kwa siku ile haziwezi kupatikana. Lakini tulikubaliana na watendaji kwamba taarifa zile watuwasilishie ili kuja kuweka taarifa yetu vizuri hapa. Sasa Mhe.Spika, cha kusikisitisha kabisa mpaka leo hii tunapozungumza hapa taarifa zile hazikuwasilishwa kwetu. Tumeziomba tumetaka hazikuletwa. Mimi huwa napenda kusema haya masuala kuna baadhi ya watendaji ninafikiria utusaidie kupitia Ofisi yako hiki kitabu hiki cha kanuni uwapatie.

Sisi tunapokwenda kama kamati, wacha kamati hata nikenda mjumbe tu wa kawaida ninafikiria ni lazima kwa taarifa ninazozihitaji kupatiwa. Kama inaenda kamati inahitaji taarifa *document* wanashindwa kutupa na *documents* zipo kwa sababu huyo mwandikaji wa hizo *documents* alisema hiyo taarifa nimeiandika ipo na nimeiwasilisha kwa uongozi. Sasa uongozi kuiwasilisha kwa kamati imekuwa kikwazo hadi hii leo tumeshindwa kuifanyia kazi ambayo wewe Mhe. Spika, Baraza lako ndio linatutuma kwenda kufanya kazi hizo. Kwa hivyo tunashindwa kufanya kazi zetu kutokana na kutokupata taarifa.

Sasa nilikuwa ninamuomba sana Mhe. Waziri, mimi sitoidhinisha fungu la matumizi la fedha hizi kwa hii Mamlaka ya Usafiri Baharini kwa sababu mpaka anieleze ni kwa nini wameshindwa kutuwasilishia taarifa zile. Taarifa zipo wameshakumbushwa kwa barua na Katibu wa Kamati yetu ninafikiria ni mara mbili lakini basi tu mtu kwa uzembe uzembe hivi tu basi hataki.

Mhe. Spika: Umalize hotuba kwa dakika tano.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Ninakubali Mhe. Spika, dakika tano nitazitumia hizo hizo palipobakia lakini hili naomba nilimalize kwamba nitalizuia hili fungu la ZMA mpaka nipate maelezo ya kina juu ya taarifa ile. Nikishapata basi inawezekana nikaridhia. Maana yake katika kanuni humu waangalie katika kifungu kile haki, fursa na kinga zile za wajumbe, kuna kifungu cha 9 kinaelekeza pale namna ya uwasilishaji wa kutoa *document* wakati wowote zinapohitajiwa.

Mhe. Spika, kwa kujali muda wako na hivyo unavyonihimiza nisogee kwenye ukurasa wa 35 nirudi nyuma kidogo hapo kwenye Kampuni ya Zantel. Mhe. Spika, pamoja na maelezo ambayo ameyatoa Mhe. Waziri hapa mimi nilikuwa naomba atusaidie namna ya ile faida inayopatikana kwenye Zantel sikuona hapa kitu, ametoa maelezo lakini hatukuona mambo ya fedha ambazo zimepatikana, hebu atusaidie SMZ imetwambia ina asilimia 18 tuone kile

ambacho kimepata SMZ kwa kipindi cha miaka miwili mpaka mitatu nyuma hii, faida ambayo inapata kutokana na ubia wake kwenye kampuni hii.

Nikimaliza hapo Mhe. Spika, mimi narejea kwenye hoja yangu ya mwaka jana ya ahadi niliyoahidiwa na Mhe. Waziri ya kwenda kutengenezewa uwanja wangu wa Bajamulenge kule Potoa. Nimeanza mwaka juzi, nikaja na mwaka jana. Mwaka jana Waziri kasema kwa sababu mpya ananiahidi kwamba atahakikisha kwamba uwanja ule unakwenda kushughulikiwa lakini mpaka hii leo haujashughulikiwa. Kwa hivyo nasema tena Mhe. Spika, nitalizuia la barabara kabisa mpaka nipate maelezo ya kina kwa nini uwanja ule mpaka leo haujatengenezwa kama ambavyo serikali iliahidi, imeahidi kwamba imeharibu ule uwanja wa wale watu, ikaomba eneo jengine na ikasema itatengeneza. Nimeshakwenda na watu wao pale si mara moja si mara mbili tunakagua tunarudi, basi tutafanya, tunakagua tunarudi tutafanya lakini mpaka leo hakijafanyika.

Kwa hivyo Mhe. Spika, maeneo mawili haya mimi ninayazuia, mafungu yake mpaka nitakapopata maelezo kamili.

Mhe. Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi . Ahsante sana.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, naomba nichukue nafasi hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uhai uzima na furaha kwa kuweza kuchangia hotuba hii muhimu hotuba ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano. Aidha nikupongeze kwa kunipa nafasi hii pamoja na kwamba Baraza limekwaza na muda lakini bila shaka kwa busara zako utatuongezea kidogo kidogo ili tuweze kutoa mchango mkubwa kwa ajili ya wananchi.

Mhe. Spika, kwanza kabisa nimpongeze Katibu Mkuu wa Wizara hii ni Katibu Mkuu mpya Dr. Juma lakini inaelekea ni msikivu. Juzi tulipokuwa kwenye semina hapa Barazani, wajumbe walichangia Ijumaa, Katibu Mkuu Jumatatu akachukua hatua. Huo ndio uungwana na huo ndio uwajibikaji kwa mambo ya umma. Mwenyezi Mungu amjaalie Katibu Mkuu huyu asimezwe na wale waliozembea akaja akaharibika.

Mhe. Spika, mimi ninakaa maeneo ya waganga wa kienyeji wengi sana kule Pemba. Unapokwenda kwa mganga wa kienyeji Mhe. Spika, ukapigiwa ubao ukaambiwa ubao wako una kiza basi hiyo ni hatari, ama kuna kifo ama kuna nuksi kubwa. Sasa kitabu hiki kina rangi nyeusi kinaashiria kuna hatari kubwa katika Wizara hii, na niwaombe wenzangu Wawakilishi wasijiingize katika hatari kubwa hii ni ishara ya hatari kubwa. Mhe. Spika, huu ni wito wangu wa mwanzo mimi ninakaa maeneo ya Muambe maeneo ambayo yana watibabu

wa kienyeji, hii ndio faslsafa yetu kwamba ukiona pahali pana kiza hapo pahali hapaendeki.

Mhe. Spika, nyuma ya kitabu hiki wametuekea meli na bila shaka ni meli ya Bakharessa lakini wameshindwa kutuwekea meli ya serikali kwa sababu hawana. Wametuekea ndege ya *Ethiopia Air Line* lakini wameshindwa kuweka ndege ya serikali ambayo Rais Aboud Jumbe na Rais Salmin Amour walikuwa nazo lakini wameziangamiza hazipo. Mhe. Spika, mtu hatii mbwembwe kwa nguo ya kuazima, unapotia mbwembwe kwa nguo ya kuazima utaumbuka, unaweza ukavuliwa koti harusini wakati si koti lako. Mhe. Spika, kwa msingi huo sithubutu kuunga mkono hotuba hii asilimia mia kwa mia hata siku moja kwa sababu zifuatazo.

Kwanza nitazuia fungu katika *ZMA*. Mhe. Spika, utakumbuka wewe mwenyewe shahidi mwezi wa nne uliopita serikali ilituletea marekebisho ya sheria mbali mbali ikiwemo sheria ya usafiri wa baharini. Mswada huo upo na naomba ninukuu kifungu 12 marekebisho 17(a). Mhe. Spika, kifungu kinasema kwamba,

> 'Hakuna meli ambayo itazidi umri wa miaka 15 tokea tarehe ya kutumika kwake itaposajiliwa na kupewa leseni kwa ajili ya kuchukua abiria na mizigo hapa Zanzibar'.
>
> Kifungu cha 17(a)2 kinasema,
>
> 'Chombo chochote kinachotua nchi kavu kwa maana ya *land craft* ikiwa asili ya utengenezaji wake ni kwa ajili ya kuchukua abiria hakitosajiliwa au kupewa leseni kwa madhumuni ya kuchukua abiria ndani ya Zanzibar'.

Msingi wa hapa kwamba meli hiyo iwe imetengenezwa asili yake kwa kuchukua abiria na mizigo na ndio maana Mhe. Spika, ukurasa wa 51 wa kitabu hiki cheusi ambacho ni kitabu hatari, Mhe. Waziri anatamwambia kwamba SMZ inaamua kutengeneza meli ya kuchukua abiria 1200 na mizigo kwa maana kwamba asili ya meli hii ya Zanzibar itakayoletwa asili yake ni kuchukua abiria na mizigo, inaenda sambamba na matakwa ya sheria hii.

Mhe. Spika, natoa masikitiko yangu makubwa kwamba *ZMA* imeshindwa kazi na naungana mkono na Mhe. Mbarouk Wadi kwamba hatupasi kuunga mkono fungu la watu walioshindwa kazi. Mhe. Spika, mimi sina maslahi yoyote, nimesema mara nyingi hapa nimekuja peke yangu, nitaondoka peke yangu, sina meli sina jahazi lakini lazima nitetee watu wetu walioamua kuekeza katika sekta ya usafiri.

Mhe. Spika, kuna meli imekuja mpya inaitwa MV Khadija, leo asubuhi mapema nimekwenda kupanda MV Khadija kule Maruhubi. Meli ile tangu ilipotengenezwa serikali kupitia *ZMA* walishirikishwa tangu siku ya mwanzo ninayo taarifa wameenda mara tatu wataalam wa *ZMA* pamoja na Naibu Waziri wa Miundombinu Tanga. Kwa maana kwamba walishirikishwa A to Z. Sasa Mhe. Spika, naomba nisome taratibu ambazo tumegundua, meli ile ya Khadija imeundwa kuchukua abiria 300 wameweka *life jacket 450*, ziada ya 150 kwa mujibu wa taratibu za sheria ya bandari kwa usafiri wa baharini. Lakini ina akiba (*storage*) zenye maji na chakula kwa uwezo wa abiria 350 kwamba meli ikizama, hiyo storage zikipasuka basi ndani yake mna chakula na maji kwa ajili ya abiria ili waweze kuishi mpaka waokolewe. Mhe. Spika, meli ile ina *life boat* moja, ina *engine* 2 kila moja ina 490 horse *power* kwa 280 engine mbili, wanambie Mapinduzi ina ngapi, wanambie Azam ina ngapi, wanambie nyengine zina ngapi.

Mhe. Spika, mwendo wa meli ile kuna kutu kinaitwa *NTS* ni *nautical miles 40* kwa sisi na wataalam wa *engineer*, maana yake unagawa kwa 12 unapata *3.3 hours* kwamba meli ile itatoka Tanga hadi Pemba masaa 3, lakini meli ile Mhe. Spika, ina mashine *system 6* za *fire extinguisher*. Kuna *system* za *Co2* kwa maana ni *oxygen*, mchanga, *pipe* za maji na nyenginezo. Hadi imefika hapa meli hiyo Mhe. Spika, tayari imegharimu zaidi ya bilioni 3 kwa ushauri wa Wizara chini ya *ZMA* imeundwa Tanga na imefika Zanzibar, sasa hivi iko Zanzibar. Kufika hapa wanawambia kwamba hatuwezi kuwasajili kwa nini.

Mhe. Spika, ni dhahiri kwamba kuna watu hawajapata chao, hatuwezi kuwaacha watu waliogharamika chini ya ushauri wa wataalamu hawa baadae ukawaambia hatuwasajili. Mhe. Spika, ni dhahiri kwamba kuna watu hawajapata chao. Naibu Waziri alikwenda Tanga mara tatu, wataalam wa *ZMA* walikwenda Tanga mara tatu, leo wanaambiwa hatuwasajili, mtalipia fidia, ni dhahiri hawajapewa chao na hivi ndio miundombinu Mhe. Spika. Mimi ninamjua Mhe. Rashid mwalimu wangu tuko kwenye *CUF* lakini hapa ni ukweli na anayekataa ukweli Mhe. Spika, ni mpungufu wa akili. Ni dhahiri kwamba *ZMA* wameshindwa kuwasajili kwa sababu hawajapata chao. Kwa hivyo Mhe. Spika, naomba maelezo katika hilo.

Lakini la pili kuna meli ya *MV Buraq III* nimechukua *hansard* mwaka jana Mhe. Waziri amesema wazi kwenye *hansard* yake hii na kuwataka kampuni ya *Buraq III* waende *ZMA*, wamepeleka barua 3 kutaka usajili wakaguliwe wameshindwa kukaguliwa. Masafa gani kutoka *ZMA* mpaka bandarini barua 3 wamepeleka kutaka wakaguliwe wameshindwa kukaguliwa. Leo aje atwambie nipeni pesa tufanye kazi za nini. Mhe. Spika, nitawashangaa sana Wawakilishi wakitoa pesa kwa fungu hili.

Mhe. Spika, kwa Pemba wanaendelea kufa kwa majahazi, ngalawa kutoka Pemba/Tanga lakini Wizara inashindwa kuwahudumia kuwapatia meli ambayo itawasaidia Tanga/Pemba kwa ajili ya ubinafsi tu. Mhe. Spika, mimi kwa nia safi kabisa sitounga mkono fungu hili kwa sababu *ZMA* chini ya Wizara hii wameshindwa kazi na lazima waondoke.

Mhe. Spika, *ZMA* tangu 2009 ipo taarifa hapa ya ukaguzi wa ndani ambayo Mhe. Waziri bila shaka hajaipata, mimi nimeipata kwa hivyo mimi ni mtu wa waganga. Taarifa hii Mhe. Spika, inasema hivi:

> "*ZMA* tangu 2009 wamesajili meli 406 za kigeni, kwa mujibu wa makubaliano ya *IMO* kila meli ina bendera lazima ipeleke mabaharia si chini ya watano. Kwa msingi huo *ZMA* kupitia meli hizi wangesajili mabaharia 2030 wa Zanzibar kwa jimbo moja, maana yake ni abiria 41. Inakisiwa kwamba baharia mmoja katika meli za kigeni ni dola 2500. Kwa msingi huo Zanzibar ingeingiza bilioni nane kwa mwezi mshahara wa baharia".

Watwambie baharia wangapi wamewapata. Zipo taarifa kwamba nafasi hizi wamezipeleka kwengine. Leo mmeshindwa kupeleka mabaharia wetu 2030 leo watu wanakula unga huko halafu utwambie hapa tukupe fedha za nini? Kama unataka sadaka nenda kwa Mhe. Haroun ndiye anayetoa sadaka. Mabaharia hao wangepata Zanzibar hapa maana yake tungeokoa watu wetu wasile unga, leo watu wanakula unga kwa malengo ya watu wachache.

Mhe. Spika, ndio maana *PAC* hawakupewa ripoti ya *ZMA* ina maana *PAC* hawakupewa ripoti ya *ZMA*, mimi barua ya *PAC* ninayo, *PAC* wamenipa barua tangu tarehe 11/6/2013 ya kukumbusha mara ya pili jamaa anakataa tu hataki, wanaita shamba la bibi lile kila mtu aamue tu, kuna uovu Mhe. Spika, *PAC* wajue kwamba kuna uovu wa upotevu wa fedha nyingi za Serikali, ndio maana hamukutoa ripoti sio kwa bahati mbaya. Kwa hivyo napendekeza Mhe. Spika, kwa msingi huo Baraza likatae bajeti hii kwa njia mbili kubwa za msingi.

Kwanza tuunde Kamati ya Wawakilishi na wataalamu iende ikachunguze Wizara nzima. Hili si dhambi Mhe. Spika, Wizara hii ikaaihirishwa mpaka baada ya siku kuu ikaja tena, hayo yalifanyika Tanzania Bara yanafanyika Tanzania nzima kwamba Wizara hii ina uovu na ndio maana Waziri akaandika hivi, bila ya kusahau ni Alhajj mkubwa Mufti anajua kwamba weupe kuna shari tupu. Kwa hivyo tuahirishe bajeti hii mpaka siku kuu tuunde Kamati ya Baraza na wataalamu tuchunguze wizara nzima, pengine hapa watu safi pengine ni watu watano tu Waziri, Katibu Mkuu na Naibu Waziri lakini mimi napendekeza tuchunguze wizara nzima.

Mhe. Spika, mimi nataka nipate maelezo ya meli yetu ya Khadija na meli ya Buraq III, kwa nini hazikusalijiwa wakati zina sifa zote zimekamilisha au kwa kuwa hamjapewa fedha kwa ajili ya futari.

Mhe. Spika, Mamlaka ya Uwanja wa Ndege, hili ndilo la kusema hasa kwamba Mamlama ya Uwanja wa Ndege ni mali ya mtu mmoja na mimi nataka uangalie *scheme of service* ya Uwanja wa Ndege. Kuna makarani wawili, mmoja anapewa laki tatu na mmoja laki tano, ni *level* moja ya elimu na *level* moja ya kazi. Mmoja laki tatu na mwengine laki tano, pengine huyu wa laki tano yuko vyengine lakini huo ndio ukweli. Mfanyakazi wa *VIP* anapewa laki saba bosi wake laki sita. Bosi wa ile *VIP* yote ile laki sita, mfanyakazi laki saba, ukiangalia utaona kama tofauti ipo.

Mhe. Spika, zipo taarifa hadi hii leo *Hangar* iko mikononi mwa Mkurugenzi. Mhe. Hamza barua anayo ataonesha, hata nidhamu ya Baraza hapana tumesema mara kadhaa hili jambo lirejeshwe serikalini watu wamekataa. Mhe. Spika, Baraza hili *ZRB* kupitia Waziri wa Fedha wameagiza kwamba ndege ya *Precision Air* izuiliwe baada ya kuwa na deni la bilioni tatu za Wazanzibari, hii imeandikwa *official* na *ZRB*, barua tena imeandikwa kwa mkono mimi sikubaliani na hayo endeleeni. Hii hapa si kaiandika Muwambe, *ZRB* anaandika kwa ushahidi zuieni fedha za *Precision Air* mpaka alipe bilioni tatu, Mkurugenzi anasema aah! hili jambo liacheni kwanza endeleeni, *ZRB* ndio aliyepewa mamlaka ya kukusanya kodi Zanzibar. *Airport* ni Mamlaka ya mtu. Nashauri mimi kwamba aandikiwe hati iwe mali yake ili tuweze kumsamehe.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo ninaomba niseme ni suala suala zima la ujenzi barabara na fidia. Mimi nimebahatika sana kufungua barabara ya Kiwani lakini naomba Wawakilishi wenzangu watahadhari sana, barabara hii tangu uhai wa Rais Jumbe tunatenga fedha tu lakini hakuna maendeleo ya kiasi hicho, mara hii alhamdullillahi imetiwa fusi mpaka Kiwani sokoni. Mhe. Waziri naomba nipate mchanganuo wa gharama za barabara ile ulivyotumia ili wenzangu wanikubalie kuomba fedha ambazo zimeombwa. Jengine ninaomba nipate maelezo kwa hii barabara inayojengwa Mtambwe, zipo taarifa kwamba mkandarasi amelipwa kwa *square metre*, Wizara imekataa inalipa kwa meter.

Mhe. Spika, jengine ni bandarini, ninayo orodha ya makontena hapa ambayo hayakulipiwa mapato ya serikali na vile vile nina risiti feki, nina orodha ya makontena na nina risiti feki ambazo zimetumika kwa ajili ya kuwanufaisha, kwa nini Wawakilishi bajeti hii waipitishe. Sasa haya ikiwa ni kwa mwezi jee, kwa mwaka ni pesa ngapi, halafu mtuambie kwamba nchi hii haina pesa.

Nitawashangaa sana Wawakilishi wenzangu wakimpa fedha huyu Waziri, watakuwa na wao ni sehemu ya tatizo.

Mhe. Spika, kwa sababu ya muda wako ninaomba nimalizie kwa kusema kwamba Idara ya Utumishi na Uendeshaji ni Idara moja mbaya sana. Kuna mfanyakazi alishutumiwa tu kwa kuchelewa kazini kafukuzwa kazi. Wizara imemkubalia mpaka Katibu Mkuu Kiongozi kwamba arejee kazini, mwisho Mahakama imesema arejee kazini, Waziri amekataa na watu wake, kwa nini apewe pesa huyu, Mahakama Kuu inaamua mara mbili kwamba huyu mtu hana hatia apewe haki yake, Waziri anasema ana watu wake wenziwe, lakini kuna watu ambao tumewashutumu humu kwa ushahidi kwa ajili ya fedha za umma, Kamati ikaundwa tukachunguza na tukathibitisha wakasimamishwa kazi leo wamerejeshwa kazini siri, wana maana gani kupewa pesa hawa Mhe. Spika, huyu ambaye kashutumiwa wamembania, Kamati ya Baraza mimi na Hamza tumechunguza tukamgundua Mkurugenzi wa Utumishi kaiba fedha akasimamishwa leo karejeshwa kazini kisirisiri. Sasa maana yake nini Waziri ni alhaji Mkubwa Mufti na huyu ambaye aliyegundua kwamba kuna makontena hayakulipwa fedha yeye kafukuzwa kazi lakini aliyefanya uhalifu amelindwa, maana yake nini.

Mhe. Spika, nimalizie kwa kusema kwamba Nabii Nuhu baada ya kaumu yake ya kufanya maasi makubwa ya shirki kwa Mwenyezi Mungu alimwambia unda jahazi, akamwambia unda jahazi utangaze kwamba wale wote wanaokuamini uwaambie nataka kuunganisha hii ardhi, jahazi ikaundwa Nabii Nuhu akabaki na jeuri hatimaye harka ilipokuja ya Mwenyezi Mungu, mtoto wa Nuhu na familia nyengine zile za makafiri wakazama. Mhe. Waziri hii ni harka na lazima tukuzamishe wewe kwanza ili iwe funzo.

Mhe. Spika, dakika mbili niseme kwamba ninaomba nimnukuu muimbaji Mwanaacha Hassan. Mhe. Spika, lazima tunukuu wasanii kwa sababu tuone. Mhe. Spika, Mwanaacha Hassan anasema kwamba, "Ukweli hauchakai na wala hauzeeki, kwenye kiza haukai, ukweli haufichiki, ukweli hauelei wala hautetereki. Mhe. Spika, msanii akaendelea kusema kwamba ukweli huwa mchungu na wala haumezeki, lakini huwa sukari kwa wale wapenda haki kama Hija, ukweli huwa mchungu na wala haumezeki lakini huwa sukari kwa wale wapenda haki". Mhe. Spika, naomba wenzangu waungwana wa Kizanzibari CCM na CUF, bajeti hii irudi wakakae tena wajipange waje tena na ndio maana tukamwambia Rais kwamba tupe sisi, si kwa njaa kwa sababu tuko makini. Mhe. Salmin Awadh yuko tayari pale, Mshimba yuko tayari na mimi leo ninaomba nipeni mimi niwasaidie hawa watu (*Makofi*).

Mhe. Spika, baada ya maelezo yangu hayo kwa nia safi kabisa nisije nikaambiwa sina shukurani, nimejengewa barabara ya Kiwani si kwa pesa ya

Waziri, si pesa ya Katibu Mkuu ni pesa ya walipa kodi Wazanzibari, siungi mkono hotuba hii na nawaomba sana Waheshimiwa Wawakilishi wenzangu Mhe. Spika, tuachie tuletee watu hawa wenye fedha warudi wajipange. Ahsante sana.

Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali:Mhe. Spika, kwanza nachukua nafasi hii kukushukuru kwa dhati pamoja na Baraza lako kwa kuweza kutuongoza katika njia ya hekma na busara na kuwashukuru Wawakilishi wenzangu wote kwa kutoa mashirikiano mazuri.

Mhe. Spika, humu ndani katika Baraza letu la Wawakilishi zima tuna Serikali ya Umoja wa Kitaifa na huku sote tumekuja kwa maslahi ya nchi na kuwatumikia wananchi katika visiwa vyetu vya Unguja na Pemba. Kwa hivyo nataka kusema tu kwamba hii *back bencher* iliyokuwepo huku hakuna wapinzani, tumekuja hapa kwa moja tu kuitetea nchi yetu na kufanya maslahi ya nchi hii.

Mhe. Spika, nilikuwa nasema siku zote hapa tulipofika hatukuwa wakweli, kuanzia viongozi na watendaji ndio tumefika nchi hii tulipofika hapa na tutaendelea kuwa hivyo kwa sababu tu kila mmoja kafika kusema umimi, umimi, ndio tumefika hapa na tutaendelea kufika hapa, kama hatukuwa *serious* na hatukuwa na maelekezo ya njia moja ya kuelekea kwenye *siratul mustakin.*

Mhe. Spika, nianze kumshukuru Mhe. Waziri wa Miundombinu kwa hotuba yake pamoja na uongozi wake Katibu Mkuu na uongozi wake mzima na Naibu Waziri. Mhe. Spika, kama nilivyosema sie sote humu ndani tumekuja kwa sababu ya maslahi ya wananchi. Mhe. Spika, nilipokuwa kwenye Jimbo langu la Uzini baada ya kupata bahati ya kuja kukaa kiti hiki, kabla sikuapishwa nilitangazwa na Tume ya Uchaguzi kwamba Jimbo la Uzini Mohamedraza Hassanali ameshinda.

Mhe. Spika, nilikwenda kwa Mkurugenzi wa Barabara, kwa sababu nina uchungu na nchi na wananchi ndio walionifikisha hapa nilipofika mimi. Nilipokwenda kwa Mkurugenzi wa Barabara tarehe 27/2/2012, nikazungumza naye kwamba bwana nimekuja, mkaa na maiti haachi kulia. Wenzangu kule Uzini kuna barabara, gari za ng'ombe hazipiti seuze binadamu. Kwa hivyo ninajua hali ya serikali imeshafanya mengi, wizara yako imeshafanya mengi lakini tunajua kwamba kuna hohe hahe. Kwa hivyo ninachoomba hizi barabara mkazikague, halafu mniambie nisaidie nini mimi, nikiwa kama Mwakilishi wa Jimbo la Uzini.

Mhe. Spika, Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu wakati analipeleka kule aliahidi barabara zote hizi kuzisaidia za ndani lakini nikasema hapana na mimi nisaidie. Mhe. Spika, nilipopeleka barua hii tarehe 27/2/2012 ikajibiwa tarehe 29/2/2012 kwamba barabara ya Pagali Umbuji 0.7 ni shs.11,178,000/=, Ndagaa Ndodongwe 1.7 ni shs.23,880,000/= kwa Kibawa Nyamatola 2.7 urefu shs.45,812,000/=, Ndondongwe Mkuku 0.2 urefu shs.6,200,000/=, jumla ni shs.87,070,000/= barua ya Serikali hiyo. Sasa nikamuendea Katibu Mkuu wa Miundombinu, nikamwambia bwana nimekuja nimepewa hii niambieni sasa mimi nisaidie nini. Kabla sijaapishwa kuingia huku wala mshahara sijaanza kuchukua. Katibu Mkuu kaniambia anamuandikia Mkurugenzi wa Barabara tukitaka tuifanye kazi hii mara moja na *estimate* hii ya shs.87,070,000/= basi utoe sasa hivi shs.20,000,000/=. Sikuapishwa bado lakini nina uchungu na nchi, bila ya wananchi mimi nisingelifika hapa na wenzangu kufika hapa, nikaambiwa nitoe *cash* shs.20,000,000/=. Katibu Mkuu kasaini anamwambia Mkurugenzi wa UUB tafadhali pokea shs.20,000,000/= na Wizara na Idara iliyobakia itakamilisha.

Mhe. Spika, kwa sababu nina uchungu na nchi na bila ya wenzangu mimi nisingelifika hapa nilikwenda kiwandani kuchukua shs/20,000,000/= nikazipeleka Wizara ya Miundombinu tarehe 1 mfungo tatu na mkataba wa Wizara ya Miundombinu wakaandika Jimbo la Uzini Mohamedraza Hassan kama nilivyotaja Pagali Umbuji, Ndagaa Ndodongwe na nyenginezo, nikatoa shs.20,000,000/= kwa makubaliano na Wizara ya Miundombinu, maana hata wangeliniambia nitoe zote ningeweza kutoa alhamdullillahi kwa sababu nina uchungu na nchi.(*Makofi*).

Mhe. Spika, baada ya kutoa fedha hizi nikamwandikia barua Katibu Mkuu tarehe 7/3/2012 wa Wizara ya Miundombinu utengezaji wa barabara zilizokaguliwa katika Jimbo la Uzini Unguja, nikiwa Mwakilishi wa Jimbo la Uzini Unguja nilitakiwa kuchangia shs.20,000,000/= fedha taslimu kwa ajili ya ujenzi wa barabara zilizokaguliwa katika Jimbo langu la Uzini, tayari nimeshalipa shs.20,000,000/= kwa ajili ya kazi hiyo.

Mhe. Spika, wakati mwaka jana tarehe 18 Julai 2012 kabla ya wiki mbili, nilikwenda Idara ya Barabara na Wizara ya Miundombinu nikawaambia jamani pesa mlizozitaka hizi nimezitoa, sasa nikawashtua ndio tatizo letu la nchi hii. Nikamwambia Rais anakuja Pagali tarehe 18 Julai 2012 kuja kufungua skuli ambayo nimeshirikiana na wananchi nimeijenga skuli ya kisasa, barabara ile ya Pagali kwa wiki moja tu ikawekwa sawa kwa sababu Rais tu anakwenda na ingelikuwa si Rais anakwenda isingefanywa kitu kwa ushahidi. Alipoondoka tu Mhe. Rais pale Pagali barabara hizi mpaka leo zote nimeekewa vikwazo.

Mhe. Spika, Januari 2013 tulikuwa kwenye mkutano pale Bwawani wa *Partnership* nikamwambia Mhe. Rais, hii nia tunayo ya kufanya kazi ya kuwatumikia wananchi, nikamtolea nyaraka, namwambia Mhe. Rais nilikuwa na mkataba na Wizara ya Miundombinu na mimi najua Serikali yangu ya Mapinduzi ya Zanzibar imeshafanya mengi lakini suala la kusaidiana mengi barabara, umeme, afya mambo mengi lakini siku nyengine hii haimo kwenye bajeti. Waziri wa Miundombinu na mzee wangu namuamkia shikamoo mimi baba yangu au babu yangu na nitaendelea kumuheshimu, akatoa ahadi Januari pale akasema mbele ya Rais mbele ya umma tumekubali kuna mashine imelala pale Pagali tutatengeneza kabla ya bajeti tutamaliza sehemu zote hizo, mbele ya Rais mbele ya umma, kimya mpaka leo.

Mhe. Spika, lakini mbali ya hivyo Mhe. Naibu Waziri *cassette* yake ninayo na hiyo *cassette* ya Mhe. Waziri ninazo, maana mimi ni mtundu wa kuweka rikodi, nina rikodi zaidi ya miaka 30 ya nchi hii kila mmoja aliyetoa kauli yake na mambo ambayo yaliyotokea katika nchi hii. Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano Mhe. Gavu alikuja Umbuji miezi mitatu iliyopita, suala la Umbuji nikamwambia masuala haya akaniambia inshallah Raza kabla ya bajeti hii tutakuwa tumeshamaliza maeneo hayo *cassette* ninayo. Sasa Mhe. Spika, *are we serious* katika nchi hii, maana yake tunakwenda kama shaghalabagala, nadhani tumekuja humu kwa sababu ya wananchi, leo tuko humu ndani kuwatetea wananchi wetu.

Mhe. Spika, mimi nakuahidi kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu kama Wizara ya Miundombinu barabara za wananchi wa Unguja na Pemba hizi za ndani kama tutawatengenezea wallahi nchi hii tutawalisha majirani zetu Mombasa, Tanga, Dar es Salaam na sehemu zote. Lakini leo Mhe. Spika, tunakwenda kutengeneza barabara hizi kutwa zinatiwa moto kwa sababu tu kuna tija pale, zinachomwa pale tunaona na wao ndio kuweka bajeti ile. Mhe. Spika, huko vijijini kuna maskini na njia ya kuwasaidia hawa ni kuwaondoshea matatizo ya miundombinu. Wizara ya Kilimo imekaa juzi hapa inasema ina matrekta ina kila kitu, Wizara ya Mifugo Mhe. Spika, ninamuomba Mhe. Waziri kama hamna miundo mbinu ya ndani, hakuna kinachofanyika na hatuwezi kuwa na kilimo wananchi kuwaondoshea umaskini kama hatujawawekea miundombinu ya ndani.

Mhe. Spika, mimi nina wazo, maana yake tunasema *when you have a problem you have to find the solution, when you have to find the solution you have to say what is next.* Sasa mimi niko tayari kusaidiana na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano, najua Serikali yetu haitoshi hebu aniambie humu ndani vijiji hivyo kuanzia Unguja, Pemba vyote hivyo waniambie kwa sababu gari tunayo, mchanga tunao, kokoto tunazo, sana itakuwa tabu kidogo. ni mafuta ya *diesel*, waniambie gharama zao zote hizi za vijijini lakini kwa

maskini huko waniambie nishirikiane nao. Mimi nina marafiki zangu Marekani, Uingereza, Denmark, Abu Dhabi, Oman na kama hawana mchanga tutaangizia kutoka nje, hawana kokoto tutawaletea ni lazima tuwe wakweli. Kwa hivyo niko tayari kushirkiana na serikali yangu watuambie kwamba kuanzia hapa Kiwani mpaka Mtambile, barabara hii inahitajia lita 2000 tutashirikiana lakini Mhe. Spika, tunakwenda tunafanya yote hayo kwa sababu tu ya wananchi, ndio ninachosema mpewa haponyeki, kama wenzangu wametangulia kufanya wasiwekewe vikwazo wananchi wa Jimbo la Uzini.

Mhe. Spika, mimi naomba na namuombaWaziri ninamuheshimu Katibu Mkuu. Wakati wa masika niliandika barua kuhusu tawi la Miwani. Nikawaambia masika skuli zimefungwa kumetokea na mvua na lile ni jambo la Mwenyezi Mungu niko tayari kuchangia, barua hii hapa ninajua bajeti hohe hahe na hii Serikali tunaijua, na hakuna hata barua moja niliyojibiwa zote hizi. Lakini tizama Mhe. Spika, leo nimemuandikia Rais wa Jamhuri ya Muungao hii barua yake, nimemuandikia kwa niaba ya wananchi wa Uzini na amejinibu hapa huyu Rais wa Jamhuri ya Muungano. Ninaandika barua Wizara ya Miundombinu mwaka mzima hakuna majibu, nimemuandikia Rais wa Jamhuri ya Muungano ameniambia Raza nipe muda mdogo nitakuja amekubali kuja katika Jimbo langu ni Rais wa Jamhuri ya Muungano Rais Jakaya Mrisho Kikwete na amejibu barua hii.

Mhe. Spika, Rais wa Zanzibar nimemualika mara mbili Jimbo la Uzini kwa sababu ya maendeleo, kwa sababu ya maslahi ya wananchi amenijibu na ametekeleza ahadi yake, hizi hapa barua imeandikwa siri. Sasa hivi kwa nini tuhangaishane kama una jambo huwezi, umetoa ahadi rudi kwa wananchi uwaambie bwana hili haliwezi kutekelezeka hali yetu hohe hahe, kuna misaada hatujapata lakini Mhe. Spika, hii nchi yetu sote Zanzibar ni *cosmopolitan* tulipofika hapa tumshukuru Mungu lakini tuwe wakweli. Leo Mhe. Spika, mimi namuonea sana huruma Mhe. Waziri wa Miundombinu na Katibu Mkuu wake ule wamechukua majukumu lakini ndio majukumu lakini kama hatukuwa wakweli, mimi nataka maelezo tu na nimepiga picha ninayo. Unajua Mhe. Spika, ushamba si kutokuwa mshamba ni kutofahamu mambo.

Mhe. Spika, barabara zetu mara nyingi wakati wa mvua za masika ndio zinatiwa lami. Sasa nipeni siri hii kuna nini, kuna uzuri, maana yake ikifika wakati wa masika ndio inatiwa lami inatengenezwa. Mimi Mhe. Spika, mshamba katika mambo haya, kuna sehemu tatu nimezipiga picha, ikifika msimu wa mvua ya masika huanza kutengenezwa barabara zile na kutiwa lami. Sasa angalau nifahamishwe na mimi nifahamu kuna usiri gani. Kwa masomo yangu niliyofika ya *Form IV* wakati wa masika tunatakiwa tusitumie kisima na mambo mengine kutokana na utaalamu kwa sababu utakuwa unajidanganya.

Mhe. Spika, tukiyaacha hayo hizi ni fedha za walipa kodi, leo Wizara ya Miundombinu, Idara ya Barabara inatia lami, kesho anakuja Idara ya Maji au *ZECO* wanakuja wanaichana ile barabara. Sasa Mhe. Spika, hivyo kweli hakuna *communication*, njia yetu ile sio sote maskini tumejenga barabara pengine dola milioni moja, sasa barabara imeshawekwa hiyo anakuja siku ya pili ZECO au Idara ya Barabara wanataka kupitisha mpira ile barabara inachanwa. Mhe. Spika, ukiichana barabara ile ni sawa sawa na shati lako iliyotoka kiwandani au koti lako likachanika inabidi ulishone haliwi kama lililokuwa mwanzo lililotoka kiwandani.

Mhe. Spika, mimi ninachoomba, hii nchi tuko hohe hahe, humu ndani tumekuja kwa maslahi ya nchi, vyombo hivi vikae viulizane kama barabara wana *plan* ya kutengeneza na kutia lami wenzetu wa Sirika la Umeme, wenzetu wa Shirika la Maji wakae pamoja, maana yule Shirika la Maji anasema mimi nitalipa fidia, hizi fedha za walipa kodi si zako, sasa kulipa fidia unaiumiza barabara unaumiza nchi. Sasa uzuri wa jambo Mhe. Spika, mimi ningeliomba kufanya kosa si kosa kurejea kosa, ni kosa hizi taasisi zikae kwa pamoja kuona kwamba jinsi gani hizi barabara, unataka kutengeneza barabara hii mwite Mkurugenzi wa *ZECO*, Mkurugenzi wa Maji, bwana eeh! barabara hii ipo tayari kutia lami na kuijenga, je kuna miundombinu nyengine inataka kupita kama simu, Idara ya Maji na Idara ya Umeme. Sasa hayo tutafikia mambo mengi kuepusha gharama lakini Mhe. Spika, yanaweza kufanyika mambo haya kila mtu anataka mteremko.

Mhe. Spika, jengine ninachotaka kusema na kumwambia Mhe. Waziri, Wizara ya Miundombinu na Wizara hizi za Kilimo na mengine haiwezi kutekeleza bila ya Wizara ya Miundombinu. Ninachoomba Wizara ya Miundombinu na namuomba Waziri angalau Waziri awe mkali na Katibu Mkuu, kuna baadhi ya Wakurugenzi tu wamefanya nafasi yao kuliko Mwenyezi Mungu, hatuwezi kwenda, kwa hivyo ninamuomba Mhe. Waziri hapa sote Mhe. Spika, ulipoona masuala 31 kila mmoja ana uchungu na nchi na kila mmoja anazungumza kwa maslahi ya nchi.

Mhe. Spika, mimi ushauri wangu kwa Waziri ninamuheshimu na nitaendelea kuwaheshimu na wenzangu lakini wawe wakweli, asikubali Waziri mtu mmoja au wawili wakaiumiza nchi kwa maslahi ambayo yao wenyewe. Kwa hivyo namshauri Mhe. Waziri na Wizara inayohusika wakae waamue mambo ambayo yenye maslahi na nchi na mimi tegemeo langu Mhe. Spika, kwa heshima na taadhima huu mkataba walionipa kwa maslahi tuliyokubaliana, mimi ninaomba wautekeleze *we are all in transit*, kwenye bajeti haimo humu, naomba watekeleze hizo na kama kuna mashine kule Mhe. Spika, imeharibika mashine ambayo ina thamani ya shs.300,000,000/= taarifa niliyokuwa nayo

mashine ile tatizo lake ni shs.16,000,000/=. Sasa ninachotaka kusema mimi kwamba sisi humu ndani hatuko na upinzani wala hatukuja kuleta ushindani na serikali. Ninachoomba Mhe. Waziri sasa hivi huko inasemwa Wizara ya Miundombinu matatizo yenye mgogoro tu.

Mhe. Spika, katika kumalizia nataka niseme kwamba maslahi ya Serikali yetu, maslahi ya nchi yetu na maslahi ya wananchi wetu tuyaweke mbele, yule hawezi atusamehe lakini tumeona leo *airport* mpya ile bilioni ngapi zimetumika; yaani matatizo sehemu zote za migogoro na hizi pesa za walipa kodi. Sasa Mhe. Spika, mimi naomba kushirikiana na Wizara inayohusika na tena niko *very serious* aniambie hizi sehemu za barabara za ndani za wakulima kutoka Uzini na nitakwenda mpaka Micheweni, nitakwenda sehemu zote kushirikiana na Serikali yangu na wananchi wangu kusaidia, si *diesel* nitawaambia tu mimi nina uwezo wa kufanya hivyo wala sitaki posho wala sitaki tiketi, wananchi wamenifikisha hapa na nyie ndio mlionipitisha hapa nitasaidie waniambie tu lita ngapi. Lakini haiwezekani tukenda watu maskini, barabara hazipitiki za ndani Mhe. Spika, nina uchungu kwa sababu ninazijua hizo barabara yule ng'ombe ninamuonea huruma mimi seuze binadamu. Mama zetu wanapoteza maisha yao, leo unamuwekea mtu barabara za ndani ana gunia la muhogo akifikisha marikiti yule muuza marikiti anakuwa tajiri hata ile fidia yake aliyoifanya ile kazi *Wallahi* Mhe. Spika, haipati.

Mhe. Spika, mimi nishukuru sana, niwashukuru wananchi wa Jimbo la Uzini, lakini pia nishukuru Baraza lako tukufu na mategemeo yangu kwamba tutafika pahala tuwekeni maslahi mbele. Ahsante sana Mheshimiwa.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia wizara hii muhimu sana katika maendeleo yetu. Kwanza naomba nimpongeze pamoja na yote Mhe. Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu kwa namna wanavyojitahidi kupapatua gamba gumu, lakini hali inaonekana kwa kweli ina mashaka.

Mhe. Spika, mimi sitochangia sana kwa sababu ya mambo hasa kwa siku ya leo, lakini naomba niseme kwamba wizara hii ni muhimu sana, Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano ni wizara muhimu sana hasa kwa maendeleo ya uchumi wa nchi yetu. Hatuwezi kuzungumzia masuala ya uchumi kama hatujazungumzia suala zima la miundombinu kwa sababu ndio uchumi wa nchi.

Mhe. Spika, ni ukweli kwamba tumekuwa tukitatizika sana katika kupiga hatua katika suala zima la uimarishaji miundombinu katika nchi, mwendo unakuwa ni wa kusuasua licha ya serikali mara kwa mara kuahidi kwamba

itafanya hiki na kile, lakini inaonekana kwamba tuna *mark time* hatwendi mbele katika hili. Sasa basi ni vyema tufike pahala Mhe. Spika, Baraza lako na sisi Wawakilishi tuweze kufikiria na kufanya tafakuri tufanye nini, si suala la kwamba kila mwaka tuletewe maneno tu, inavyoonekana hapa ni *trend* kwamba kila mwaka tunaletewa maneno yanakwenda awamu inapita lakini kwa kweli hakuna hatua.

Sasa nadhani kupitia bajeti hii ambayo imekuja katika kitabu cha kutisha hehee! vitabu vyote vinakuja na sura nzuri lakini hiki cha leo! Nadhani Mhe. Spika, na niwashauri sana wenzangu Waheshimiwa Wawakilishi tutafakari sana bajeti hii tufike pahala ikiwezekana tufanye maamuzi magumu lakini kwa maslahi ya nchi yetu na hili si geni.

Bajeti iliyopita ya Jamhuri ya Muungano, Bunge lilisita kwa muda wa siku na likaunda kamati maalum ikaunda tume maalum na ikasitisha bajeti ya Wizara ya Maji nafikiri. Kwa hivyo, Mhe. Spika, ikiwezekana na sisi licha ya ukwasi wa muda tulionao na siku kuu iliyotuelekea lakini katika kutimiza mambo ya msingi sisi tuko tayari kufanya kazi hata siku kuu kwa ajili ya hili. Ninachokizungumza hapa ni suala zima linalohusiana na mustakabala wa taifa letu.

Mhe. Spika, bajeti yetu imekuja na sura ile ile ya kawaida, ina sura kuwa na bajeti ile ya matumizi ya kawaida, yaani *OC.* Hili sina tatizo nalo kwamba lazima wizara ipo na lazima iendeshwe lakini hofu na shaka yangu iko katika suala zima la bajeti, fedha zilizotengwa katika bajeti ya maendeleo. Mhe. Spika, mimi katika hapa kwa kweli nitakuwa na matatizo na sina mashaka katika fedha zilizoombwa kutengwa na serikali juu ya bajeti ya maendeleo, kwa sababu najua hili kutokupatikana kwa fedha hizo si tatizo la Mhe. Waziri ni tatizo la serikali kuu katika kutoa vipaumbele kwenye mipango yake ya maendeleo.

Mhe. Waziri alipokuja mwaka jana aliniahidi kwamba atalishughulikia kama anavyokereketwa yeye binafsi na Uwanja wa Ndege wa Pemba. Ni hadithi ya miaka mingi iliyopita na itaendelea kuwa ni hadithi ya miaka mingi ijayo. Mhe. Waziri akanambia kwamba atajitahidi kwa mwaka ule wa bajeti alishughulikie, bajeti imepita na hadithi ni ile ile tumeona tena katika hili. Naamini kwamba hajapata fedha ndio maana asitekeleze lakini hiyo lawama si yake ni lawama ya serikali kuu kwamba haioni umuhimu wa kutoa vipaumbele katika mambo ya msingi. Tatizo langu Mhe. Spika, litakuja na leo ndilo nitakalozungumzia eneo hilo ni kuhusiana na matumizi mabaya na yasiyoeleweka juu ya fedha hizi zinazotengwa. Hapo Mhe. Spika, ndipo ninapojenga hoja.

Naomba nianze na suala zima la kutaka ufafanuzi wa bajeti katika suala zima la baina ya Mfuko wa Barabara na bajeti inayotengwa kwa ajili ya matengenezo ya barabara, kwa sababu kwa mujibu wa utafiti wetu tuliofanya takriban barabara zote hizi zinazojengwa na zinazofanyiwa matengenezo zaidi ya asilimia 80 ni fedha zinazotolewa na Mfuko wa Barabara na katika mfuko huu huwa kuna sehemu mpaka matengenezo ya zana zinazotumika. Lakini leo Mhe. Spika, bajeti hii na nyengine zilizopita huwa kunatengwa bajeti maalum, tunaidhinisha bajeti maalum katika idara hii juu ya matengenezo na ujenzi wa barabara hizo. Bajeti ya Mfuko hapa haipo bajeti ya Mfuko iko kwenye Wizara ya Fedha, maana yake ni kwamba hapa kunaonekana kuna bajeti mbili kwa wakati mmoja, kuna bajeti inayotoka wizarani tunayoidhinisha katika Baraza hili na bajeti inayotengwa na Mfuko wa Barabara inafika pahala hatujui tunatekeleza vipi.

Sasa naomba tufike pahala tupate ufafanuzi na si suala la ufafanuzi tu kwa sababu tutake kujua namna ya fedha tunazoziidhinisha kupitia idara hii. Lakini vile vile tutake kujua namna ya fedha zinazotokana na Mfuko wa Barabara kwa sababu inawezekana kwamba kitu kimoja kinatumika na bajeti mbili ambazo hatuna hapa. Hivyo Mhe. Spika, mimi siwezi kuidhinisha kwa sababu katika hali yoyote hapa katika ukumbi huu hatuwezi kupata jawabu muafaka. Hili ni jambo ambalo linahitaji kuchunguzwa si kwa bajeti hii tu lakini hata bajeti mbili tatu ili tupate kuanzia yale ya nyuma. Fedha zilizotoka serikalini zilizoidhinishwa hapa na fedha ambazo zinaidhinishwa na Mfuko wa Barabara kupitia Wizara ya Fedha. Kwa hivyo, mimi nahitaji hapa papite uchunguzi, uchunguzi juu ya bajeti hizi mbili zinazotumika kwa kitu kimoja.

Lakini la pili Mhe. Spika, ni suala zima la ujenzi wa barabara tatu ambazo tumezowea kuzisikia katika Baraza hili. Kuna barabara ambayo ni maarufu barabara ya Wete/Gando, Wete/Konde na Wete/Chake Chake. Mhe. Spika, hili ni tatizo, mara hii tumetakiwa tuidhinishe shilingi bilioni saba ambazo zitatolewa na mfadhili pamoja na shilingi bilioni tatu ambazo zitatolewa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Mhe. Spika, mimi binafsi sishawishiki na nawaomba wenzangu wasishawishike kuziidhinisha pesa hizo, tunaidhinisha fedha lakini wakati huo huo tunaambiwa tayari mkandarasi kishakimbia hayupo tunafanya nini, hatma ya mkandarasi ni ipi na kwa nini akakimbia?

Katika Baraza hili hili kwa kweli tuliuliza kwamba kwa siku moja aliyoiumba Mwenyezi Mungu serikali inaingia gharama, Mhe. Waziri akaulizwa lakini akasema hana *figure*, akakubali kwamba ni kweli serikali inaingia gharama kupitia hili, gharama ni kiasi gani sisi hakutwambia lakini tulimwambia ni zaidi ya shilingi milioni kumi kwa siku serikali inaingia gharama. Sasa leo tunaambiwa tuidhinishe fedha tena kama hizi shilingi bilioni tu kwa serikali na shilingi bilioni wakati hatujui hatma ya barabara hizi ni zipi, mkandarasi

tayari *MECO* kishakimbia na vitu vyengine. Mhe. Spika, mimi siko tayari kuidhinisha fedha hizi kama iwapo hatujapatiwa jawabu za kina, wala si jawabu tu za Mhe. Waziri kwenda pale akatujibu ndivyo sivyo aah! hapana, tunataka kupitisha uchunguzi ili tuweze kupitisha bajeti hii.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo hili nalo pia linahitaji uchunguzi na Baraza hili lijitosheleze ili liweze kuidhinisha ni suala zima la ujenzi wa *terminal* mpya. Tuliambiwa na kila mmoja ni shahidi kwamba *terminal* kwa maelezo tunayoyasikia kuwa imefeli, tukaambiwa kwamba mshauri nasaha, sijui mshauri gani kakodiwa au atakodiwa tena mshauri mlekezi kwa ajili ya kuja kuiambia serikali kwamba jengo limefeli. Sasa Baraza tunahitaji kujua ripoti za hao washauri welekezi hatuwezi kuidhinisha fedha kama ikiwa hatujajua mustakabali wa jengo lile.
Mhe. Spika, mjumbe aliyenitangulia kaeleza ni mabilioni ya shilingi yaliyotumika katika jengo lile, leo hatujajua mustakabali wa jengo lile tuidhinishe tena fedha haiwezekani, mara tulisikia jengo linataka kutiwa viringi sijui liondoshwe, sijui vipi. Kwa hivyo, Mhe. Spika, hatuwezi tukaruhusu kuidhinisha fedha ni eneo la ujenzi wa *terminal* mpya, lazima tupate majibu na ikiwezekana tupate ripoti kabla ya kuidhinisha bajeti hii.

Mhe. Spika, eneo jengine ambalo linahitaji uchunguzi maalum ni suala zima la ujenzi wa barabara ya Amani/Mtoni. Inavyoonekana kwamba lile sasa ni chaka, barabara ya Amani/Mtoni ni chaka tunazo taarifa hapa, nyinyi ficheni lakini mimi taarifa ninazo na taarifa ipo hii kwamba kuna ufisadi mkubwa katika ujenzi wa barabara ya Amani/Mtoni. Siwezi kusema hapa ni eneo gani na eneo gani lakini nasema ripoti ipo kwamba kuna ufisadi wa hali ya juu. Sasa hivi kila kinachotokea Amani/Mtoni Baraza hili Mhe. Spika, haliwezi kutumika katika kuhalalisha uovu. Kwa hivyo, eneo hili Mhe. Spika, tunahitaji kupatiwa taarifa na ikiwezekana kama nyinyi hamna sisi taarifa tunazo.

Mhe. Spika, katika bajeti hii barabara sita zile za Kaskazini Pemba zimetajwa ambazo zimeombewa jumla ya shilingi 150, kwa upande wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar lakini kuna bilioni nne kutoka kwa wafadhili. Kadri tunavyofahamu kwamba barabara zile zinafadhiliwa na *MCC,* hatuna taarifa kwamba *MCC* kuwa fedha hazikutosha na kauli nyenginezo, leo barabara zile kama ya Daya/Mtambwe, Kipangani/Kangagani na sehemu nyengine kwa sababu ni miradi inayofadhiliwa na *MCC*. Taarifa tulizonazo kwamba hakuna tatizo la fedha katika miradi ile, iweje leo tena waombe fedha au wanataka kuhaulisha fedha hizo wazipeleke katika sehemu nyengine. Baraza hili haliwezi likaidhinisha fedha hizi *unless* tupate taarifa kwamba fedha zilizomo katika *MCC* zimepungua au namna yoyote ile.

Mhe. Spika, eneo jengine ambalo wenzangu wamelielezea lakini na mimi naomba niligusie ni suala zima ambalo hilo ni jambo linanihusu mimi binafsi kama Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza Mahesabu ya Serikali. Tuliomba taarifa kupitia wizara kwa Idara hii ya *ZMA*, bahati mbaya sana, nasikitika sana licha ya kwamba kamati tuna mamlaka kamili ya kudai taarifa zozote zile ambazo hatupaswi kuzijua zimeelezwa ndani ya sheria. Mhe. Spika, kamati yako imenyimwa taarifa na si kamati tu, ukiinyima kamati taarifa maana yake umelinyima Baraza la Wawakilishi, ukiidharau Kamati ya Baraza maana yake umelidharau Baraza la Wawakilishi. Sasa sisi hatuwezi kuvumilia kudharauliwa chombo hiki, tena kudharauliwa na mtu mdogo sana katika nchi hii haiwezekani.

Mhe. Spika, tulidai katika Kamati ya Wenyeviti, mimi binafsi nilimuuliza Mhe. Waziri wa Fedha, hebu twambie wewe unataka kukusanya na unataka kutumia, lakini twambie ni kiasi gani cha fedha umekipata kupitia *ZMA* iliyopo Dubai. Tunajua kwamba chombo hiki kuna nchi sasa hivi uchumi wao hutegemea taasisi kama hii tu katika kuendesha nchi, Liberia inaendesha uchumi wake kwa ajili ya kutegemea usajili wa meli za kigeni tu, Kenya sasa hivi na wao uchumi wao mkubwa wanategemea usajili wa meli za kigeni, Zanzibar tuna kituo ambacho kwa kweli kinasajili meli za kigeni.

Mhe. Spika, takwimu zimetolewa hapa Mhe. Waziri wa Fedha akasema mimi sijui taarifa, nikamwambia mimi taarifa zinaonesha kwamba tuna meli 406 tangu pale mwaka 2008 hadi leo umekusanya kiasi gani? Waziri wa Fedha hajui hadi leo amekusanya kiasi gani? Lakini licha ya kunyimwa taarifa mimi taarifa ninayo hapa ni mabilioni kwa mabilioni ya shilingi ambayo kwa kweli Zanzibar inakosa kupitia hili na ndio sababu kamati yako Mhe. Spika, ikanyimwa. Sasa ikiwa Baraza linanyimwa taarifa kuna uhalali gani sisi wa kuidhinisha bajeti, tutawafanyia vipi wananchi wetu haki iwapo tutapitisha bajeti hii. Mhe. Spika, kila mmoja ana eneo lake la kujidai na eneo letu la kujidai sisi Wawakilishi ni katika ukumbi huu.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, mimi binafsi nawashawishi wenzangu ikiwezekana bajeti hii iakhirishwe, si jambo geni iundwe kamati kwa ajili ya kuyaangalia maeneo haya, kwa sababu kwa vyovyote vile naamini kwamba Mhe. Waziri pale atakuwa hana jibu la kuturidhisha katika mambo haya. Kwa vyovyote vile iundwe kamati maalum ikakae pamoja na wizara kuyapitia maelezo haya ndio baadae tuje tuipitishe bajeti hii.

Mhe. Spika, naomba nimalizie kwa nukuu ya mshairi mmoja maarufu sana Mhe. Shaaban Robert alisema, “Kuna hekma katika upumbavu wa mtu mpumbavu”. Mhe. Spika, nakushukuru.

Mhe. Asha Bakar Makame: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametuwezesha siku hii ya leo kuingia katika shughuli zetu hizi lakini hasa Wizara hii ya Miundombinu na Mawasiliano.

Mhe. Spika, pamoja na yote nimpongeze Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wake wote waliopanga miundombinu yao ambayo kwa kweli imetuonesha sura mbaya. Mimi nasema kwamba hii ni lami itufunike na lami ikikaa pahala usoni itatukunyaza, hii ni lami wamekusudia lakini lami hii si ya kuwatia binadamu, lami hii ni ya barabara. Pamoja na yote lakini hili tabu halikukaa vizuri. Niungane mkono na wenzangu kwamba kwa kweli weusi huu hata sijui niite weusi wa nini. Lakini kwa kweli wanatuonesha dhahiri kwamba haya mambo tuyafumbie macho maana ukifumba macho unaona nini, si unaona kiza tu na weusi, lakini sisi Mhe. Spika, hatutofumbi macho.

Kwanza mimi nipongeze kwamba tumetimiza ile Serikali ya Umoja wa Kitaifa nimuunge mkono Mhe. Mohamedraza Hassanali pale, kwamba tuko katika Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Humu hamna mpinzani, upinzani tukitoka hapa tunakwenda kwenye viriri ndio tunatukanana huko kila mtu na chama chake, lakini hapa dhamira kubwa ya kuundwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa Mhe. Spika, ni kuhakikisha tunaungana pamoja tunatetea wananchi wa nchi hii. Lakini pia tunaihimiza serikali ifanye yale ambayo tumeletwa kwa ajili ya wananchi kuwatatulia matatizo yao.

Mhe. Spika, wasemaji wawili hawa kidogo wamenifilisi lakini na mimi nitaeleza, kwa sababu hii ilikuwa ni miongoni mwa Kamati Teule, sasa mawasiliano tunaijua *A to Z* hakuna atakayetudanganya. Mimi niseme Mhe. Spika, kwanza ununuzi wa meli. Serikali dhamira yake ni nzuri sana kwa wananchi wake hapa nitakuwa sina la kusema nimpongeze Mhe. Rais pamoja na yote, lakini lazima Mhe. Rais nimpongeze kwa kukubali kuchukua pesa kila wizara kuhakikisha kwamba kunanunuliwa meli.

Mimi leo kidogo nimeingia moyo kwa Mhe. Waziri alivyosema kwamba mwaka 2013 kidogo nilipata moyo, kwa sababu juzi hapa tuliambiwa mwaka 2015. Sasa leo kidogo nimeingia moyo. Ninaiomba serikali pamoja na wizara husika ya Miundombinu isije ikafika mwaka 2014 tukaja tukapigwa bwabwasa hapa hatutokubali, kasema mwaka 2014 aliposoma kitabu, kama kakosea aseme. Hilo moja.

Lakini jengine Mhe. Spika, nizungumzie barabara. Kwanza nisiwe mwizi wa fadhila niipongeze serikali kwa upande mmoja lakini baadae nitakuja kuisakama kwa kujengewa barabara kutoka Bahanasa/Mtambwe/Daya na mzunguko wake wote naipongeza. Lakini suala hili ni la miaka mingi lazima

niseme. Kwanza nishukuru awamu zilizopita. suala hili nililiomba toka mimi mwakilishi wakati huo Mhe. Amani Abeid Karume alikuwa Waziri wa Mawasiliano na Mwenyezi Mungu akajaalia akawa Rais, nikamwendea akanambia kama haikujengwa kwa Mfuko wa Barabara basi itajengwa kwa pesa za wafadhili. Nisiwe mwizi wa fadhila nimshukuru Rais ambaye yuko madarakani sasa hivi kwa sababu na yeye ameendeleza yale ambayo ameyaacha mwenzake. Nishukuru sana na niwatakie kila la kheri.

Mhe. Spika, lakini mimi nasikitika sana kwenye kitabu hiki, jamani msije mkanishuku nagombea huku na huku, maana Unguja na Pemba ni visiwa sawa sawa hivi isipokuwa ukubwa tu kidogo tumezidiwa hapa na sisi kule tuna haki. Kitabu hiki ukurasa ule ambao unaelezea habari ya barabara lakini halafu kuna kurasa hizi zinazoonesha barabara zilizojengwa kuanzia ukurasa wa 61, 64 na 67.

Mhe. Spika, ninavyoelewa mimi kodi inayolipwa kwa mambo yoyote hapa Unguja basi na Pemba inalipwa. Mimi kilichonishangaza Mfuko wa Barabara barabara zote zilizotajwa humu na toka mwaka gani sijui mpaka leo, ni barabara za Unguja. Hili nalisema kwa nia safi kabisa, Sasa huu Mfuko wa Barabara kule Pemba watu hawalipi, niulize swali langu hilo hawalipi? Kama wanalipa kwa nini barabara za Pemba hazijengwi katika Mfuko huu hamna toka mwaka elfu mbili na ngapi sijui hata huo mwaka 2013/2014 hamna zilizomo ni hizi hizi ambazo zinaendelezwa. Hilo moja.

Halafu mimi nauliza hii barabara ya kutoka Gando/Wete iliyoanzia Bopwe kuelekea Gando ina madhambi gani, barabara kutoka Wete kwenda Konde ina madhambi gani, barabara kutoka Chake-Chake kuja Wete ina madhambi gani. Naomba Mhe. Waziri hapa akiacha mengine nitakayoyazungumza kama sikupata maelezo ya kuniridhisha basi baada ya hili tutakalokuwa hatupitishi pesa hili fungu na hii sipitishi fungu Mhe. Spika.

Nikiondoka hapo Mhe. Spika, nije katika malipo ya Uwanja wa Ndege kwa watu ambao walichukuliwa sehemu zao zenye mazao, zenye nini; kuna siku hapa tuliuliza tukaambiwa watu wote wameshalipwa hakuna mtu hata mmoja aliyekuwa hajalipwa. Mhe. Spika, nina vielelezo hapa kuna sehemu ambayo ya makaburi ya wenzetu akina Mzee Majaliwa; nitamuomba sana Mhe. Waziri maana kuna barua zimeandikwa kwa sababu hili ni shamba la Bibi Luice Majaliwa limeandikwa kila barua, mabarua yote yameandikwa mawasiliano na nini lakini hakuna jawabu ambalo watu wote wengine wamelipwa isipokuwa kuna watu watatu ambao hawajalipwa. Shamba hili Mhe. Spika, lina waraka tokea enzi za akina Sayyid Khalifa.

Kwa hivyo, nataka nije nipate jawabu ni sababu zipi ambazo pamoja na barua kuandikiana lakini wizara hii wasiwalipe na hawa wenyewe hawakukataa. Hiyo sehemu waliyonayo ilikuwa imetiwa uzio wakasema basi na hii sehemu ya mita 20 tutaichukua, huyu usiichukue ilimradi ni kuvutana tu watu hawaelewani. Na wao wamesema sisi hatuwezi tukavutana na serikali, tunaijua serikali hatuwezi tukavutana nayo. Namuomba Mhe. Waziri aje anipe maelezo madhubuti hakunipa maelezo madhubuti kama kawaida.

Mhe. Waziri kasifu hapa wafadhili wa nje na ndani lakini kweli hii *ZAT* haikufanya chochote pale Uwanja wa Ndege? Sikuona mimi humu *ZAT*, wakati *ZAT* mfano wake ndiyo iliyoleta mambo mengine, si kwa sababu Mhe. Raza ndio mwenye *ZAT*, angefanya vibaya tungemsakama humu humu. Lakini kwa kweli hii *ZAT* ndio iliyoanzisha jamani basi hata kuitaja tu msiisifu itajeni tu, mmetaja watu ambao ndio wameletwa na *ZAT* mfano wake. Hilo Mhe. Waziri ni kosa.

Lakini jengine nije katika Uwanja wa Ndege wa Pemba. Mhe. Spika, hivi karibuni kikao kilichopita tuliuliza baadhi ya maswali humu na moja likawa ni la Uwanja wa Ndege wa Pemba. Mimi niliuliza swali la nyongeza, nikaambiwa maana yake tutatia taa kabla ya bajeti. Sasa namuuliza Mhe. Waziri zile taa zimeshatiwa?

Mhe. Spika, mimi naiomba serikali ikae ifikiri, itafakari ule si uwanja wa ndege wa Pemba jamani, sisi Waheshimiwa wako tukisema tuchangishane humu uwanja kama ule tunaweza tukaujenga, lakini leo uwanja ule miaka yote jamani hauna lolote hivyo kweli ni haki. Halafu umepewa jina kubwa la Karume, jina kubwa lile si dogo, sasa sijui Karume mkubwa au mdogo. Kama ni Karume mkubwa kwa kweli hatumtendei haki kwa jina lile na uwanja ule ulivyo. Naiomba wizara jamani sitaki nikumbushe kilio matangani. Kuna siku aliumwa mkubwa pale mimi nakumbuka ilikuwa kizazaa usiku kutaka kumsafirisha, tusifanye jamani mambo mengine tutizame mbele hebu tubadilike.

Mhe. Spika, lakini sishangai nitawaomba Waheshimiwa wenzangu tuvae nguo zile za *superman* yanayozuia magari tutoke hapa kwa pamoja twende *airport* hiyo hapo tukalisogeze lile *terminal* lililojengwa ili hiyo *terminal* nyengine ianze kujengwa. Lakini kwa kweli Mhe. Spika, hili mimi sitaki nilizungumzie sana maana tulilizungumza hapa tukaelezwa maneno mengi wenzangu wameshazungumza naomba kwa kweli jamani pesa za watu za wavuja jasho tunaziumiza. Hebu leo tuje kuelezwa hapa na kwa busara kuhusu ile *terminal* na tulieleza tukasutwa humu mfano wake kama kusutwa Mhe. Spika, samahani kuzungumza neno hili kusutwa. Kweli tukaambiwa

kuwa aah! mkandarasi ndivyo alivyosema, sijui nani alisema lile lile ndio zuri, leo tumeambiwa halifai tuje tuelezwe.

Mhe. Spika, mimi nimalizie maneno mawili, nimalizie na mashirika yetu ya ndege haya madogo madogo sisi wengine hatujui hata kuyatamka. Mimi nimuulize Mhe. Waziri hakuna sheria katika nchi pamoja na kwamba wanatusaidia usafiri wa angani lakini hakuna sheria. Saa nyengine unaachwa na ndege pale unaambiwa ngojea mpaka irudi iende wapi wanakuacha na ndio ndege yako. Saa nyengine wana-*delay* wananyamaza kimya mpaka wewe mwenyewe unaona tafrani mpaka ukaulize.

Mimi natoa wito kwa wananchi ndege yoyote iki-*delay* tudai haki zetu. Kuna sheria iki-*delay* ndege ulipwe kwa sababu kuna wengine wafanyabiashara Mhe. Spika, wanaagana na watu wana *appointment* zao lakini wanachelewa kwa ajili ya uzembe wao wenyewe mashirika yetu haya madogo madogo yalioko nchini. Sio mashirika makubwa kwa sababu mashirika makubwa wanajua taratibu na sheria. Sasa mimi nauliza na sisi hapa sheria au kwa sababu sisi Waafrika ndio watufanyie mambo ya ki-Afrika Afrika hapa Unguja. Naomba hilo Mhe. Waziri lishughulikiwe.

Mhe. Spika, la mwisho wenzangu wamezungumza Mhe. Hija Hassan Hija amezungumza sana na mimi niunge mkono na hata Mhe. Omar Ali Shehe amezungumza. Lakini nasema kwa kweli ubinafsi tuuache. Haya yote Mhe. Spika, ni ubinafsi hatuna ukweli, ubinafsi umetutawala na ndio unaotuongozea mabaya na ndio unaotufisidia serikali yetu.

Lakini nitakuwa ni mwizi wa fadhila Mhe. Spika, kama sikumpongeza Bahressa pamoja na yote kwa sababu yule ni mzalendo wa Zanzibar hii. Nimpongeze sana tena sana jinsi alivyotufanyia kazi pale bandarini, *wallahi* utafikiri huko Unguja. Nimuombe ndugu Bahressa kwamba bado aendelee na uzalendo wake aendelee kutusaidia na sisi tuko pamoja naye.

Mhe. Spika, naiomba Serikali mzalendo kama huyu akijitokeza, basi apewe yale masharti tu, apewe nafasi wasiingie watu tena kijuu juu wakaweza kumsakama. Baada ya hayo siungi mkono hoja mpaka tupate maelezo yatakayoturidhisha katika hii Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, na mimi nashukuru kupata nafasi hii ya kuzungumza machache kuhusu hotuba hii ya bajeti ya mwaka 2013/2014 ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano.

Mhe. Spika, kabla ya kuanza kuzungumza chochote kwa kufuata maelezo yako ya asubuhi ya leo kutoa shukurani kwa Mwenyezi Mungu kutujaalia

kwa siku ya leo ya tarehe 31/07/2013 kwa kusimama hapa ikiwa ni siku tukufu kwangu.

Nafikiri hii ni siku ambayo wananchi wa Zanzibar kwa pamoja wakiongozwa na Tume ya Maridhiano walipiga kura ya kuchagua muundo mpya wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa na Mwenyezi Mungu katukubalia asilimia 67 ya wananchi wa Zanzibar walikubali kuwa na muundo mpya wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa na leo hii tunayo Serikali wengi wanaita Serikali ya Umoja wa Kitaifa.

Lakini katika Katiba ya Zanzibar inaandikwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yenye Muundo wa Umoja wa Kitaifa. Namuomba Mwenyezi Mungu atujaalie iwe ni Serikali ya Umoja wa Kitaifa mia juu ya mia na isiwe yenye muundo tu.

Pia nitoe shukurani kwa wale waliotuelimisha wakatuelekeza na tukafahamu mpaka wananchi wakakubali kuwa na Serikali yenye muundo mwengine na hawa kwa ruhusa yako naomba niwataje majina ni pamoja na:-

1. Mhe. Ali Mzee Ali - Mwenyekiti.
2. Mhe. Abubakar Khamis Bakar
3. Mhe. Nassor Ahmed Mazrui
4. Mhe. Zakiya Omar Juma
5. Mhe. Haji Omar Kheir
6. Mhe. Ali Abdalla Ali

Mwenyezi Mungu atujaalie juhudi yao na kazi yao kubwa walioifanya iendelee kuzaa matunda mpaka tufikie Serikali ya Umoja wa Kitaifa iliyokuwa ya Umoja wa kikweli kweli.
Jengine Mhe. Spika, mimi pamoja na kuwa kitabu hichi tuliokuwa nacho tena nasema kwa nia safi kujua kwamba kitakuwa kizuri kwa namna hii rangi ni nyeusi lakini *wallahi* ni kizuri sana, kinavutia kimesomwa vizuri msomaji nampongeza na watungaji. Lakini kwa masikitiko makubwa kimeacha mambo mengi sana na hakikuonesha hasa ni namna gani kitaleta mageuzi ya makusudio ya wizara hii kwa maana ya kusongo mbele. Kwa hivyo, mimi binafsi nailaumu sana wizara safari hii hawakuwa makini na kuangalia tunachokitaka wametunga tu kwa maana ya kuwa kitabu kipo. Lakini hata hivyo kwa sababu hiyo naomba nizungumzie machache na wala sikufurahika na kitabu hiki na ningelikuwa na uwezo ningeomba kikatungwe chengine.

Mhe. Spika, tuanze na Shirika la Bandari. Tukiangalia Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano ni wizara ambayo ina sehemu kubwa ya kukusanya mapato katika nchi hii kuliko wizara yoyote. Na moja ni Shirika la Bandari.

Mhe. Spika, katika visiwa vyetu vya Zanzibar; Unguja na Pemba tuna bandari 5 zilizokuwa ni rasmi. Bandari ya Malindi, Mkokotoni, Mkoani, Wesha na Wete. Mhe. Spika, toka nyuma tulikotoka tuliona ili tuingie katika ushindani ni lazima kwa makusudi tuziimarishe bandari zetu kwa sababu ndizo zinazoingiza mapato makubwa sana. Sisi si peke yetu tuliozungukwa na bandari hata ndugu zetu wa damu wa Tanzania Bara ambao kesho kutwa watakuwa Tanganyika vile vile wana bandari. Lakini wao kila uchao wanaimarisha bandari zao. Hivi sasa wana mpango mkubwa sana wa kujenga bandari kubwa sana kule Bagamoyo ambao kama na sisi hatukuingia ndani ya ushindani itakuwa ni sababu ya kuangusha uchumi wa Zanzibar.

Siku nyingi na ni miaka mingi tulisema Mhe. Spika, kwamba bandari kuu ya Malindi Zanzibar inahitaji matengenezo makubwa na inahitaji kuongezwa na tukakubaliana kuwa juhudi ya Serikali itakuwepo ili kuona kuwa Mpigaduri kumeongezwa gati kubwa sana ambayo itasaidia uchumi za Zanzibar, lakini humu halikuzungumzwa lolote inasikitisha. Sisi tunajua kuna watu wamekuja hapa na wanataka kuekeza hivyo na Serikali imewapokea na juzi Mhe. Waziri wa Fedha alizungumza mpango wa kutia mkataba, lakini humu haikuzungumzwa chochote kama kile kitu hakipo. Hii inanisikitisha sana kweli kweli.

Jengine pale katika bandari ya Malindi tunacho kitega uchumi kikubwa sana na hii tunasema ni Chelezo. Wakati ndugu yetu Mustafa Aboud Jumbe alipokuwa ni Mkurugenzi Mkuu alijitahidi na kujenga Chelezo kile ambacho kimeshatumika na kuingiza fedha nyingi na alikuwa na azma ya kukipeleka maji mengi zaidi ili mpaka meli kubwa ziweze kupandishwa Chelezoni na kuingiza fedha katika bandari na kuingiza fedha katika mfuko wa taifa.

Haikuzungumzwa chochote kama kitu hiki kipo na kinafanyakazi. Kwa hivyo, nasema tena Mhe. Waziri wa watendaji wake hawakuwa *serious* kuonekana tufanye vipi katika wizara ili tuone kuwa tuna azma ya kukuza uchumi kwa kutumia bandari zetu kama wengine wanavyofanya.

La kusikitisha zaidi tunajua Pemba tuna bandari 3 kubwa ikiongozwa na bandari ya Mkoani, hakuna asiyejua kwamba kuwa bandari ya Mkoani sasa iko katika matatizo, hakuna asiyejua kwamba kule chini ya bandari ya Mkoani kumesegekwa mawe kama ilivyo juu na kila siku kwa sababu ya

vyombo vinavyoingia na maji yanavyopiga ndivyo inavyochimbika na hivi sasa sehemu kubwa yake imezama.

Tuliambiwa huko nyuma kwamba bandari hii itakuwa ni mlango mkuu wa kupitia katika vyombo vya kimataifa, yaani itakuwa bandari ya kimataifa. Lakini inazidi kufa na kilichozungumzwa humu ni kutengeneza ile sehemu ambayo meli zinagonga na zikachimbuka chimbuka basi hakuna jengine. Mimi nilifikiria kwa sababu nafasi ipo na tunaingia katika uchumi Mhe. Waziri ataeleza kuwa ana azma gani ya kuikuza ile bandari ya Mkoani wakati ndio bandari mkubwa inayotumika hivi sasa.

Ikikuzwa bandari ya Mkoani ni kuingiza uchumi Zanzibar, ni kuwasaidia watu wa kisiwani Pemba kupata faraja zaidi ya kuingiza na kutoa mizigo kwa sababu bandari itakuwa inahudumia hivyo. Lakini hakuna kilichozungumzwa na wala hakuna lilizungumzwa kama bandari ya Wete, Wesha na Mkokotoni hii inasikitisha.

Mhe. Spika, zamani ilifika kuelezwa kuwa bandari ya Mkokotoni itajengwa iwe ya kudumu na hivi sasa inatumika vizuri tu na tunajua kuwa Pemba ilio ndogo ina bandari 3, lakini Unguja iliyo kuwa ina bandari 1 tu na hakuna asiyejua kwamba kwa kuimarisha bandari wa Mkokotoni ni kuimarisha uchumi wa nchi hii, ni kuwasaidia wananchi walioko Kaskazini katika safari zao Mhe. Waziri hakuitaja. Kwa hivyo, ningeomba kujua kwa nini wakati haya ndio mambo tuliotaraji tuyapate kwa maendeleo ya nchi hii hayakuingizwa tukabakia katika sehemu ile ile labda kubwa lililozungumzwa ni kujenga jengo la abiria kwa mfadhili wetu Sheikh Bahressa Mwenyezi Mungu azidi kumpa uwezo atusaidie na kwengine.

Jengine kwa sababu ya wakati Mhe. Spika, naomba kuzungumza kidogo tu kuhusu mradi wa ujenzi wa barabara. Nitaanza na barabara tatu zilioko Kaskazini Pemba ikiwa ni barabara ya Konde/Wete, Gando/Wete na barabara Wete/Chake-Chake. Kitabu kimeleeza kuwa ujenzi umesita kwa sababu serikakali inadaiwa na hivi sasa imeshapata asilimia 66 ya fedha inayodaiwa na mkandarasi na imeshaombwa serikali kuimalizia deni lililobakia na kazi ya ujenzi ianze.

Mimi najua serikali inasema hivyo lakini kwa macho yangu hasa na ninavyoona kwanza hizi barabara hazikupata kampuni nzuri ya ujenzi. Mimi *MECCO* sina imani nao na ujenzi wa barabara zile kwa sababu hazijaanza leo, zimeanza miaka miwili mitatu iliyopita na ndio kwanza ziko katika hatua ya kifusi na mengineyo.

Mhe. Spika, nataka nijue kwa sababu uwezo wao ni ndogo na kwa sababu serikali wanajua kuwa wana matatizo. Hiyo kweli barabara hizi zimefeli kwa sababu serikali imeshindwa kuwalipa au kwa sababu na hii kampuni nayo yenyewe hasa. Halafu barabara hii ya Wete/Chake-Chake ambazo zote zinafadhiliwa na *BADEA* pamoja na *SAUD FUND,* nayo nasikia inataka kupewa kampuni hii ya *MECCO*.

Ushauri wangu kwako mimi nimeona kampuni ya *H.YOUNG* iliyotengeneza barabara 5 zilioko Kaskazini Pemba imeanzaa juzi tu na kampuni inafanya kazi usiku na mchana na kazi yao ni nzuri. Kwa nini serikali haibadili msimamo ikatafuta kampuni nyengine kwa maslahi ya nchi yetu na utengenezaji bora wa barabara zetu au wanipe sababu za msingi kutokana na huku tunakotoka mpaka tunakofika, kwa nini *MECCO* waendelee na barabara hii.

Jengine Mhe. Spika, ninavyofahamu mimi mfuko wa barabara ni mfuko wetu sote. Lakini humu kama kitabu nimekitizama vizuri nimeona barabara 23 zitakazojengwa zenye urefu wa kilomita 285.762 na zote hizi barabara za Unguja hakuna hata moja ya Pemba. Naomba maelezo na kama sikupata maelezo ya kutosha pengine kuna sababu maalum za kufanya hivyo, nitakuwa mkaidi kabisa kabisa wa kupitisha bajeti ya kitabu hiki.

Mhe. Spika, ningemba nikumbushe kuwa Mhe. Waziri anapojibu masuala hapa anayapeleka sisi tunachukua kuwa ile ni majibu ya wizara, ndio majibu ya serikali. Mhe. Waziri aliniahidi kuwa barabara zangu zote zile za vijijini zile ambazo zinaungana na barabara kuu inayojengwa na zinatumia pesa nyingi sana zitakuwemo kwenye bajeti hii na zitatengenezwa. Nasikitika sana hata ile barabara inayotoka Uondwe ambayo alikuwa anaizungumza mara kwa mara inamkereketa anataka kuitengeneza haimo. Nasema hii hakuifanyia haki na mpaka anipe maelezo kwa barabara zote nilizozitaja sizitaji tena hapa kwa sababu ya wakati ni mdogo.

Mhe. Spika, katika shughuli za kamati nakumbuka siku moja tulijadili barabara ya Mkapa hii inayopitia Daraja Bovu na niliona katika pesa zilizotolewa kwa haya matengenezo yanayoendelea kulikuwa na shilingi milioni mia moja na ishirini na tatu laki tano na sitini na saba kitu kama hivyo ambazo zimetumika kwa vifaa, nyengine ni kwa matengenzo.

kini kuangalia hali ya barabara ilivyo kwa hivi sasa na sehemu nyengine sijui kitaalamu zitakuwa vipi na fedha iliyotumika ni nyingi sana. Mimi ningeliomba Mhe. Spika, ile barabara iundiwe kamati maalum tukafanye uchunguzi kwa maslahi ya pesa za wananchi, pesa za wananchi, pesa za wafadhili ili tujue kama kweli pesa hizi zilitumika ipasavyo na hizo milioni

nilizozitaja ambazo niliuliza maana ni 1, 2, 3, 4, 5, 6 na 0 huko sijui zimepangwa vipi. Na kwa sababu ya wakati naingia kwenye viwanja vya ndege naiona juhudi ya wizara kuhusu jengo jipya la abiria lakini nilitaka kujua aliyesababisha mpaka jengo lile likasitisha kukatafutwa mshauri muelekezi, ni gharama gani iliyopatikana hivi sasa na ni kiasi gani cha zaidi ya fedha serikali imeagiza au imeomba kwa kupitia hii kampuni ya *Exim Bank* ya China ili kuweza kumaliza jengo lile la abiria.

Mwisho kabisa kwa sababu ya wakati Mhe. Spika, kiwanja cha ndege cha Pemba kila siku kinazungumzwa kutengeneza. Safari ile tuliambiwa kuna mfuko wa Afrika Mashariki utahusika katika kukijenga kile kiwanja upya safari hii hakikutajwa hasa. Mimi namuuliza Mhe. Waziri hajui kuwa hivi sasa huduma ya viwanja imeongezeka, viongozi wanapokwenda kule wanakwenda na ndege kubwa siku nyengine lazima iwe ni usiku sijui kutokana na kazi ilivyo, kwa nini anatupangia mfumo wa maisha kwa kiwanja kile ambacho kama kingetengenezwa kikawa kinafanyakazi kama cha Unguja ni kwa maslahi ya wananchi wote.

Mhe. Spika, nashukuru kwa kupata nafasi hii *inshallah* Mwenyezi Mungu atujaalie Mhe. Waziri anijibu ambavyo ndivyo ili tuweze kuipitisha bajeti yake. Ahsante.

Mhe. Salmin Awadhi Salmin: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii na mimi nikaweza kuchangia mawili matatu juu ya hotuba hii ya Makadirio na Mapato na Matumizi ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano.

Mhe. Spika, kwanza niungane na wenzangu waliotangulia juu ya hoja mbali mbali walizozitoa nakubaliana nazo yaani hoja za msingi na kwa kweli zinahitaji majibu tena ya kina. Mhe. Waziri kwa kweli aje atueleze zile hoja ambazo zimetolewa vyenginevyo basi niungane na wenzangu wote juu ya hoja hii iliopo mbele yetu.

Mhe. Spika, mimi nataka maelezo juu ya maeneo mawili makubwa na nakusudia kutumia kifungu cha 68 (6)(b). Nitaeleza sababu ya kutumia kifungu hicho sitaki nikinukuu Mhe. Spika, unakielewa ili nijiridhishe na majibu ambayo Mhe. Waziri atayatoa. Kwanza Mhe. Spika, nataka Mhe. Waziri atakapokuja kufanya majumuisho anieleze sababu zilizopelekea Shirika la Meli la Uwakala kushindwa kuwarejesha kazini wafanyakazi 6 waliokuwa wa Shirika la Meli waliotuhumiwa kufanya upotevu wa vitabu vya tiketi wa Shirika la Meli licha ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuwaamuru kuwarejesha kazini watuhumiwa hawa 6 na 3 miongoni mwao kuendelea na mashitaka, aje anipe maelezo.

Wafanyakazi hawa waliotuhumiwa walikuwa 9 na Mwanasheria Mkuu akaamuru kwamba wafanyakazi 6 warejeshwe kazini na 3 waendelee na kesi lakini shirika lilishindwa kuwarejesha kazini mbali ya ushauri uliotolewa na Ofisi ya *DPP* wakati ule kwamba wafuate maagizo ya Mwanasheria walishindwa. Jambo ambalo Mhe. Spika, lilishababisha Mahakama Kuu ya Zanzibar kutoa hukumu ya kuwarejesha kazini wafanyakazi wale na kulipwa fidia ya kila mmoja wao shilingi milioni 45 kwa kushindwa kurejeshwa kazini na shirika.

Lakini hata Mahakama ya Rufaa ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilikubaliana na hukumu iliyotolewa na Mahakama Kuu ya kuwarejesha kazini na kuwalipa fidia ya shilingi milioni 45 kila mmoja jambo ambalo litasababisha kuliingizia hasara Shirika la Meli na Uwakala kwa zaidi ya shilingi milioni mia mbili na sabini juu ya hukumu iliyotolewa.

Mhe. Spika, watu hao niwataje ili Mhe. Waziri awaelewe wafanyakazi wenyewe ni:-
Moh'd Hassan Juma
Moh'd Najim Hamad
Khamis Hamad Khamis
Othman Abdalla
Mkubwa Haji
Abdalla Omar Mjawiri

Mhe. Spika, inasikitisha kuona kwamba viongozi wanaosimamia vyombo hivi mashirika na mamlaka hujifanya kama vyombo hivi ni mali yao inasikitisha. Na kwa sababu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mahakama ni vyombo ambavyo vipo kwa mujibu wa sheria na mara zote sisi tunazungumzia juu ya utawala bora, utawala wa sheria na Katiba. Sasa kama Mahakama, Mwanasheria Mkuu wanatoa maelekezo, viongozi wa shirika wanashindwa kutekeleza agizo lile, sasa watamsikiliza nani. Kama Mwanasheria wa Serikali hasikilizwi na taasisi zake watamsikiliza nani. Kwa kweli, Mhe. Spika, nataka Mhe. Waziri aje anipe maelezo ni kwa nini watu hawa walishindwa kurejeshwa kazini hatimae kulisababishia hasara kubwa shirika milioni mia mbili na sabini na aje anieleze pesa hizi zitalipwa na nani. Hilo moja.

La pili nahitaji maelezo juu ya maendeleo ya ujenzi wa uwanja wa ndege, kwa lugha ya kuzungu tunaita *new terminal*, jengo la abiria jipya. Kwa kweli hapa tunataka maelezo ya kina kwa sababu tumekuwa tukipata maelezo mengi tokea Baraza lililopita hadi Baraza hili na hakuna kinachoendelea. Maelezo ya mwanzo ni kwamba tulikopa fedha kutoka Benki ya *EXIM* ya

China milioni 50 kwa ajili ya ujenzi ule lakini sasa maendeleo yake mpaka kufikia leo hayaeleweki imekuwa hadithi.

Sasa namtaka Mhe. Waziri aje atupe maelezo kutoka hatua ya kwanza ya mkopo na mikataba hadi sasa hivi suala hili limefikia wapi. Ni kiwango gani cha fedha kinahitajika sasa hivi na serikali itaingia hasara ya kiasi gani, kwa sababu Mhe. Spika, huu ni mkopo. Mhe. Ismail Jussa Ladhu mara nyingi huwa anasema kwamba mkopo dhana yake unatakiwa ulipwe na zitakazolipwa ni fedha za wananchi. Kwa kweli Mhe. Spika, inasikitisha sana kwamba jambo hili imekuwa kila mwaka ni hadithi. Mwaka jana Mhe. Waziri alituambia kwamba halan jengo lile litaanza kujengwa lakini bado imekuwa ni hadithi hatujui linaishia wapi, linakwendaje. Kwa hivyo, kama walivyotangulia wenzangu kusema kwamba haina haja ya kuwaidhinishia fedha za walipa kodi hawa na huku hatujui kitu gani kinachoendelea, haiwezekani kwamba tunakaa hapa watu wazima tunaambizana maneno lakini hakuna linaloendelea, hakuna haja. Mimi nimesema mwanzo nakubaliana na wenzangu wote kwamba hakuna haja ya kuidhinisha fedha kwa ajili ya watu ambao hawataki kufanyakazi. Tunahitaji maelezo Mhe. Waziri.

Baada ya kueleza maeneo ambayo nitahitaji maelezo, sasa nije kwenye bajeti kwa jumla. Mhe. Spika, nije kwenye Idara ya Utunzaji wa Barabara. Kwanza niipongeze serikali kwa kujitahidi katika kutandika miundombinu ya barabara kwenye maeneo mbali mbali. Barabara ni maendeleo, bila ya kuwa na barabara basi maendeleo yanakuwa hakuna na ni ushahidi Mhe. Spika, kwamba pale ambapo barabara itapita basi na wananchi wanasogea karibu ya barabara zile. Kwa hivyo barabara ni maendeleo lakini pamoja na juhudi wanazochukua wenzetu wa Idara ya Barabara, bado wanakabiliwa na changamoto ya vifaa, idara hii haina vifaa vya kutosha. Kwa kweli serikali inahitaji kuliangalia sana eneo hili na kuwatafutia vifaa ili waweze kutekeleza kazi zao hizi za ujenzi wa barabara, kila wakati tutakuwa tukiwalaumu, kwa kweli vifaa vyao ni vibovu na vimechakaa.

Mhe. Spika, Idara ya *UUB* ni idara muhimu sana, tusipoiwezesha tukaipa vifaa vya kutosha basi kila wakati tutakuwa tunalaumu. Mimi nimuombe sana Mhe. Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo pamoja na kwamba hayupo lakini awatengee fedha ili waweze kutafuta vifaa na magari ya kisasa kwa ajili ya kutengeneza barabara zetu na hususan barabara za ndani. Wakati mwengine Mhe. Spika, Wawakilishi wako tunakuwa na vijisenti vya miradi kwa ajili ya kutengeneza njia zetu za ndani, lakini Idara ya *UUB* wanashindwa kuzitekeleza shughuli zile kwa sababu ya upungufu wa vifaa au ubovu wa vifaa, ikiwemo magari na vitu vyengine. Kwa hivyo eneo hili Mhe. Spika, ni muhimu sana.

Mhe. Spika, kuhusu Idara ya Usafiri na Leseni. Mhe. Waziri hapa ametueleza kwamba Idara ya Usafiri na Leseni inafanyakazi zake vizuri lakini pia alitueleza kwamba inakabiliwa na changamoto kadhaa, ikiwemo uchakavu wa jengo la idara, ukosefu wa mtambo wa kisasa wa kutolea nyaraka za huduma ya usafiri na kukosekana kwa jengo lenye vifaa vya upasishaji wa magari.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri hajatueleza ni jinsi gani atakabiliana na changamoto hizi kwa sababu Karakana wanayoitumia watu wa Idara ya Usafiri na Leseni, kwa kweli jengo lile halifai kuishi binadamu, huwezi ukakaa katika jengo lile kwa muda wa saa moja, ni lazima utoke nje ukatafute hewa. Mna joto kali na wanafanyakazi katika mazingira magumu pamoja na kwamba wamefunga ma-*AC* yenyewe yanatoa joto. Kwa kweli jengo lile halifai kufanywa kama ni ofisi muhimu ya upasishaji wa magari.

Suala hili Mhe. Spika, tumelizungumza sio leo wapo pale kwa muda mkubwa sana. Serikali iliwahi kutueleza kwamba wapo pale kwa muda lakini imeonekana sasa ni maeneo yao na limeshakuwa eneo la kudumu. Kwa hivyo, Mhe. Waziri hebu uje utueleze una mpango gani wa kuwatafutia jengo jengine mbadala ambalo litalingana na mazingira halisi ya shughuli yao wanayoifanya na kuwawezesha kufanya shughuli zao kwa ufanisi katika siku za baadae. Uje utueleze Mhe. Waziri kwa sababu jengo lile kama umeshatembelea halifai kabisa, huwezi kufanyakazi katika mazingira kama yale. Mhe. Spika, Mhe. Waziri nahitaji maelezo juu ya jambo hili atueleze amejipangaje ili kuona kwamba idara ile mule ilimo Karakana wanahamishwa na wanatafutiwa eneo jengine mbadala ili waweze kufanya shughuli zao kwa ufanisi.

Mwisho Mhe. Spika, ni kuhusu viwanja vya ndege. Mamlaka ya Viwanja vya Ndege hapa wametueleza mambo mengi. Malengo ya mwaka 2013/2014, wameeleza ujenzi wa ukumbi *business arrival lodge*, ujenzi wa kituo cha biashara na mambo mengine kadhaa. Lakini mimi ninalotaka kujiuliza Mhe. Spika, fedha hizi zinazotumika kwa ajili ya jengo lile, hivi ndio tumeshakata tamaa na ujenzi huu wa *new building* kwa jengo la abiria. Kwa sababu kuna fedha nyingi karibu bilioni 7 zimetengwa kwa ajili ya kufanya mambo haya ambayo pengine kama jengo lile jipya ambalo tunakusudia kulifanya lingeweza kukamilika, basi mambo haya tusingeweza kutumia kiasi hiki cha fedha kwa ajili ya kutengeneza jengo hili la zamani. Kwa hivyo Mhe. Spika, mambo haya ambayo yamekusudiwa kufanywa na wenzangu hawa, mimi naona kama kweli tuna nia ya kujenga *terminal* mpya, basi hayafai sasa hivi kushughulikiwa, labda kama tumeshakata tamaa basi tunaweza tukaweka pesa kwa ajili ya kutengeneza. Lakini inaonekana tumeshakata tamaa na ujenzi wa jengo jipya lile la abiria.

Mhe. Spika, hii *business arrival lodge* mimi nahitaji maelezo Mhe. Waziri, hii ni kwa ajili ya kitu gani kwa sababu kikawaida wageni wanapofika pale wao ni kuondoka, lakini nadhani kitu cha muhimu zaidi kujengwa ni sehemu ya *departure*, kuliko hii sehemu ya kufikia, wageni wakifika pale wanaondoka.

Mhe. Waziri hapa anatuambia anaandaa mradi huu kwa lengo la kuongeza huduma za abiria katika ukumbi wa kuondokea abiria wa daraja la kwanza, yaani *business lodge* na kuanzisha ukumbi mpya wa abiria wa kuwasili *business arrival lodge* ili kujenga mazingira mazuri kwa abiria wanaotumia uwanja wetu. Mimi nahitaji kidogo maelezo juu ya eneo hili ambalo wamekusudia kulitengeneza.

Mhe. Spika, kwa kweli kiwanja cha ndege au mamlaka ya viwanja vya ndege imekuwa ikilalamikiwa sana. Wananchi wengi wamekuwa wakilalamikia mamlaka ya viwanja vya ndege.

Mhe. Spika: Muda wako unakaribia sana kumaliza.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Namalizia Mhe. Spika. Kumekuwa na malalamiko namna ya uendeshaji wa viwanja vya ndege. Sasa nadhani kunahitaji marekebisho ya kweli kweli katika eneo lile. Haiwezekana mahala panapotolewa huduma za wananchi ikawa kila wakati watu wanalalamika, inaonekana hawaridhishwi na uongozi wa mamlaka ya viwanja vya ndege. Kuna malalamiko mengi, inaonekana kama vile ni mamlaka ya mtu binafsi. Hili ni jambo la hatari Mhe. Spika, kama tunafika pahala eneo kama lile ambalo linatoa huduma za watu lakini wafanyakazi wanalalamika, abiria wanaokwenda pale wanalalamika na kila mtu analalamika, hii ni hatari.

Mhe. Waziri unatakiwa uwe makini sana kwa sababu tunavyofahamu sisi mamlaka ile sio mamlaka ya mtu binafsi, ni mamlaka kwa ajili ya wananchi. Kwa hivyo hebu tupe maelezo namna ya uendeshaji wa mamlaka hii mpaka inafika pahala kila mmoja analalamika juu ya uendeshaji, inakuwaje kila mtu analalamika katika utoaji wa huduma pale. Wenye ndege wanalalamika, wenye makampuni ya meli na ndege wanalalamika.

Mhe. Spika, niiombe Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ifanye *follow up* juu ya mamlaka ile. Ningethubutu kusema tuunde kamati teule lakini naona tutakuwa na kamati nyingi, panahitaji uchunguzi wa kina, mamlaka ile inahitaji kuchunguzwa, hata wafanyakazi wa mamlaka wamekuwa wakilalamika, wengine wanalipwa mishahara hii na wengine wenye shughuli moja wanalipwa mishahara hii. Kwa maana hiyo, hii inaonekana kama ni taasisi ya mtu au kama ni kampuni ya mtu, anapoamua kwamba huyu nimlipe

kiasi fulani basi anamlipa, akiamua huyu alipwe kiasi fulani ina maana hakuna hata utaratibu wa kulipana mishahara.

Mhe. Spika, wenzangu walitangulia kusema hapa, kwa hivyo hii ni hatari, hatuwezi kuendesha taasisi kwa utaratibu huu. Mhe. Spika, tunahitaji maelezo ya Mhe. Waziri kwa nini taasisi hii inaendeshwa kwa utaratibu ambao haukubaliki, jamii haikubali uongozi uliopo pale.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe muda wako umekwisha nakushukuru sana.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Baada ya maelezo hayo Mhe. Spika, nashukuru kwa kunipa muda wako kama nilivyotangulia kusema kwamba naungana na wenzangu wote waliotangulia kusema kwamba hakuna haja ya kuidhinisha fedha kwa wizara hii ambayo utekelezaji wake unaonekana dhahiri umefeli kwa ajili ya wananchi. Pia nahitaji maelezo juu ya hoja mbili za msingi za mwanzo ambazo nimezieleza. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, kutokana na muda leo sitokushukuru, isipokuwa niende moja kwa moja.

Mhe. Spika, kabla sijaingia kwenye hoja iliopo mbele yetu, ningeomba hiki kitabu tulichopewa na Mhe. Waziri cha Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano, maelezo ya bajeti inayotumia mfumo wa program *base budget* kwa mwaka wa fedha 2013/2014.

Mhe. Spika, hiki kitabu kina tatizo, kina mapungufu ya kisiasa na kina mapungufu ya kiufundi. Kuna *political problem* na kina *technical error*, kwa sababu ukiangalia hapa hii ni bajeti ya serikali, tena serikali yenyewe ni Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, sio serikali tu hivi hivi ndogo ndogo. Bajeti ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuweka *Ethiopian Airline*, ni tatizo. Hata wangeweka jahazi kama ndege hatuna Mhe. Spika, hapa badala ya kutuwekea meli ya mfanyabiashara basi wangetuwekea meli ya Maendeleo japo imeshakomaa lakini wangeiweka hapa.

Mhe. Spika, kama angekuwa hai Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Marehemu Mzee Abeid Aman Karume basi nadhani waziri huyu kama angekuwa yuko katika serikali yake angemfukuza kazi, kwa sababu wangekuwa wanaudumisha ukoloni mambo leo, ni *Ucolonialism* jambo ambalo ni tatizo sana katika nchi ya mapinduzi kama hii.

Baada ya dibaji hiyo Mhe. Spika, sasa niende katika hoja. Kama itakuwa sio kukiuka Kanuni basi wajumbe watakapoondoka hii karatasi wangeitoa na wakabakia na hii tu. Mhe. Spika, nianze na suala zima la usafiri wa nchi kavu

lakini kabla sijaanza suala la usafiri wa nchi kavu, naomba sana niungane na mwenzangu kuipongeza ile kamati ya watu sita ya maridhiano ambayo imetufanya sisi wengine kuwemo humu. Nichukue nafasi hii kuwapongeza, sitowataja majina lakini nimtaje Mwenyekiti wao Mhe. Ali Mzee Ali kwa kuweza kuiongoza ile kamati mpaka tukafika hapa.

Mhe. Spika, nadhani kama sio ile *GNU* basi inaonekana kwamba nisingekikalia hiki kiti hapa, Mwenyezi Mungu mkubwa. Lakini katika hili nashukuru sana na nampongeza sana ndugu yangu pale Mhe. Waziri ananitizama, nakupongeza vile vile katika hili, tunashukuru sana.

Mhe. Spika, kuhusu usafiri wa nchi kavu ili uweze kuunganisha watu baina ya kijiji na kijiji, baina ya mji na mji, baina ya nchi na nchi kwa zile nchi ambazo sio za kisiwa basi ni lazima uwe na mtandao mzuri wa barabara.

Mhe. Spika, barabara ni muundombinu ambao unawaunganisha watu wa nchi moja na nchi nyengine. Sasa kwa sababu sisi ni visiwa napenda sana niipongeze serikali ya Awamu ya Sita iliyokuwa inaongezwa na Dk. Aman Abeid Aman Karume kwa kuweza kujitahidi sana katika kutuwekea miundombinu ya barabara. Kwa kweli Awamu ya Sita wamefanya jambo kubwa ukilinganisha na awamu nyingi zilizopita huko nyuma. Ninapenda kuchukua fursa hii kuwapongeza sana. Barabara hata Vitongoji imefika, mgongo wa ngisi inateleza mwanangu mpaka Vitongoji. Kwa hivyo, nadhani nitakuwa mchache wa shukrani kama sikuitumia fursa hii kuwapongeza Serikali ya Awamu ya Sita kwa kuweza kufanya kazi nzuri sana. Kwa hivyo, kwa niaba yangu na kwa niaba ya wapiga kura wa Jimbo la Wawi, nachukua fursa hii kuwapongeza sana Serikali ya Awamu ya Sita kwa kuweza kujenga barabara.

Mhe. Spika, mimi sio Chama cha Mapinduzi kabisa sijawahi kuingia katika Chama cha Mapinduzi, nilikuwa Afro Shirazi ambaye sikuwahi kuwa kwenye Chama cha Mapinduzi, sijawahi na nadhani sitawahi. Mhe. Spika, lakini Waingereza wanasemaje, 'Usiache kumsifu ukiona anafanya vizuri'. Serikali ya Awamu ya Sita mmefanya vizuri ahsanteni sana.

Mhe. Spika, sasa kazi iliopo mbele yetu ni katika kuzienzi na kuzitunza barabara hizi pamoja na kujenga mule ambamo Awamu ya Sita hawakumalizia kujenga. Sasa katika hili Mhe. Spika, naomba nimwambie Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano pamoja na jitihada yote hiyo iliyofanywa na awamu ya sita, lakini kuna maeneo katika jimbo langu hawakuweza kumalizia kujenga barabara hizo. Sasa naomba Mhe. Spika, nizitaje baadhi ya hizo barabara katika jimbo langu ambapo awamu ya sita hawakuwahi kuzigusa katika kupeleka maendeleo ya barabara.

Mhe. Spika, kuna hii barabara ya inayotoka Uwandani Kwareni kwenye machimbo ya mawe, kupitia Dodeani kuja zake Vikunguni mpaka *Scanning Mass,* hapa mjengo wa banda. Hii barabara Mhe. Spika, ni muhimu sana kwa sababu kuanzia kule Kwareni wanachukua matofali ambapo matofali yale yameshafika Unguja yanajengewa, ni matofali mazuri sana Mhe. Ismail Jussa anayejua hayo matofali ni mazuri sana na yanajengeka vizuri. Watu wanayataka kule Mkoani, wanayataka hapa Unguja na Nungwi yameshaanza kujengewa matofali yale. Lakini Mhe. Spika, barabara ya kutoka huko yanakochimbwa mpaka kufika barabara ya bandari ya Mkoani ili yakapata kufika kwa ndugu zangu wa Nungwi ni tatizo. Sasa naomba awamu ya saba na nyinyi muone umuhimu wa hiyo barabara.

Mhe. Spika, barabara nyengine ambayo wenzenu hawakuwahi ni barabara ya kutoka Vikunguni pale kupitia Skuli ya Ng'ambwa, kuja zake Gombani ya Kati mpaka uwanja wa mpira Gombani, ule uwanja mnaouona mkenda kucheza *football* na hatimaye kuunganisha katika barabara kuu, vile vile barabara hii haipitiki na ni muhimu sana Mhe. Spika.

Mhe. Spika, katika barabara hii nikuambie kuna ndizi sana watu wa Vikunguni, wanazalisha viazi vitamu sana watu wa Vikunguni, wanazalisha muhogo mtamu sana, watu wa Vikunguni ambao hivi sasa ndio unaofutariwa hapa Unguja. Lakini kuutoa muhogo kutoka Vikunguni ukaupitisha Ng'ambwa ukaja nao mpaka barabara kuu, kuja nao Mkoani bandarini ni tatizo na kwa bahati mbaya Dk. Aman Abeid Aman Karume, ile barabara hakuwahi kuifikiria muda wake umemalizika. Sasa naomba Dk. Shein na wewe kwa kupitia hii serikali yako ya *GNU* muione ile barabara ili watu wanufaike.

Mhe. Spika, sasa niende katika barabara ya Kili Koani Kibokoni kwa kupitia Madungu, uje zako moja kwa moja mpaka barabara kuu katika Skuli ya Vitongoji pale. Mhe. Spika, kama mnataka mule samaki watamu basi muwapate kutoka Kili Koani. Lakini wanavuliwa samaki wanaozeana kule hawapati kusafirishwa kuja kwenye soko. Mimi nadhani mheshimiwa katika hili kuna haja ya kuwa makini sana kwa kuiona hii barabara ya Kili Koani mpaka kufikia Skuli ya Vitongoji pale. Ingawa Mhe. Raza na yeye nitamuona amesema tumuone katika mambo haya ya kusaidiana saidiana, nitamuona Mhe. Raza. Lakini ng'ombe akivunjika mguu malishoni basi hujikokotea zizini Mhe. Spika, kusaidiwa na zizi letu Mhe. Spika, ni *GNU* inayoongozwa na Dk. Ali Mohamed Shein pamoja na wadogo zangu hawa waliopo mbele. Kwa hivyo, nawaomba sana muzione barabara hizi kusudi tuweze kuleta maendeleo katika nchi yetu.

Mhe. Spika, katika suala zima la ujenzi wa barabara na gharama zake. Kuna tatizo kidogo, sisi tunajua hakuna maendeleo ambayo hayana gharama lakini mambo mengine enhe! Wapemba wanasema hivyo. Wapemba tunasema hivyo, usemi huo upo.

Mhe. Spika, barabara zinazojengwa katika visiwa vyetu kabla ya ujenzi wa barabara katika mwahala mwengine, kwanza inabidi nyumba na mazao yapishe ujenzi wa barabara. Sisi hili hatuoni tabu lakini Mhe. Spika, inasikitisha sana kwamba wanaofanya tathmini katika Wizara hii ya Miundombinu na Mawasiliano, kwa kweli wanawadhulumu sana wananchi wetu.

Mhe. Spika, juzi nilitembelea barabara moja mitaa ya Unguja nikiikosea kuitaja jina lake halisi samahani siijui sana. Kuna barabara inatoka sijui Mwera hapa Pongwe, barabara hii haijajengwa ndio inataka kujengwa sasa. Lakini wamefanya tathmini katika barabara hii ni barabara ya Mwera Pongwe au Koani Pongwe, ukitoka Mwera tu pale mbele kuna barabara inataka kujengwa kuelekea Pongwe huko. Miti imeshaanza kukatwa, majumba yameshaanza kupigwa alama ya X, Lakini inasikitisha sana Mhe. Spika, kwamba tathmini iliyofanywa hawakushirikishwa wenye mali na matokeo yake ni dhulma tupu iliopo.

Mhe. Spika, mimi nilikwenda kuiona nyumba ya bwana mmoja wala simjui, ni jamaa yangu wa Kijaninge kapata kiwanja pale, kwao ni Donge kule kwa sababu na mimi Wajaninge ni ndugu zangu, nilikwenda kumtembelea. Nilipofika Mhe. Spika, ananiambia baba si unaona hapa wanataka kunilipa shilingi 600,000. Nyumba ya tofali, japo ni kijumba ambacho hakijamalizika vizuri lakini kiwanja tu kwa shilingi 600,000 Mwera hupati, kiwanja kinaanzia shilingi milioni 5, leo unataka kumlipa mtu shilingi 600,000 mheshimiwa. Hili ni tatizo, naomba barabara ile zoezi lisitishwe na katika hili ikiwa Mhe. Waziri hajaniambia nikafahamu, siwezi kuwaacha wananchi wetu walipa kodi wa nchi hii wa Pongwe na sehemu za Mwera wakidhalilishwa hatuwezi. Nitazuwia kifungu mpaka nipate maelezo ya kutosha, kwamba azuwie kufanya makisio yale na waende wakarudie ili waweze kupata maslahi hawa wananchi walipa kodi wa nchi hii tena maskini, sio halali kabisa.

Mhe. Spika, ninayo majina zaidi ya 25 ambao nyumba ya shilingi milioni karibu 10 anaandikiwa unalipwa shilingi milioni moja. Nilipokwenda pahala kichekesho nilichokiona, kuna kijiwanja tu kidogo hana nyumba ni kiwanja tu,

Mhe. Spika: Mhe. Saleh Nassor Juma, hebu kidogo kidogo.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa maelekezo yako. Mhe. Spika, nimekwenda katika kiwanja kitupu tu hakina nyumba, kinaingia kama nyumba moja wala sio kubwa, basi yule mwenye kiwanja kaandikiwa atalipwa shilingi milioni 15, kiwanja tu hata nyumba hakina. Haya jamani yule ana kibanda chake japo hajakimaliza vizuri mnataka kumpa shilingi 600,000, halafu huyu kiwanja tu shilingi milioni 15. Hii ni dhulma na hili ni tatizo.

Mhe. Spika, mimi nadhani nizuie kifungu hapa kusudi nipate maelekezo ya kina kwamba ni lini watarudia hilo zoezi. Tatizo jengine ni kwamba waziri kila nikitaka suala la fidia ya tuliokatiwa minazi yetu na miembe yetu basi ananiambia pesa zimeshakuwa tayari usiwe na wasi wasi, wala usiwadai watu wa umeme tudai sisi. Umeme uliotoka Darajani kupitia Vitongoji, Umangani kupitia Vitongoji hadi Kwareni Makaani umegharimu mali za watu wengi na siridhiki kwa lile jibu lako la juzi tu, kwamba usiwaambie watu wa umeme. Nataka uje uniambie ni lini, kinyume na hivyo hapa ni tatizo.

Mhe. Spika, nadhani kwa sababu ya muda niende haraka kuna mambo mengine nitakuja kuyaacha.

Mhe. Spika: Kwa dakika tano.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ehee! Allahu Akbar. Mhe. Spika, usafiri wa baharini.

Nilikuwa nazungumza kwamba ili ufanye vizuri katika usafiri wa nchi kavu basi uwe na *network* ya barabara. Lakini ili ufanye vizuri katika usafiri wa baharini mheshimiwa ni lazima uwe na ma-*jetz* ya kutosha, mabandari mazuri ya kutosha na meli za kutosha kabisa kwa nchi za visiwa kama sisi. Bila ya kuwa na bandari na meli za kutosha basi Mhe. Spika, watu wa visiwa utakuwa huwafanyi haki sana katika kufanya shughuli zao.

Kwanza Mhe. Spika, napenda nimpongeze mfanyabiashara Said Salim Bakharezsa. Huyu ni mfanyabiashara mzalendo nampongeza sana kwa kuweza kutuwekea miundombinu ya safari. Ukenda Dar es Salaam utafikiti uko Ulaya, ukikaa pale *VIP* na ukija hapa Unguja ni tofauti. Kwa kweli ninampongeza pamoja na Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Bandari kwa kutoa mashirikiano na yule mfanyabiashara na kuweza kutufanyia mambo kama haya. *(Makofi).*

Mhe. Spika, mchezo kwao hutunzwa.Yule Said Salum Bakharessa pamoja na mambo yote aliyotufanyia anaomba sehemu ndogo pale kwa ajili ya kujenga ofisi, mpaka leo serikali ina kisisi wakati mtu ametufanyia mambo makubwa

kama yale. Kwa hivyo, ni vyema apewe ili aweze kujenga ofisi na pale kuna ghala tu na anaweza akaihamisha na ajenge ofisi na halafu ile ghala atajenga jengo la kisasa pale nyuma, hivi jamani hilo dogo. Mhe. Spika, hilo dogo hebu serikali isikie katika hili. Vile vile kuhusu suala la kusajili meli munatakiwa musiwe *bias* katika usajili wa meli hizi. Kwa mfano, mimi nimepata malalamiko ya kampuni moja hapa wanaita *Seven Seas Marine Service Limited*, hawa wanayo meli yao inaitwa *Burak III* na meli yao inachukua abiria na mizigo. *(Makofi)*

Sasa jambo la kusikitisha Mhe. Spika, hoja hiyo ilikuja hapa kwenye swali la ikaletwa Sheria Nam. 17(a)(iii) na Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano alijibu katika swali hili la kutafsiri ile sheria na ninayo *hansard* hapa, na alisema kwamba Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano.

Mhe. Spika, hapa kuna majibu mawili na jibu la kwanza ni kwamba sheria inawataka wamiliki wa vyombo walete zile *certificates* zao, kwa hivyo ndani ya *certificates* hizo itaonesha kwamba imetengenezwa kwa ajili ya abiria au laa.

Jibu la pili alisema kwamba hali hiyo ilio ile meli inaweza ikawafanya wakaguzi wakaifelisha kuchukua abiria hata kama hapo mwanzo ilikuwa ikichukua abiria. Kwa maana hiyo, inategemea sana mmiliki mwenyewe aende kwenye mamlaka akaombe ukaguzi. Kwa hivyo, hawa walikwenda na walipokwenda pamoja na kufuata maelekezo yote lakini jambo la kusikitisha Mhe. Spika pamoja na Mkurugenzi kukubali kwamba meli hii *specifications* zake ni nzuri, lakini hadi leo hii bado hawajapewa *go ahead* kwa hii meli ya Burak III, ambayo haina tofauti hata kidogo na ile ya meli ya *Azam Sea Link*, yaani sawa na ile ni kwamba inachukua abiria na mizigo.

Sasa kwa nini wawe *bias* wakati kuna hitajika usafiri huu wa Wete – Tanga na wakiikagua na kuona kwamba hakuna tatizo na inaonekana haina tatizo. Kwa nini wasiiruhusu kuchukua abiria angalau baina ya Wete na Tanga pale na tukaweza kuwanufaisha hawa vijana wetu ambao wanafanya biashara Mhe. Spika, nadhani katika hilo wasiwe-*bias*. *(Makofi)*

Aidha Said Salum Bakharessa mfanyabiashara anataka aweke kitu kama alichokiweka hapa Unguja na kule Pemba au kama alivyokiweka Dar-es-Salaam ama aruhusiwe Wete au Wesha. Kwa kweli inasikitisha kwamba wizara hivi sasa ni kimya haimjibu wakati na yeye anataka kwenda, kwa nini hatuwaachi Wapemba na wao wakanufaika na hii huduma kama tunavyonufaika sisi hapa Unguja ama kule Dar-es-Salaam. Mhe. Spika, tunapomruhusu kuweka geti zake pale basi usafiri utapatikana. *(Makofi)*

Baada ya hayo, Mhe. Spika nimalizie kwenye Mfuko wa Barabara.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, nadhani muda umekwisha. Sasa utoe neno la kwamba unafunga hotuba yako.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, ahsante na siwezi kuunga mkono hoja hii mpaka nitakapoambiwa kwamba kwa nini *Burak III* hawajasajiliwa, kwa nini zile sehemu za Wawi kule barabara zangu hazijajengwa ndio nitaweza kupitisha.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, nakushukuru. Sasa naomba nimkaribishe Mhe. Hamza Hassan Juma na baadaye Mhe. Asaa Othman Hamad.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, na mimi kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kwamtipura kwanza tunaomba tumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetujaalia uhai na uzima kuja kutekeleza majukumu tuliotumwa na wananchi.

Pili nikushukuru wewe Mhe. Spika, kwa kuweza kunipa nafasi hii na mimi nikaweza kuzungumza machache sana katika bajeti hii ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, kwanza napenda kutamka moja kwa moja kwamba hotuba hii ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano siungi mkono. Mhe. Spika, ninazo sababu nyingi na nitaanza moja moja. Kwanza kutotendewa haki wananchi wa Jimbo langu la Kwamtipura. Mhe. Spika, nimezungumza miaka mingi hivi sasa tokea serikali hii awamu ya saba imeingia madarakani lakini hata Serikali ya Awamu ya Sita ilipokuwepo madarakani.

Kwa kweli jambo hili si geni kwamba barabara ya Shaurimoyo Kwa-Abasi Hussein mpaka Darajabovu. Mhe. Spika, barabara hii imetajwa mpaka kwenye Ilani ya Uchaguzi ya CCM na mimi ni Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa ya CCM. Sasa kudharauliwa Ilani ya Chama cha Mapinduzi sikubali hata siku moja. *(Makofi).*

Mhe. Spika, nadhani Mhe. Waziri alipokabidhiwa wizara alikabidhiwa Ilani ya Uchaguzi ya CCM. Kwa hivyo, sina haja ya kusema sana katika eneo hili na kwamba barabara hii anaijua na nilisema sana tena niliwahi kujibiwa na mtu mmoja na akasema aah! Kwani labda hizi barabara kila mtu anavyotaka lazima akajengewe yeye na wala sikutaka mimi, isipokuwa Ilani ya Uchaguzi ya CCM. *(Makofi).*

Mhe. Spika, hata Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Awamu ya Sita aliagiza siku ambayo tulikuwa tunazindua Skuli ya Chekechea ya Kwamtipura kwamba barabara ile ijengwe tena katika kiwango cha lami, ili kupunguza *traffic* njia hii ya Mikunguni kuendelea mpaka Amani. Lakini kutokana na dhararu ya watendaji kutokuwasikiliza viongozi wa nchi basi barabara hii mpaka leo imedharauliwa. *(Makofi).*

Hata hivyo, Rais wa Awamu ya Saba kabla ya kuingia madarakani mimi mwenyewe binafsi na wala sikwenda kuomba cheo, isipokuwa nilikwenda kuomba maendeleo katika Jimbo langu la Kwamtipura. Mhe. Spika, nilizungumza suala la kumalizwa hospitali yangu. Namshukuru sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwamba Hospitali ya Kwamtipura hivi sasa imemaliza. Kwa hivyo Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri wa Afya kwamba hospitali ile angalau ifanye kazi mpaka saa 3:00 za usiku, kwa sababu watu wetu mnawafukuza wasije Hospitali ya Mnazi Mmoja na kuwaambia rudini huko huko. Sasa leo Hospitali ya Mnazi Mmoja watu wanafukuzwa lakini Hospitali ya Kwamtipura wanaotaka waende ikifika saa 8:30 daktari hayupo, basi waruhusuni watu wetu Hospitali ya Mnazi Mmoja ndivyo mnavyotaka. *(Makofi).*

Mhe. Spika, nimekaa na uongozi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja na uwezekano.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, rudi kwenye hoja hii ambayo iko mezani sasa.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, sawa. Ahadi ya Rais nilikuwa nikishajihisha ahadi ya Mhe. Rais.

Kwa kweli nashukuru sana Mhe. Spika, sasa Rais wa Awamu ya Saba tukamuomba na barabara yetu ile ya Shaurimoyo tena tumemwambia kwamba tunakula hasara sana kwamba kila mwaka baada ya Masika tunatia kifusi. Hata hivi karibuni Mhe. Spika, kupitia mfuko wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tumetumia karibu shilingi milioni 5,000,000/= kwa ajili ya kutia kifusi na hivi sasa hakipo Mhe. Spika. Kwa kweli kifusi hicho tena tumeomba tu eneo dogo angalau la kilomita mbili au tatu, basi tutiliwe lami kwa sababu kuna mporomoko mkubwa wa maji na huko kwengine watakuja kumaliza baadae mpaka leo dhararu kubwa wanatuonesha Jimbo la Kwamtipura. Kwa hivyo, mimi kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kwamtipura sitoikubali bajeti hii. Mhe. Spika, kwa bahati nzuri kwa ile jeuri yao mwaka wa ngapi ninataja na haki ya Mungu hata kwenye kitabu haikutajwa si dhararu kitu gani na siungi mkono bajeti hii. *(Makofi).*

Nikiendelea na mchango wangu sasa naomba nizungumzie barabara ya Amani/Mtoni. Mhe. Spika, tunashukuru kwamba juzi tulipata semina ya Mfuko wa Barabara, sasa tunawataka basi Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano waimalize barabara ya Amani/Mtoni.

Mhe. Spika, katika barabara hii ya Amani/Mtoni kuna gharama ya fidia iliyopangwa tokea mwaka ilipotaka kujenga barabara ile na leo Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kwa sababu zao mbali mbali barabara ile wameshindwa kuimaliza kwa wakati. Kwa hivyo hata thamani ya nyumba na viwanja imeongezeka. Kutokana na hali hiyo, tunawataka wananchi wale ambao wanataka kuwalipa hivi sasa basi wawalipe fedha zao kwa mujibu wa soko, kwa sababu haya wameyataka wao wenyewe, gharama hii kama ingelikuwa pale mwanzo ilipofanyiwa tathmini ilikuwa *valid* lakini kwa hivi sasa imeshapitwa na wakati.

Mhe. Spika, tunataka tathmini ifanywe upya na wananchi wetu waweze kulipwa haki zao lakini barabara tunataka ijengwe kwa sababu Wizara ya Fedha kupitia Mfuko wa Barabara wamesema fedha wanazo tena Mhe. Spika, fedha kila mwaka hivi sasa wanasema mwaka uliopita fedha zimerudi, kwa sababu Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano wao wenyewe hivyo vifaa hawana. Sasa hapa ninaomba Mhe. Spika, tuangalie utaratibu wa kutoa *tender* hasa kwa hizi barabara zetu ndogo ndogo za *feeder road*.

Sasa naomba nizungumzie kuhusu Mamlaka ya Viwanja vya Ndege. Mhe. Spika, kwa mujibu wa kifungu cha 98(b), (c), (e) kinashereheshwa na (f) cha Kanuni ninaondoa shilingi mia moja ya mshahara wa Mhe. Waziri mpaka afanye maamuzi magumu na nina sababu kama nilivyoeleza na wala Kanuni sitoinukuu, naomba Makatibu Mezani wanainukuu na watakwambia nini nimekusudia. *(Makofi).*

Mhe. Spika, katika Mamlaka ya Uwanja wa Ndege kwanza ninalo jambo moja ambalo nitaliunganisha na hoja zangu nyengine. Kwa kweli kuna usumbufu anaoupata mwekezaji ambaye mwekezaji huyu nilizungumza katika Wizara ya Ardhi na unaniambia sio pahala pake na nikakwambia uje unipe ruhusa hapo pahala pake nipazungumze. Sasa leo hapa ndio pahala pake. *(Makofi).*

Mhe. Spika, kuna mwekezaji huyu ambaye ameekeza katika mradi wa kufundisha marubani ambapo nilizungumza kwamba tayari ameshafundisha marubani 50 hivi sasa na kwenye marubani 50, basi 33 hawa ni marubani wa Kizanzibari, wako Wafaransa, Wataliana, Waingereza na hata ndugu zetu Watanzania Bara watatu wamefundishwa hapa. Kwa hivyo, kwanza hii ni kampuni ambayo inayoitangaza Zanzibar, pia inatoa ajira pamoja na kwamba

ni sehemu inayotoa taaluma, yaani ni chuo na wenzetu hawa mpaka leo wanawazungusha huku na kule. Mimi nina wasi wasi na wala wasi wasi sio maradhi ukeshakuwa na uhakika nao, kwa hiyo mimi wasi wasi wangu uhakika wake ninao. Mhe. Spika, kwa sababu mwekezaji huyu amekodi *hangar* kwa bodi wa Uwanja wa Ndege. *(Makofi)*

Kwa kweli suala hili nimelisema kwa sababu tulifanyia utafiti kwenye kamati na tukalileta katika ripoti ya Kamati Teule na serikali ikatuahidi hapa kwamba huyu bosi munayemsema tumesikia kama serikali na tunaipongeza sana serikali yetu ni sikivu imesikiliza ripoti ya Kamati Teule. Vile vile serikali ikatuambia basi tutamuuliza na tutampa *option* aidha aendelee kuwa bosi wa Mamlaka au aendelee kuwa Mkurugenzi wa Kampuni wa *AERO TECH*.

Mhe. Spika, ninao mkataba wake hapa na wala sitaki kumtaja jina Mhe. Spika, naomba kunukuu kidogo.

> "*P. O. Box* hiyo hapo *with transfer in consideration of the natural love and affection to be Mr. Moyo Lazaro* doo! Huyu nimeshamtaja Mhe. Spika samahani.
>
> Mhe. Spika, *transfer Zanzibar to here by transfer and sign to him my 54 ordinary share in undertaking code AERO TECH Zanzibar Limited, liability Company in co-operating and so on".*

Kwa hivyo, hapa bosi huyu aliidanganya serikali kwamba tayari ameshatoa *share* zake kwa kumpa bwana huyu, ulimi umeteleza nimemtaja. Sasa barua hii au mkataba huu umefungwa tarehe 24/10/2012.

Sasa nakuja na nyengine na hii inatoka *AERO TECH Zanzibar*, inasema '*rent for the year 2013* na hii ni *rent* ya hilo *hangar* ninalolizungumza, Mhe. Spika naomba kunukuu kidogo.

> "*Kindly refer to your letter of 17th April, 2013 concerning above subject.*

Mhe. Spika, tuangalie tarehe na hii barua ya mwanzo inasema 24th October, 2012 na hapa ndipo alipo-*surrender share* zake. Sasa barua hii inasema *letter* of 17th April, 2013, kwa hivyo hii ni mpya kabisa.

> "*As per conservation with our team and captain Said some point highlighted in your letter have been noted and changed in agreement below. (Makofi)*

Mhe. Spika, huku ameidanganya serikali kwamba ameshatoa *share* na hapa barua hii ya kampuni yake inasema vipi "*As per conservation with our team and captain Said some point highlighted in your letter have been noted and changed in agreement below*. *(Makofi)*

Mhe. Spika, hii inasema nini the *the date of contact as from agreed* hii hapa na inaendelea. Sasa huu ni mkataba wa kuongeza bei kwa hilo *hangar*, vile vile kubadilisha mkataba kutoka miezi sita kwa mwaka mmoja. Kwa hivyo, bado ana-*negotiate* katika kukodisha na huyu ameliachia? Kutokana na hali hii Mhe. Spika, hapa Mhe. Waziri kama hawezi kufanya maamuzi magumu, basi hapa ninatumia kifungu cha 98 cha Kanuni na ninaondoa hapa shilingi mia moja katika mshahara wa Mhe. Waziri. Sasa kama atakwenda ofisini au hendi na ofisi nyengine ipo Baraza la Wawakilishi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, sikubali na kudanganywa na juzi Mhe. Mwanasheria Mkuu nilipozungumza hoja zangu katika Wizara ya Ardhi alizungumza kwamba huyu tumemwita na tukazungumza naye, na alizungumza hapa na *hansard* ipo na tayari amesema kwamba ameshaiacha na leo barua hii hapa ana-*negotiate*, yaani bado wanaendele ku-*negotiate* ndani ya Julai hii. *(Makofi).*

Suala jengine kwenye mamlaka hii na Mhe. Salmin Awadh Salmin alizungumza kwamba hii mamlaka inaendeshwa kama ni mamlaka ya mtu. Mhe. Spika, mimi niliwahi kutoa jina katika bajeti iliyopita na nikasema lile jina la *Abeid Amani Karume International Airport* lifutwe kwa vitendo vya aibu vinavyofanyika pale uwanja wa ndege na nilipendekeza jina limo kwenye *hansard* na wala sitaki kulirejea, yaani iitwe *So and So International Airport*, kwa sababu hapa ninayo *pay rolle* ya wafanyakazi wa Mamlaka ni aibu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, hapa kuna watu wa bustani analipwa shilingi 500,000/= wakati pale Manispaa *Engineer* Mkuu tu, yaani ndiye Fundi Mkuu wa Baraza la Manispaa analipwa shilingi 120,000/=. Sasa nitamshawishi yule aje aombe kazi ya kukata majani *airport*. *(Makofi)*

Nikiendelea hapa hapa na hii nitaisema haraka haraka, lakini nitaomba kamati baadae iifanyie kazi. Vile vile kuna mama mmoja yeye huko *VIP* na wala sitaki kuwataja watu majina kwa sababu hizi *documents* zote zipo zitaonekana na yeye huyu mshahara wake analipwa shilingi 706,000/= na bosi wake analipwa shilingi 600,000/=. Sasa nani bosi hapo. *(Makofi)*

Pia hakuna utaratibu katika malipo. Kwa mfano, kuna hawa *secretaries* Mhe. Spika, kuna wengine wanalipwa shilingi 500,000/= wengine shilingi 300,000/=. Kwa kweli ukiangalia elimu zao sawa na wengine wanaolipwa

kiwango cha chini wako *senior* kuliko wale wapya, Mhe. Spika hapa kuna nini? *(Makofi)*

Mhe. Spika, hapa lazima tuwe wakweli kwa sababu hapa kuna mtu yeye anacho cheti cha *FTC*.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, unazo dakika tatu kwa ajili ya kumaliza hotuba yako.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, sasa hii watakwenda kuimaliza wao. Sasa nakuja ili nisije nikakosa kumalizia.

Kwa hivyo jengine Mhe. Spika, nataka yule mwekezaji, yaani yule mama aliyetaka kujenga uwanja wa ndege, yaani *airstrip*, nataka nipewe maelezo kwa nini mpaka leo amezuiliwa na huyu bosi wa mamlaka, alimwambia kwamba serikali inataka kujenga kiwanja cha ndege chengine kule Nungwi ingawa hichi cha hapa kinawashinda. Sasa hebu atuambie nini kinachoendelea na hapo nitapiga buti vile vile.

Mhe. Spika, kuhusu ujenzi wa *terminal II* nataka maelezo kwamba je na wenzangu wameshazungumza na mimi nitataka maelezo, lakini utamaliza lini, gharama au hasara kiasi gani tunayoipata.

Jengine Mhe. Spika, nitazuia kwenye fungu la mapato la mamlaka kwa sababu tunatoleshwa shilingi 500/= pale mlangoni na sisi wageni tunaokwenda pale, lakini hata wafanyakazi. Mhe. Spika, mfanyakazi akiingia analipa shilingi 500/= akitoka akiingia tena shilingi 500/=, kwa kweli huu sio utendaji mzuri. Kwa hivyo, nadhani kama hawa *staff* wangelipishwa ile ada ya mwaka na wakapewa *sticker* zao pale kama bandarini na mtu analipishwa *sticker* anaingia. Lakini leo *airport* mfanyakazi imekuwa hicho anachokipata kwa kila mwezi kinarudi pale pale. Mhe. Spika, na mimi nina wasi wasi ule mradi wa kukusanya zile *ticket* pale shilingi 500/= sijui kama si wa mtu fulani.

Mhe. Spika, kwa hivyo hapa nataka nizungumze kwamba *scheme* ya Mamlaka ya Uwanja wa Ndege inatakiwa iangaliwe na ifanyiwe kazi. Vile vile kwenye ripoti ya Kamati Teule na tulikaa na uongozi wa mamlaka, na tukakubaliana kwamba wale vijana waliokuwa wakibeba mizigo wauziwe *share* katika ile kampuni aliyokuwa inabeba mizigo. Kwa kweli Mhe. Spika, tulikubaliana vizuri lakini mpaka leo halikutekelezwa. Naomba maelezo.

Vile vile *ZMA* nataka maelezo kwenye ile hoja yangu niliyoijenga kipindi cha nyuma na nikaambiwa nisubiri katika wizara hii kwa ajira za zile meli

ambazo zilizosajilia nje ya nchi. Sambamba na hilo mapato yanayopatikana na nitakuja kuzuia kwenye eneo la mapato. *(Makofi)*

Mhe. Spika, naomba maelezo kuhusu barabara zinazoshughulikiwa na *MECCO* kule Pemba zitamalizwa lini na kama kuna ingia hasara basi ni kiasi gani na serikali itawajibika vipi kwa kuingia hasara ambayo kila siku isiyokwisha.

Mhe. Spika, napenda sana kuwasifu pia hawa wawekezaji wakubwa hasa katika sekta ya usafirishaji. Hata hivyo, ninaomba na hawa wadogo tusiwadharau tuwape haki zao. Mhe. Spika, inaonesha hapa kuna wawekezaji binafsi wazalendo waliowekeza katika eneo la usafiri wanazuiwa kwa sababu fulani na wala sitaki kusema kwa sababu gani, isipokuwa hapa nina mashaka. Kwa mfano, hoja walizozizungumza wenzangu kwamba kuna meli hapa tokea zilivyosajiliwa na tumepitisha kwenye sheria kwamba kama meli haijabadilishwa matumizi yake tokea kule ilikotoka basi iruhusiwe kufanya kazi. Mhe. Spika, imezuiliwa mpaka leo, yaani meli zinazuiliwa na huyu mwengine anafanyakazi. Hali hii ni sawa sawa kumpiganisha Tyson ngumi na yeye kama umemuacha na mikono yake na Hamza ukamfunga mikono. Mhe. Spika, hii sio haki na nitakuja kuzuia vifungu hivyo. *(Makofi).*

Baada ya hayo machache Mhe. Spika, napenda tena nikushukuru kwa kunipa nafasi hii. Lakini la mwisho kabisa Mhe. Spika namuomba Mhe. Waziri aje aniambie kwamba hapa tulipiga kelele sana kuhusu Kampuni ya *ZAT* kupewa kampuni nyengine na tukaambiwa hivi sasa uwanja wa ndege wa Zanzibar unaweza kuchukua abiria zaidi ya 500 kwa mwaka.

Mhe. Spika, kulikuwa na Kampuni ya *SWISSPORT* tuliipigia kelele sana na serikali tunaishukuru ikatusikiliza na kazi ile ikaiambia mamlaka iifanyie kazi upya. Kwa kweli kazi ile imefanywa na bodi imeshakaa na imeshachagua kampuni, lakini kwa taarifa tulizonazo Mhe. Waziri amekataa, hivyo atuambie ni sababu gani aliyoikataa.

Mhe. Spika, tuna wasi wasi inaonesha hapa kuna vitu ambavyo havina jawabu moja kwa moja, kuna *interest* ina maana ile bodi kwa hivyo bodi ninajua mwenyekiti ameteuliwa na Mhe. Waziri na wale waliomo mule ni wataalamu na watu wamefuatilia kampuni mpaka Afrika ya Kusini, yaani imekidhi vigezo vyote. Sasa kuna sababu gani Mhe. Waziri akaizuia mpaka hivi sasa bodi isitangaze. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwa hayo niliyoyazungumza kifungu cha 98 cha Kanuni nitaendelea kukishikilia katika maeneo yote hayo niliyoyataja.

Baada ya hayo, machache Mhe. Spika kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kwamtipura walionileta hapa, siungi mkono hotuba hii na Mhe. Waziri inaonesha labda hii kazi sitaki kusema kama imemshinda lakini inaonesha kama haiwezi. Mhe. Spika, ahsante sana. *(Makofi).*

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, ahsante sana, sasa ni zamu yake Mhe. Asaa Othman Hamad na baadaye Mhe. Mgeni Hassan Juma.

Mhe. Asaa Othman Hamad: Mhe. Spika, nikushukuru baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi hii na mimi kujumuika na Waheshimiwa wa Baraza lako tukufu kuweza kuchangia machache, lakini lenye umuhimu kwenye hotuba ya Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano.

Mhe. Spika, Zanzibar kwa jiografia na historia yake kwenye maeneo matatu kwetu sisi ni muhimu mkubwa sana ni bandari, anga na barabara za nchi kavu.

Mhe. Spika, nitaanza na barabara pamoja na matatizo ya kiuchumi tulionayo, lakini serikali ina juhudi zake kwenda mbio huku na kule, mikopo na misaada na mengineyo tuweze kujenga anagalu wananchi wetu waweze kufaidika usafiri wa ndani kusafirisha na hayo.

Lakini tumefika mahali wizara hii kwa bahati mbaya sana, Mhe. Spika karibu ni miaka 30 isiyopungua tunaimba barabara Wete/Chake-Chake, Wete/Konde, Wete/Gando na leo naona tena barabara tatu nimezitizama zinasomwa hivyo hivyo na pia nimeona tena na Wete/Chake-Chake.

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri hii nyengine Wete/Chake-Chake ni Chake-Chake ipi na Wete ipi, mbona hatufahamu. Sasa hizi tatu ambazo tuliambiwa na wenzetu hawa wa *BADEA* au *Saudi Fund* na *Zanzibar Government* ndio wanagharamia chini ya Kampuni ya *MECCO*. Kwa hivyo, hapa namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, wakati atakapokuja kufanya majumuisho atuambie kwamba ni lini barabara hizi zimekusudiwa na wizara ya zikamilike. Kwa kweli Mhe. Spika, harufu ya mbali inayonukia kwenye hili na barabara hizi kila siku zinatiwa fusi, lakini haziwekwi lami ni mradi maalum wa ulaji ni *man made claims* ndizo zinazofanyika baina ya wizara fedha kucheleweshe kulipwa *MECCO* na *MECCO* wafike mahala fulani serikali kucheleweshwa kwao watu wakipata ulaji.

Mhe. Spika, katika suala la barabara kwa ufupi kwa mujibu wa muda. Barabara za *MECCO* Pemba, barabara ya Fumba Unguja tunakiomba kiti

chako tunataka kamati ya Baraza lako kufuatilia kwa ajili ya kuchunguza kulikoni huku mpaka barabara hizi hadi leo zimefikia hapa zilipofika. *(Makofi)*

Jengine ni kuhusu Kampuni ya *H. YOUNG* nitazungumzia barabara ya Mtapwe. Mhe. Spika, kuna sifa kwamba kuna *speed* kubwa ya ujenzi lakini kubwa ubadhirifu mkubwa wa ujenzi vile vile katika barabara hii. Mhe. Spika, kawaida mtumishi wa mahala popote suala la *overtime* ni hiari, lakini hawa wanalazimishwa, yaani ni lazima waingie *overtime*, lakini mahesabu ya masaa sio wanayolipwa.

Vile vile wenzetu wale ambao wameshapata uzoefu wa muda mfupi wanayoyaona si sahihi katika suala zima la ujenzi. Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri atoe kauli hapa ni lini tutaweza kwenda barabara hizi zote tano kuzipitia na kuzungumza na watendaji wa daraja hili la chini wenyewe kusikiliza matatizo yao bila ya kuwepo mabosi wao na Mhe. Waziri atoke na kauli katika hili na mimi nikiwa miongoni mwa timu hiyo.

Nikiendelea na mchango wangu sasa naomba nizungumzie kuhusu bandari. Mhe. Spika, tulipitisha sheria na juzi tukafanya *amendment* ya sheria kuhusu Usafiri wa Baharini. Mhe. Spika, Baraza hili lazima liheshimiwe kwa sababu ni Baraza linalowawakilisha wananchi wa nchi hii, pia Baraza hili ndilo linalotunga sheria, Baraza hili ndilo linaloridhia mikataba ya kimataifa na hivi kutokea mtu tu au kikundi cha watu kwa dharua au kiburi tu, sisi kwa nini tumvumilie? *(Makofi)*

Mhe. Spika, usajili wa meli tumepitisha sheria zaidi ya miaka 15 na hiyo meli isiweze kuchukua abiria na leo inatolewa amri meli ina umri wa miaka 33 imesajiliwa, ilihali mwanzo imeshakataliwa. Mhe. Spika, tunataka Mhe. Waziri akuambie MV. Wete imesajiliwa kwa amri ya nani?

Jengine Mhe. Spika, huu utaratibu wa kusajili vitu vibovu na halafu tukiua watu na baadae tukapiga kelele tupewe msaada tunaita nini kwamba tumeshapata maafa na wazungu wanatuletea mpaka juzi wametuambia wenzetu hapo juu. Kwa hivyo, hatuoni haya na halafu sisi wenyewe tunafanya ubadhirifu wa kiasi chote hichi.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri katika maeneo haya na mengine ambayo nimeyagusa gusa ya bandarini na shutma mbaya inayoendelea ya namna ya *tickets* zinavyouzwa kipumbavu pumbavu samahani Mhe. Spika, na kuachwa abiria meli inakwenda na nyengine ndio inakuja kumalizia, ameshindwa Mhe. Waziri kudhibiti katika eneo hili.

Mhe. Spika, nataka nije *Karume Air Port.* Muda wangu nataka nimalizie hapo. Mhe. Waziri hebu atwambie Baraza hili lifahamu mamlaka ya Uwanja wa Ndege ni mamlaka yake nani? Ni mamlaka ya baba yake nani? Kama mamlaka ni ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, maana yake Wazanzibari ndio wenyewe. Inakuwaje Wazanzibari wanaofanya kazi uwanja huu wanaokwenda kutafuta rizki kiwanja hichi wanyanyaswe, wadhalilishwe, wasumbuliwe bila ya sababu ya msingi tunayofahamu kwa sababu kama ni sheria, sheria huwa zinapitishwa hapa. Kwa nini hatuelezwi kwamba hawa wanapata tabu kwa sababu wamekosa hili na lile kwenye sheria.

Mhe. Spika kuna ndugu zetu Wazanzibari wana kampuni zao za *tours*, wana kampuni zao za kupakia mizigo na abiria hao. Lakini kampuni hizi ama mashirika haya, utaratibu si lazima wote wamiliki kitu kimoja. Shirika la meli linaweza likaendesha kazi ya biashara ya meli bila ya kumiliki meli. Shirika la ndege ndiyo hivyo hivyo, Shirila la Magari linatizama mahesabu ya faida na gharama.

Mhe. Spika, kuna hawa *tours* wana wenzao wanaowaita pale *airport*, wanapovimbiwa na abiria wale wanzao ndio wanaowachukua abiria wao. Kuna huyo anayemiliki huko ndani na huku nje pia ni kwake yeye. Magari ya hawa wanakuja kusubiri wageni, hataki uwanja ule yaingie, cha ajabu wanalipa *gate pass* halafu wanakaa kwenye *park*, kwenye *park* wanakwenda kutiliwa mnyororo. Mnyororo kutolewa ni lazima ulipe shilingi 50,000 (hamsini elfu). Hebu Mhe. Spika, atwambie Waziri pesa hizi yeye anakwenda nazo wapi. Si hilo tu yale mabao tunayokalia kwa kusubiri wageni wetu wao hawatakiwi wakae wanafukuzwa. Mhe. Waziri hii ya wapi. Ndio nikauliza mwanzo swali uwanja huu wa nani?

Jengine, wanawatobolea mpaka mipira ya magari yao kwa sababu wageni wanaokuja waweze kuchukuliwa na magari ya huyo bibi mkubwa au bwana mkubwa. Mhe. Waziri tunataka atujibu hilo. Kwa nini amemuweka mtu au watu kudhalilisha wengine kiasi chote hicho.

Mhe. Spika, jengine ni *Terminal II.* Uwanja huu umejengwa kwa gharama na mkopo wa wenzetu wa *Exim Bank* ndugu zetu Wachina. Nina maswali nataka Mhe. Waziri anisikilize kwa makini sana na anijibu akiwa na hakika na anachokijibu. Nina kila *documents* ya kila mikutano yao ya washauri wao na hawa wanaowashirikisha, sasa kutoka ofisi za ubalozi ambazo Kampuni ya ujenzi inatoka.

- *Terminal II* atwambie Mhe. Waziri kwa nini ilikwama?
- Kukwama kwake hakukuwa na ushauri wa kitaalamu?
- Kama ulikuwepo nani kavunja ushauri huo kutokuufuata?

- *Faulty* hiyo imetokea kwa nani?
- Mkataba wa Ujenzi wa *Terminal II* ni mkataba wa aina ipi?

Mhe. Spika, nitashindwa kupitia kila kitu kufuatana na muda lakini haya ninayoyafanya ni kwamba yote yamo mikononi mwa wajumbe wako. Haya tumefanikiwa baada ya kazi nzuri ya *UNDP* na kupikwa kwetu na kuiva kwetu, tumeweza kuyajua haya. Sasa tunataka kuisimamia vizuri sana serikali hii fedha ya walipa kodi itumike pale inapostahiki, na pale ilipotumika sivyo aliyefanya sivyo na yeye afanyiwe sivyo. Tutaanza mfano huo kwa kuanza kwa wizara hii. (*Makofi*).

- Mhe. Spika, *Terminal II* mshauri wa kwanza kuambiwa alishauri vipi na ushauri wake utakuwa na hasara ipi kama ujenzi utabaki pale ulipo?
- Kama kuna faida ni faida ipi kama jengo litabaki pale?
- Mshauri wa pili ambaye Mhe. Waziri alimtaja hapa siku moja ni Mfaransa huyu, kagharamiwa na nani na kwa nini?
- Je, yeye mshauri wa pili kashauri kitu gani?
- Kina maslahi gani kwa Serikali ya Zanzibar?
- Kama tusipofuata tuna hasara ipi?

Mhe. Spika, kuna ushauri wa hati hati tunausikia jengo liondoke lilipo liende mita 60, kuna faida likipelekwa mita 60 *West* na kuna hasara kama litabaki pale, *operation cost* kwa sasa na kadri inavyoendelea. Nataka Mhe. Waziri athibitishe haya ninayoyasema ni kweli au akanushe. (*Makofi*).

Mhe. Spika, pesa ambazo zimebakia sasa *Exim Bank* mkopo huo tulionao na pesa ambazo juzi ndugu zetu au wenzetu wamekwanda kuziomba tena China, 47 zimetajwa ndani kitabu hichi, zinatosha kabisa kujengwa *Terminal II* mpya na sio ile *Terminal* ambayo itatupa mahitaji tunayoyahitaji. Heshima ya uwanja ule na jila la Mzee wetu Abeid Amani Karume litakuwa ni kweli. Ataonekana amefanya nini tarehe 12 lakini pia kwa Wazanzibari suala zima la uchumi ni hizi ndege tunazohitaji na wageni wetu kufunga. Katika hali iliyopo Mhe. Spika, haitokuwa hayo ninayoyasema badala yake ni hasara kubwa tutakayoipata.

Mhe. Spika, nizungumzie kifungu cha kanuni 98 nitakizuia miye kwa wizara hii. Niwambie Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kutokana na vurugu la ufujaji mkubwa wa fedha ya wananchi hawa wa Zanzibar. Kwanza Mhe. Spika, nimeomba la kwanza kwenye barabara, Kamati yako na naomba tena Kamati yako kwenye suala la *airport* lakini Wizara hili kwanza twende tukapumzike na siku kuu.

Mhe. Spika, tujadili wizara zilizobaki wala usikamate kichwa tutakuja kufanyia kazi bila ya lolote kwa hili. Nakwambia tutaifanya kazi bila ya kukudai lakini tunataka kuwathibitishia Wazanzibari kwamba tunawatafutia haki yao inayopotezwa bure. Mhe. Spika, nataka nimalizie na *Zantel*.

Mhe. Spika, *Zantel* Zanzibar ina ubia kama nchi. *Zantel* kwenye bodi tuna wajumbe wetu Wazanzibari. Tulipiga kelele kwamba hawa watu wanahama sasa kuelekea Bara, watu hawataki kusikia. Wakaanza kuwafukuza wafanyakazi Wazanzibari na wanakataa kuwapa mikataba. Mhe. Spika, kwa taarifa yako kesho tarehe 1 Agosti ilikuwa *Zantel* wanaanza kuhamia Bara na kuilipa Bara badala ya Zanzibar. Waheshimiwa na Mawaziri wanisute katika hili, nina hakika Mhe. Waziri anazo taarifa kama nilivyokuwa nazo mimi hapa.

Mhe. Spika, kulikuwa na mpango wa kuwafukuza wafanyakazi 178 Wazanzibar. Kuna mtu Ofisi Kuu pale Dar-es-Salaam ana asili ya nchi moja kutoka Asia, hataki kumsikia hata kwa jina Mzanzibari.

- Hivi Mhe. Spika, ile sisi kutoa ardhi, kutoa jina kwa *Zantel* malipo leo ni haya?
- Mhe. Waziri alikuwa hana taarifa hizi mpaka lifikie hilo?
- Wenzetu waliokuwepo kwenye Bodi walikuwa hawatoi taarifa kwa serikali hapa mpaka likafika nyanyaso la kiasi hichi?

Mhe. Spika, sisi ni Wazanzibari, Wajumbe wako ni wawakilishi wa Wazanzibari, majimbo 50 yamo ndani ya jengo hili, hatukubali kudhalilishiwa Mzanzibari wetu hata kama yumo ndani ya tumbo, kwa hilo hatuna muhali nalo.

Mhe. Spika, hatutoipitisha wizara hii kwanza, hata kama tutapata maneno ya majibu ya sasa hivi na kesho. Tuna mengi ambayo hatujaweza kuyawasilisha mbele ya Baraza hili ndio tukaomba twende tukale siku kuu tutakuja kufanya kazi hii. Kwa sasa kifungu cha 98 ndicho tunachokitumia kuzuia suala lote la mshahara wa Mhe. Waziri hadi pale angalau aje ajieleze mwenyewe udhaifu wa Wizara hii. Mheshimiwa nakushukuru.

Mhe. Mgeni Hassan Juma: Ahsante sana kunipa nafasi hii kuchangia Wizara hii ya Miundombinu na Mawasiliano. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehma. Pia nikushukuru na wewe Mhe. Spika, kwa kunipa fursa hii kumpongeza Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote kwa kutuwasilishia bajeti hii ambayo leo hii tumepata nafasi nzuri ya kuweza kuchangia.

Mhe. Spika, mimi nitasema machache kwa sababu wenzangu waliotangulia wamesema mengi. Nataka kuchukua fursa hii Mhe. Spika, kuwaunga mkono wenzangu wote ambao waliotangulia kwa yale ambayo wamechangia. Nasema hivyo kwa sababu ni yale ambayo mengi nilikuwa nayo kuyachangia lakini wenzangu wameshatangulia kuyachangia. Kwa hivyo nasema naunga mkono hoja ambazo zimewasilishwa na *back benchers*.

Mhe. Spika, kwanza kabla ya kuanza lolote nataka kuzungumzia suala la barabara ya Kisima Majongoo mpaka *Wireless.* Wazungu wanasema *charity beginning at home* na mimi ni kwetu pale. Barabara ile Mhe. Waziri unaifahamu vizuri sana, ile barabara pale Kisima Majongoo mpaka Wireeless ilikuwa ni barabara ambayo ni nzuri sana na watu wengi wanaitumia kwa kwenda upande wa pili wa ng'ambo kupitia pale, wakiacha ile ya Skuli ya Haile Selassie.

Unaifahamu vizuri sana barabara ile kwa sababu na wewe ni mdau wa mtaa ule na unasali Msikiti ule wa *Wireles*. Mhe. Waziri barabara ile tumeipa jina inaitwa Nungwi kwa sababu ya hali iliyokuwepo pale. Barabara ile ipo katika hali mbaya sana. Hivi karibuni Mhe. Rais alikuja kufungua *SACCOS* ya Kikwajuni alituahidi na mimi naamini ahadi yoyote ambayo anatoa Mhe. Rais, basi inatakiwa itekelezwe. Aliahidi kwamba barabara ile itajengwa. Sasa nakuomba Mhe. Waziri naona humu kwenye bajeti yako sijaiona kabisa, kama imo imeandikwa kwa lugha nyengine lakini hii lugha ambayo naifahamu mimi na jina la mtaa ule haimo.

Mhe. Waziri na mimi naongezea hapo hapo, bajeti hii sijawahi kupiga buti lakini nitapiga buti kwenye bajeti yako Mhe. Waziri. Nataka uniahidi barabara yangu kutoka Kisima Majongoo mpaka *Wireless* lini itatengenezwa na utunihakikishie kwamba barabara ile utaitengeneza ili watu wanaoishi katika eneo lile na wao wafaidike na mapinduzi ya nchi hii. Mhe. Waziri baada ya kusema hayo nataka kuzungumzia suala zima la barabara. Mimi nashukuru sana kama walivyopita wenzangu vile vile na nampongeza sana Rais wa Awamu ya Sita Dkt. Aman Abeid Karume kwa kuliona suala zima la umuhimu wa miundombinu katika nchi yetu.

Mhe. Spika, serikali inatupa fedha nyingi sana kwa ajili kutengeneza hii miundombinu. Tunajua serikali inatumia nguvu kubwa ya kuhakikisha kwamba miundombinu inakaa vizuri. Tatizo ni kwamba miundombinu hii baada ya kujengwa lakini kiwango kinaonesha dhahiri ni kidogo mno kiasi ambacho barabara hizi zinaharibika mara moja.

Lakini la pili tunawaachia wananchi wazitumie vibaya barabara hizi. Nasema hivyo kwa sababu kuna barabara natoa mfano Mombasa. Watu pale

wanatumia sasa hivi kwenye barabara imekuwa ni gereji wanamwaga mafuta ya *dizel* pale, hata wale wananchi wambao wamejengewa ile barabara kuweza kuitumia vizuri wanashindwa kuitumia vizuri pamoja na hayo pia barabara inaharibika. Mhe. Waziri, wizara yako iko wapi kwenye hili.

Vile vile kuna barabara ya Mikunguni na tumesikia hawa wamepewa *notes* lakini *notes* haifai kitu. Mhe. Waziri chukua hatua, nenda na magari yako katoe vitu pale uiwache barabara iwe wazi, uwezo unao Mhe. Waziri, umepewa uwezo huo fanya kazi hiyo na sisi tutakuunga mkono. Lakini haiwezekani leo barabara zinajengwa, serikali inatoa fedha chungu nzima lakini wanaachiwa watu waharibu barabara zile na ni kwa manufaa ya kila mwananchi wa nchi hii. Mhe. Waziri nakuomba sana uchukua hatua kwa hilo.

Mhe. Spika, vile vile nimeliona suala zima la baadhi ya barabara zinazojengwa kwa kutumia mfuko wa barabara. Nina hofu kubwa huu mfuko kweli una fedha za kutosha. Naweza kukwambia kwamba katika bajeti ya mwaka jana kuna baadhi ya barabara ambazo zimesemwa zitajengwa na mfuko wa barabara, mfano barabara ya Hale/Kiongele ambayo inaishia Mkwajuni. Humu kwenye kitabu cha mwaka jana imo lakini kwenye kitabu cha mwaka huu haijaguswa na hiyo barabara haijajengwa kabisa.

Mhe. Spika, kwa nini Mhe. Waziri hujatupa sababu, tupe sababu ya kutwambia kwamba umeruka umekwenda kwengine kabla ya huku kumaliza wakati na huku umeahidi. Hii ni ahadi Mhe. Waziri umetupa hapa mwaka jana lakini ahadi yako haikutimia halafu hujatupa sababu. Barabara nyengine ya Amani/Mtoni, barabara hii tunaambiwa kila siku itajengwa na mfuko wa barabara lakini tunaona haimaliziki. Mhe. Waziri twambie kuna nini?

Mhe. Spika, baada ya hapo nataka kuzungumzia suala zima la bandari. Kwanza na mimi nichukue fursa hii kuipongeza serikali, Rais wa Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuweza kutupatia bandari nzuri na ya kisasa, bandari nzuri na ya kisasa. Kila anayekwenda pale anaridhika na bandari ile. Nimpongeze mfanyabiashara, Mzanzibari ambaye yeye kwa nguvu zake zote amejitahidi naye ni bwana Said Bakharessa ana haki ya kupongezwa.(*Makofi*).

Mhe. Waziri nakuomba sana katika hayo ambayo tunayozungumza tatizo letu kubwa tunakuwa na vitu vizuri lakini vile vitu tunakuwa hatujui kuvitumia, mara moja vinakuwa chakavu. Mhe. Waziri nakuomba sana Idara yako ya Bandari ijipange kwenye kuhakikisha kwamba bandari ile tunahifadhi, tunailinda ili tuwe nayo kwa muda mrefu.

Vile vile nilikuwa nataka kukuuliza kwa sababu huku kwenye kitabu chako umezungumzia suala zima la kununua *cranes* zile za bandarini. Mwaka juzi

kwenye bajeti ilikuwemo hiyo, sasa nilikuwa nataka kuuliza haya ma-*crane* ambayo tunayanunua inaonesha kila mwaka tunanunua haya. Je, yale ya zamani yapo na kama yapo utunzaji wake uko vipi? Yanatunzwa vizuri au ndio kila mwaka sisi tunanunua halafu haya mengine tunayapeleka kwenye vitu vilivyoharibika. Naomba na hili uje utupe maelezo.

Mhe. Waziri kidogo nilikuwa nataka kuzungumzia suala la hii jumuia ya madereva na utingo. Mhe. Spika, nimesikia malalamiko nimefuatwa kuna baadhi ya wawekezaji wa ndani wanasema sasa zile taratibu za ndani ambazo zilikuwa zifanywe na mamlaka yako zinafanywa na jumuia hii. Hii inaleta kuhangaishwa hawa wawekezaji. Mhe. Waziri utwambie kuna sheria gani inayowaruhusu hawa kama jumuia kuanza kushughulikia mambo ambayo haijawahusu. Hii inasababisha wengine wakashindwa kuwekeza, kwa sababu tayari wao wanawekewa vikwazo ambavyo vinasababisha wawekezaji wengine wanavunjika moyo. Mhe. Waziri nakuomba sana, uje utwambie huu utaratibu ambao pamoja na kupata leseni na kila kitu. Je, inafanywa na mamlaka yako au jumuia hii ndio inafanya.

La mwisho kabisa Mhe. Spika, na mimi naomba kidogo nizungumzie na hili limenigusa, nizungumzie suala zima la Uwanja wa Ndege. Mhe. Spika, inasikitisha sana kwa sababu hatujui lini tutafika, Uwanja wa Ndege umenivunja moyo na kila mtu hapa Zanzibar. Inasikitisha zaidi kwamba gharama za Uwanja ule wa Ndege na ujenzi wake kila siku zinazidi. Ametafutwa mtaalamu ambaye atatuelekeza. Huyu mtaalamu Mhe. Waziri uje utwambie zimetumika fedha ngapi za serikali kwa ajili ya kumlipa mtaalamu huyo. Tunasikia nje wanasema mtaalamu kalipwa fedha nyingi sana. Hivi hakuna wataalamu *local* ambao tuonaweza kuwatumia. Tuna vijana wetu wengi ambao wamesoma tayari wapo katika wizara hii wana utaalamu wa kutosha, basi tungechukua Tanzania Bara au Kenya, tumekwenda kuchukua Ufaransa *is very expensive*. Mhe. Waziri twambie kwa nini yametoka maamuzi hayo, wananchi wanalalamikia fedha zao. Mhe. Waziri tupe majibu.

La mwisho nataka kulizungumzia suala zima la maegesho ya *airport* ambalo wenzangu wengi wamelizungumzia. Wafanyakazi wa Mamlaka na wanaoingia *airport* kwa ajili ya kufanya kazi, walalamika kwa sababu kila wakiingia wanalipishwa. Sasa hawa tunajua wengi wao kipato chao ni kidogo mno, kwa nini wananyanyaswa hivi. Mtu kwa sababu amepelekwea kule kwa ajili ya kufanya kazi ataingia atalipa.

Mhe. Waziri hili suala lisimamie tena upya, ulisimamie uhakikishe hawa watu wanaondoka na hili, kwa sababu uwezekano wa kuwa wale wakawa na wizara zao zinaweza kulipa basi wapewe mamlaka yao ambayo imewanawapeleka pale walipe, tena walipe kodi ya jumla pale waingie kwa vibali, linawezekana

hilo. Sasa hivi *parking* imekuwa kila mtu anajaribu kutafuta pesa, lakini haya mambo yana tofauti. Utaratibu wa *parking* za wenzetu inakuwa kama mimi nikienda kuweka gari yangu pale nikikaa kutwa nzima kuna kodi yake, anayeingia na anayetoka kunakuwa kuna kodi yake, Jumamosi na Jumapili kuna kodi yake, *holiday* inakodi yake. Wenzetu ndio wanavyofanya sio kila anayeingia pale anatoa pesa hizo hizo, hilo haliwezekani. Mhe. Waziri tunakuomba sana hili ulifanyie kazi tuhakikishe kwamba wafanyakazi wetu kwa kweli hawaumii kwa suala la kutoa kodi pale wakati wanapokwenda kufanya kazi.

Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi kuchangia machache. Nasema hivi kwamba leo Mhe. Waziri utanisamehe swahibu wangu, leo naweka ngumu kwenye bajeti. Ninakushukuru sana Mhe. Spika, Mhe. Waziri nakutakia kila la kheri. Ahsante sana. *(Makofi).*

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe nadhani makofi haya mnataka tuendelee, mimi niko tayari. Waheshimiwa Wajumbe nikushukuruni kwa michango mbali mbali na mashirikiano makubwa ambayo mnaendelea kutoa katika kutekeleza shughuli zetu. Sasa niahirishe kikao hichi hadi kesho tarehe 01/08/2013 saa 3:00 za asubuhi.

(Saa 9:00 mchana Baraza liliakhirishwa hadi tarehe 01/08/2013 saa 3:00 asubuhi)